



USEMEZANO KATIKA DIWANI YA

SIKATE TAMAA

NA

DORCAS JEROTICH SUTER

TASNIFU YA UZAMILI

NOVEMBA 2017

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

Sahihi:..... Tarehe:.....

Dorcas Jerotich Suter

C50/73903/2014

Sahihi:.....

Tarehe:.....

Prof. Rayya Timammy

Sahihi:.....

Tarehe:.....

Bi. Mary Ndung'u

TABARUKU

Kwa babangu Micah Yano na marehemu mamangu Naomy Kangogo kwa kunipigania nipate elimu na kunilea. Pia kwa mume wangu Linus Tonui na mwanangu Abisha Kipkemoi kwa kuniunga mkono na kunipa msukumo na ari ya kusoma.

SHUKRANI

Utafiti huu si mchango wa mtu mmoja. Wengi walinishika mkono ili nifaulu. Hivyo sina budi kuwapa shukrani zangu za moyo za dhata.

Kwanza namshukuru Mola kwa kunipa uwezo wa kushughulikia kazi hii. Pili shukrani za dhata ziwaendee wasimamizi wangu Prof. Rayya Timammy na Bi. Mary Ndungu. Maelekezo yenu yalinifaidi sana. Tatu, wahadhiri walionifundisha: Prof. Habwe, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Mbatiah, Prof. Iribe Mwangi, Dkt. Amiri Swaleh, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Jerono na Dkt. Mbuthia. Kwao Maulana awazidishie maarifa na busara maishani.

Vile vile nawashukuru wanafunzi wenzangu ambao tuliabiri dau la masomo pamoja hadi ufuoni. Nao ni Sarah Kivuva, Virginia Wairimu, Lily Njagi, Tecla Kiptum, Jacklyne Bosibori, James Kimwea, Edward Lokidor, Wakesho Lonyce na Seraphine Kemuma. Wote nawaombea ufanisi katika kila hali aushini.

Sina budi kumpa kongole babangu na mamangu kwa kuhakikisha nimepata mwanga wa elimu na kunitia moyo daima nipige hatua mbele. Namshukuru mume wangu mwandani Linus Tonui kwa kunishika mkono si kwenye ndoa tu bali pia katika kupanda vidato vya elimu. Mola akujalie nyota ya jaha. Vile vile namshukuru mwanangu Abisha Kipkemoi kwa uvumilivu usiomithilika; Rabana akuinue maishani.

Nawashukuru kaka na dada zangu kwa kunichochea kuendelea masomoni licha ya changamoto nyingi. Joyce Jebet, Stephen Kipkorir, Amos Kipruto, Hosea Kiprono na Ruth Jepchumba kwenu Mungu awape heri aushini.

Sitasahau kuwashukuru walimu wangu Bw. John Nyongesa na Everylne Nyongesa kwa kunipa nasaha nitie bidii masomoni. Pia nampa heko Mike Sang kwa kuchochea ari ya kuendelea kusoma ndani yangu.

Pengine sikuweza kutaja kila mmoja aliyenifaa kwa njia moja au nyingine, kwenu nyote nasema asante. Pokeeni shukrani zangu.

IKISIRI

Katika tasnifu hii tumechunguza usemezano katika ushairi wa Kiswahili. Tumetumia diwani ya *Sikate Tamaa* (1980) kubainisha kuwa usemezano upo katika ushairi wa Kiswahili. Tumefanikisha haya kwa kutambua na kuchunguza vipengele vya usemezano vinavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili kwa ujumla. Tumetafiti vipengele kumi vya usemezano. Vipengele hivi ni: uzungumzi nafsia, tamko ni jibu kwa tamko lingine, utendaji, majibizano, usimulizi wa kisanaa, uwingi sauti, kumiliki sajili mbalimbali za lugha, kronotopu, kani pewa na kani kitovu na kanivali. Ilibainika kwamba usemezano upo katika ushairi wa Kiswahili. Pia tulibaini kuwa vipengele vya usemezano vimechangia katika ukuzaji wa maudhui ya mwandishi. Tulichunguza usemezano katika diwani ya *Sikate Tamaa*. Tulifanikisha haya kwa kuchunguza vipengele saba vya usemezano vinavyojitokeza katika diwani hii. Vipengele hivi ni majibizano au mjadala, matumizi ya shani kwa mujibu wa Bakhtin, lugha ya wahusika, usemi kuwa ni jibu la usemi, masimulizi ya moja kwa moja, kumiliki sajili mbalimbali vile vile uhusiano na matini zingine. Ilibainika kuwa vipengele vya usemezano vimechangia katika kufanikisha dhamira na maudhui kwenye diwani ya *Sikate Tamaa*. Tulichunguza namna ambavyo muktadha wa mazungumzo unavyoathiri mawasiliano baina ya wahusika katika diwani ya *Sikate Tamaa*. Tulifanya hivyo kwa kutafiti muktadha rasmi ambapo tulichunguza muktadha wa kiuongozi tukilenga shairi la “Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo” na muktadha usio rasmi ambapo tulijikita katika muktadha wa kitabaka, kifamilia, kutoleana wasia na muktadha wa umaskini. Tuligundua kwamba miktadha hii imeathiri mazungumzo katika diwani hii. Aidha tulitambua kuwa miktadha hii imeendeleza dhamira na maudhui.

YALIYOMO

UNGAMO	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI	iv
IKISIRI	v
UFAFANUZI WA ISTILAHU	x
FAFANUZI ZA VIFUPISHO	xi

SURA YA KWANZA	1
1.0 Utangulizi	1
1.1 Tatizo la Utafiti.....	2
1.2 Madhumuni ya Utafiti	2
1.3 Maswali ya Utafiti	3
1.4 Sababu za Kuchagua Mada.....	3
1.5 Upeo na Mipaka.....	4
1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada	5
1.6.1 Yaliyoandikwa kuhusiana na Nadharia ya Usemezano.....	5
1.6.2 Yaliyoandikwa kuhusiana na Mashairi katika Sikate Tamaa	14
1.7 Msingi wa Nadharia.....	19
1.7.1 Mihimili ya Nadharia ya Usemezano	23
1.8 Mbinu za Utafiti.....	24
1.9 Hitimisho	25

SURA YA PILI: VIPENGELE VYA USEMEZANO KATIKA USHAIRI WA

KISWAHILI	26
2.0 Utangulizi	26
2.1 Uzungumzi Nafsia	26
2.2 Tamko ni Jibu la Tamko Lingine	28
2.3 Utendaji	30
2.4 Majibizano	32
2.5 Usimulizi wa Kisanaa	34

2.6 Uwingi Sauti	36
2.7 Sajili Mbalimbali	36
2.8 Kronotopu	36
2.9 Kuwa Na Kani Pewa Na Kani Kitovu	37
2.10 Kanivali	37
2.11 Hitimisho	37
SURA YA TATU: USEMEZANO KATIKA DIWANI YA SIKATE TAMAA	39
3.0 Utangulizi	39
3.1 Majibizano	39
3.1.1 Mwanakupata	40
3.1.2 Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo	41
3.1.3 Imani ya Mwana	42
3.2 Dhana ya Shani kwa Msingi wa Bakhtin	44
3.2.1 Watu Hawajali	45
3.2.2 Watoto wa Afrika	46
3.2.3 Si Dunia ya Kulala	47
3.2.4 Wananambia Mchafu	48
3.2.5 Ajabu	49
3.2.6 Chui wa Kufuga	50
3.3 Sajili Mbalimbali	51
3.3.1 Sajili ya Biashara (Dukani)	51
3.3.2 Sajili ya Matangazo	52
3.3.3 Sajili ya Siasa	52
3.4 Lugha ya Wahusika	53
3.4.1 Sikate Tamaa	53
3.4.2 Nawaita Washairi	54
3.5 Usemi Kuwa ni Jibu la Usemi	54
3.6 Masimulizi ya Moja kwa Moja ya Kifasihi	55
3.6.1 Methali	56
3.6.1.1 Uungwana Sambe ni Jadi Kubeli	56

3.6.1.2 Si Kupanda Ngazi, Usijali Kushuka Chini.....	57
3.6.1.3 Damu Haiwi Maji.....	57
3.6.1.4 Hujipalia Makaa.....	58
3.6.1.4 Ni Firauni wa Kweli, Utayaona Mageni	58
3.7 Uhusiano na Matini Zingine	58
3.7.1 Mtu Hachagui Kazi.....	59
3.7.2 Ndoto	61
3.8 Hitimisho.....	62
SURA YA NNE: ATHARI ZA MUKTADHA KATIKA MAZUNGUMZO.....	63
4.0 Utangulizi	63
4.1 Mukstadha wa Kijamii	63
4.1.1 Mukstadha wa Kifamilia.....	63
4.1.2 Mukstadha wa Kitabaka.....	66
4.1.2.1 Mwanakupata.....	66
4.1.2.2 Nilipokwenda Dukani	67
4.1.2.3 Chui wa Kufuga	68
4.1.3 Mukstadha ya Kimaskini	68
4.1.3.1 Nilipokwenda Dukani	68
4.1.3.2 Mwanakupata.....	69
4.1.4 Mukstadha wa kutoleana wasia (Mawaidha).....	70
4.1.4.1 Imani ya Mwana	70
4.1.4.2 Muhali	71
4.1.2.3 Nawaita Washairi.....	71
4.1.2.4 Mtu Hachagui Kazi.....	72
4.1.2.5 Sikate Tamaa.....	72
4.2 Mukstadha wa Kiuongozi	73
4.2.1 Mukstadha wa Kikoloni na Kikoloni Mamboleo.....	73
4.2.1.1 Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo.....	74
4.3 Hitimisho.....	75

SURA YA TANO: HITIMISHO, MATOKEO YA UTAFITI NA MAPENDEKEZO	76
5.0 Utangulizi	76
5.1 Hitimisho	76
5.2 Kuhusu Madhumuni Yetu	77
5.3 Matokeo Kuhusu Maswali ya Utafiti	78
5.4 Mapendekezo.....	79
6.0 MAREJELEO	80

UFAFANUZI WA ISTILAHU

- Nadharia:** Ni mwongozo uliopangwa ili kusaidia kuelezea, kutatua au kutekeleza jambo fulani.
- Usemezano:** Ni usemi ujidhihirishao baina ya nafsi mbili. Ni mtagusano unaohusu zaidi ya nafsi mbili zinazobadilishana kauli.
- Shani:** Ni dhana ambayo imetumika kurejelea jumla ya mambo ambayo yanakiuka miiko na mbeko za kibinadamu. Mambo haya yangukuwa ya kufedhehesha laiti yangekengeushwa na miktadha mahususi ya kijamii ambamo yanapatikana.
- Majadiliano:** Istilahi hii, kimsingi inahusu masemezano kati ya watu wawili au vikundi viwili vya watu. Katika kazi hii, majadiliano si lazima yawe ya ana kwa ana. Badala yake, yatarejelea hali ya kuwepo kwa usemi ambao unajibu usemi wa awali huku ukitarajia jawabu kutoka kwa usemi utakaofuata.
- Uhakiki:** Kauli yenye mantiki anayotoa msomaji kuifafanua kazi ya fasihi. Ni utoaji wa hukumu au uamuzi kuhusu kazi yoyote ya kisanaa.
- Sajili:** Ni matumizi ya lugha yanayokwenda na mukhtadha maalum. Ni mitindo mbalimbali ya lugha.
- Msemeza:** Anayetoa habari au mzungumzaji.
- Msemezwa:** Anayepokea habari au anayezungumziwa ama anayesikiliza.
- Kronotopu:** Matukio yanayotimbwa katika mpito wa wakati na mahali.
- Toni:** Hii ni dhana inayotumiwa kuelezea mwelekeo wa kihisia alionao mwandishi wa kazi hiyo au unaotokana na kazi yenyewe.
- Usimulizi:** Ni uelezaji wa tukio moja au mengi ya kihalisi au kibunilizi.
- Usambamba:** Ni istilahi inayotumiwa kuelezea ule urudiaji wa muundo sawa au ruwaza sawa ya kisintaksia katika virai, vishazi au sentensi.
- Uzungumzi nafsi:** Ni dhana inayotumiwa kurejelea hali ambayo mtu anazungumza na nafsi yake.

FAFANUZI ZA VIFUPISHO

T.Y – Tafsiri yangu

Uk – Ukurasa

Ub – Ubeti

TANU- Tanzania African National Union

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi

Katika utafiti huu, tunashughulikia Usemezano katika *Sikate Tamaa* (1980). *Sikate Tamaa* (1980) imeandikwa na mwandishi anayesifika Said Ahmed Mohamed Khamis. Mwandishi huyu amechangia kuendeleza fasihi ya Kiswahili kwa kiasi kikubwa sana.

Usemezano ni hali ambapo mtu mmoja anazungumza na mhusika mwingine. Usemezano unajitokeza katika hali ya kawaida ya binadamu hasa binadamu anapotagusana. Huonekana katika mawasiliano ya kila siku kwa sababu kuna msemaji na msemewa; hili linadhihirika kupitia kwa ishara vitendo na ishara tamkwa. Ishara hizi zinaboresha uelewa au maelewano kati ya msemzwa na msemaji. Mawasiliano katika jamii kwa ujumla hufanikiwa wakati binadamu anapobadilishana kauli na binadamu mwenzake. Haya huonekana kunapokuwa na nafsi mbili zinazosemezana yaani nafsi neni anayetoa matamshi na mnenewa anayepokea matamshi hayo au ishara hizo. Vile vile usemezano hudhihirika mtu anaposema na nafsi yake.

Hali ya kubadilishana usemi hujitokeza katika mazungumzo na maandishi. Katika mazungumzo huonekana wakati watu wanapoonana ana kwa ana au wanapokuwa katika sehemu zinazokaribiana kiasi kwamba wanaweza kusikilizana. Pia wanapotumia simu kuwasiliana. Katika maandishi hutokea wakati ambapo mwandishi amewasawiri wahusika wawili au zaidi wakiwa katika hali ya mazungumzo hususan kuhusu maswala mbalimbali yanayozunguka ulimwengu wao au anapomchora mhusika mmoja akizungumza na nafsi yake.

Lugha ni muhimu katika mazungumzo. Hii ni kwa sababu ndiyo malighafi ya mawasiliano na huboresha mawasiliano zaidi hasa kwenye uwanja wa fasihi. Usemezano hujitokeza katika riwaya, tamthilia na ushairi. Katika riwaya usemezano huonekana pale ambapo mtunzi amewachora wahusika wake wakiwa katika maongezi ya kawaida au wakizungumza faraghani; dhana hii inarejelea mazungumzo kati ya wanadamu. Kwenye tamthilia hudhihirika pale ambapo mwandishi amewasawiri wahusika wake wakiwa kwenye mjadala au wakiwa katika majibizano. Utafiti huu unajikita katika kuchunguza kuwepo kwa maongezi au mjadala katika ushairi. Hili hubainika wakati ambapo kuna usimulizi wa kisanaa wa moja kwa moja ufanywao na mwandishi na pia

usimulizi huu unapofanikisha ukuzaji wa dhamira na maudhui ya mtunzi. Haya yanabainika katika diwani ya *Sikate Tamaa* kwa kiasi kikubwa na katika mashairi mengi kwa mfano kwenye shairi “Nawaita Washairi” (uk. 3) ambapo mwandishi anawasemesha wasomaji (watunzi) kuwa waandike kwa ari mashairi kiufundi na waache mashindano.

1.1 Tatizo la Utafiti

Katika utafiti huu tunachunguza jinsi vipengele vya usemezano vinadhihirika katika mashairi ya Said Ahmed Mohamed kwenye diwani ya *Sikate Tamaa* (1980) na namna vipengele hivi vinafanikisha dhamira na maudhui. Vipengele hivi humwezesha msomaji kuelewa au kufahamu kinachowasilishwa na mwandishi. Hii ni kwa sababu hivi vipengele humsaidia atakayesoma kazi hii kupokea habari iliyokusudiwa. Mifano ya vipengele hivi ni kama vile kuwepo kwa maongezi ya kisemezano, athari zinazopatikana kutokana na matamshi ya msemaji na msikilizaji, kuwepo kwa majibizano kati ya wahusika na matamko ya ki-uzungumzi nafsia. Hivyo tunaangalia namna vipengele hivi tulivyoviorodhesha vinavyotumika katika mashairi mbalimbali katika diwani ya *Sikate Tamaa*.

Usemezano una umuhimu katika kufanikisha mawasiliano katika ushairi wa Kiswahili. Mawasiliano katika ushairi hufaulu pale ambapo kuna kubadilishana usemi baina ya msemaji au nafsi inayotoa usemi na msikilizaji au nafsi inayopokea usemi. Mawasiliano ya aina hii huweka wazi dhamira na maudhui. Katika kufanikisha haya, utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Usemezano iliyoasisiwa na mhakiki wa Kirusi Mikhail Bakhtin (1895-1975).

1.2 Madhumuni ya Utafiti

- (i). Kuainisha vipengele vya usemezano katika ushairi wa Kiswahili.
- (ii). Kutathmini namna muktadha wa mazungumzo unavyoathiri mawasiliano kati ya wahusika wanaowasiliana katika diwani hii. Mfano, muktadha rasmi, usio rasmi na muktadha wa kutoleana wasia.
- (iii). Kuchunguza jinsi vipengele vya usemezano vinakuza dhamira na maudhui katika diwani ya *Sikate Tamaa*. Mfano ni kama vile usimulizi wa kisanaa wa moja kwa moja ufanywao na mwandishi.

1.3 Maswali ya Utafiti

- (i). Je, ni vipengele vipi vya usemezano vinavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili?
- (ii). Je, muktadha wa mazungumzo unaathiri vipi mawasiliano kati ya wahusika wanaowasiliana katika diwani ya *Sikate Tamaa*?
- (iii). Je, vipengele vya usemezano vinakuza vipi dhamira na maudhui katika diwani ya *Sikate Tamaa*?

1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Suala lililotuchochea katika utafiti huu ni kudhihirisha kuwa usemezano upo katika ushairi wa Kiswahili. Hili linajadiliwa na kuwekwa wazi katika utafiti huu kinyume na maelezo ya mwitifaki mkuu wa Nadharia ya Usemezano Mikhail Bakhtin ambaye ametwaza riwaya na kuutweza ushairi. Bakhtin alisifu sana riwaya akisema lugha yake ni wazi inayokubali mwingiliano wowote na inayochanganya sajili zote kwa pamoja na kukashifu ushairi kuwa lugha yake ni ya kizamani na kuwa mwandishi ndiye asemaye tangu mwanzo hadi mwisho na maudhui yake yamepitwa na wakati (Bakhtin;1981:13-16).

Tumeamua kushughulikia mada hii ili kuonyesha jinsi vipengele vya usemezano vinavyofanikisha mawasiliano katika ushairi wa Kiswahili hususan katika mashairi teule ya *Sikate Tamaa*. Jambo lingine ni kuwa, utafiti huu umeweka wazi kwamba usemezano ni muhimu katika kuchangia au kujenga dhamira na maudhui katika ushairi wa Kiswahili. Tumejikita katika mada hii vile vile kwa kuwa ni njia ya kukuza utafiti wa Kiswahili ili wasomi wa baadaye wapate kufaidika kutokana na matokeo yake.

Tumechagua mada hii pia kutokana na pendekezo la mtafiti Murithi (2002), aliyechunguza usemezano katika Tamthilia za Kiswahili. Alifanya haya kwa kuhakiki: *Mashetani* (1971), *Kilio cha Haki* (1981) na *Amezidi* (1995). Yeye alitoa pendekezo kwamba utafiti zaidi unahitajika kufanywa ili kutafiti iwapo usemezano unaweza kupatikana katika mashairi ya Kiswahili na kuchunguza namna usemezano huo unavyojitokeza.

1.5 Upeo na Mipaka

Said Ahmed Mohamed ni mwandishi wa kazi nyingi tofauti zikiwemo riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Mohamed pia ameandika kazi nyingi za ushairi lakini utafiti huu umejifunga katika kushughulikia usemezano kwenye diwani ya *Sikate Tamaa*. Hii ni kwa sababu mashairi katika diwani hii yameonyesha umahiri wa mwandishi katika kuvyaza mbinu mbalimbali za kibunifu. Mtunzi ameibuka na mbinu tofauti katika ushairi wake. Tunajikita katika mashairi kumi na manane tu kati ya mashairi arubaini na manne yaliyoandikwa kwenye diwani hii kwa sababu ndiyo mashairi yanayotupa data lengwa tunayohitaji kuchunguza. Mashairi haya ni: “Sikate Tamaa”, “Watoto wa Afrika”, “Si Dunia ya Kulala”, “Nawaita Washairi”, “Siku Njema”, “Wanambia Mchafu”, “Ajabu ”, “Watu Hawajali”, “Ukoloni na Ukoloni Mambo–Leo,” “Nilipokwenda Dukani”, “Mtu Hachagui Kazi”, “Ndoto”, “Chui wa Kufuga “Imani ya Mwana”, “Mwanakupata”, “Ungwana ”, “Huba kwa Wazee Wangu” na “Muhali”. Tumetumia nadharia ya usemezano kwa sababu ndiyo mwafaka katika kutazama usemezano uliopo katika mashairi haya pia kuipa nguvu nadharia hii katika kuhakiki mashairi ya Kiswahili. Tumejikita katika usemezano wa kawaida ambapo wahusika wawili wanabadilishana mawazo na usemezano ambao waandishi wanasemezana kupitia tungo zao.

Nadharia ya Usemezano ina vipengele kumi na vitatu kama vile: uzungumzi nafsia, utendaji, majibizano kati ya wahusika wawili au vikundi viwili, uwingi lugha, dhana ya shani kulingana na Bakhtin, kronotopu, kuwa na kani pewa na kani kitovu, kanivali, kumiliki sajili nyingi za lugha, lugha ya wahusika, tamko kuwa jibu la tamko, uhusiano na matini zingine na usimulizi wa kisanaa. Kati ya vipengele hivi, tumeangazia vipengele saba tu. Navyo ni majibizano baina ya wahusika wawili, kumiliki sajili nyingi za lugha, masimulizi ya kisanaa, matumizi ya shani, lugha ya wahusika, usemi kuwa jibu la usemi na uhusiano na matini zingine. Tumechagua vipengele hivi saba kwa kuwa vimetutosheleza katika utafiti huu. Isitoshe hivi ndivyo vinadhihirika katika diwani ya *Sikate Tamaa*.

1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Sehemu hii imeshughulikia masuala mawili. Kwanza yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya usemezano ambapo tumetoa mawazo ya wataalamu mbalimbali na pili yaliyoandikwa kuhusu diwani hii ya *Sikate Tamaa*. Kuhusu diwani hii, tumeeleza yaliyochunguzwa na watafiti wengine waliotangulia, matokeo ya tafiti zao na namna ambavyo tafiti hizo za mwanzo zilivyotufaidi katika uchunguzi wetu.

1.6.1 Yaliyoandikwa kuhusiana na Nadharia ya Usemezano

Sehemu hii imeshughulikia yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya usemezano kulingana na kauli za wataalamu mbalimbali na namna ambavyo kauli zao zimetufaidi katika uchunguzi wetu. Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa usemezano ni dhana ambayo inatokana na kiarifa ‘kusemezana’. Istilahi ‘usemezo’ ilitumika kabla ya istilahi ‘usemezano’ kuundwa. Baada ya majadiliano marefu iliamuliwa kwamba istilahi iliyoafiki ni ‘usemezano’.

Wamitila (2002:152) anasema usemezano ni dhana inayorejelea mazungumzo kati ya binadamu na hasa kama maongezi hayo yakiwa yameandikwa. Mazungumzo hayawezi kutimia bila ya kuwako kwa lugha ambayo ina sifa ya kusemezana. Bakhtin (1986) alisema kwamba lugha huwa ina sifa za kusemezano. Kulingana naye kanuni ya usemezano ina umuhimu kabisa, fauka ya kuchochea hutamalaki katika uandishi wowote.

Fikra za Bakhtin (1981) zinaelekeza dhana ya usemezano katika kiwango cha binadamu, kinachochochea kuwaza. Yeye anasema, mawazo ya mtu huwa mawazo ya kweli iwapo tu yatapatana na mawazo ya mtu mwingine; yaani mawazo ya mtu tofauti.

Ingawa mengi sana kuhusu usemezano hayajasemwa katika ushairi hususan kwenye *Sikate Tamaa*, mengi yameandikwa kuhusu dhana hii katika kazi zingine. Kuna waandishi ambao wameandika mengi kuhusu usemezano mfano kwa kuangalia riwaya.

Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007), kinadharia Bakhtin alijihusisha sana na sajili ya riwaya kuliko tanzu nyingine za fasihi. Kutokana na utafiti wake alifafanua riwaya za kimonolojia na riwaya za kipolifoni. Kwa mujibu wa Bakhtin (1986), kazi za fasihi ni uwanja ambao una

mwingiliano wa matini. Kazi za kifasihi zina sauti mbalimbali zilizotangulia, zilizopo au zitakazotokea baadaye. Anasema mwingiliano huu ni wa kiusemezano. Katika baadhi ya riwaya za kimonolojia, kuna uhusiano wa karibu kwa mfano uhusiano uliopo kati ya hadithi kama vile *Adili na Nduguze* na *Alfu-Lela Ulela*. Hali kadhalika inadhihirika pia kuwa kuna mwangwi wa *Nyota ya Rehema* (M.S. Mohamed) katika *Utengano* (Said A. Mohamed).

Bakhtin (1981), ambaye ndiye mtaalamu mkuu wa nadharia hii, anafafanua katika kitabu hiki tofauti zilizopo baina ya utendi na riwaya. Mawazo yake yanaonyesha waziwazi kuwa riwaya ndiyo utanzu bora zaidi kuliko tanzu nyinginezo. Hii ni kwa sababu, riwaya ina lugha iliyo hai kuliko utendi. Anaongezea kwa kusema kuwa riwaya inashinda tanzu nyingi kwa kuwa lugha yake haifungwi na kujitenga na lugha nyingine. Lugha ya ushairi imefinyika na kufungika na zaidi ya hayo inazingatia uhafidhina kiasi kwamba haikubali athari zozote kutoka lugha zingine zinazozungumzwa katika jamii.

Bakhtin (1986) anaeleza kuhusu suala la sajili za lugha. Kulingana naye anaonelea ya kuwa matamshi yako katika sajili. Hivi kwamba matamshi yana mitindo iliyojimakini yenye kudhihirika wakati wa matumizi. Kulingana naye, mtu hujifunza kuzungumza kwa mitindo hiyo pindi tu anapomsikia mtu mwingine akisema. Katika mkabala huu wa matamshi ambayo yana mtindo maalum ndipo Bakhtin anatoa maelezo bayana baina ya tamko na sentensi. Anasema kuwa sentensi jinsi ilivyo ni kavu na haiwezi kutoa maana yoyote inayoeleweka. Hii ni kwa kuwa sentensi hujiepusha na muktadha na mazingira ambayo ilitumiwa. Yaani inajitenga na kujiweka peke yake. Hata hivyo kwa maoni ya Bakhtin, tamko ndilo kipashio cha pekee katika lugha kinachoandamana na viimbo vinavyobainisha maana katika tamko hilo.

Morson (1986) ambaye ndiye mhariri wa kitabu cha Bakhtin ambacho kimekusanya makala kadha wa kadha yaliyoandikwa na waandishi wengine kuhusu Bakhtin, anasema kuwa wazo kuu la Bakhtin ni kwamba watu katu hawatamki neno la mwisho bali hutamka lile la pili kutoka mwisho. Hii ni kwa kuwa ubinadamu unajulikana kwa “kutokwisha” kwake (1986:vii). Hili ni kwa sababu kila tamko ni jibu la tamko lingine na katika mfuatano huu huu wa majibu ndio kutomalizika kwa matamshi kwapatikana. Maelezo haya ya Morson yanatufaa katika utafiti wetu kwa kuwa yametuwezesha kufahamu kuwa matamshi hayatakwisha na hivyo basi hata kama *Sikate Tamaa*

iliandikwa mwaka wa themanini bado mashairi katika diwani hii yanawahamasisha watunzi wengine. Wao pia hujibu kwa njia yoyote kwa mfano kukubaliana nalo au kulipinga.

Holquist ni mtaalamu ambaye amemtafiti kabisa Bakhtin na kuangazia mawazo yake katika uwanja wa uhakiki wa fasihi. Vitabu vyote vya Bakhtin vilivyotajwa hapo juu vimepatikana kutokana na bidii za Holquist ambaye amevifanyia uhariri mwema baada ya kutafsiriwa kutoka Kirusi. Holquist (1990) anakubali kwamba lazima matini zote ziwe zinahusiana japo anasisitiza kuwa ni riwaya pekee ndizo ambazo zinatumiwa kuathiriana ili zipate kubakia. (Holquist 1990:89). Kwa ufupi anagusia suala la historia katika usemezano na kudhihirisha umuhimu wa historia katika kuelewa maana ili kufaidika na kazi za fasihi. Hili linaupa nguvu utafiti huu ambapo historia ya uandishi wa Said Ahmed Mohamed inatiliwa maanani hadi pale ambapo alijiingiza katika uandishi wa ushairi.

Fischer na Abedi (1990) waliandika makala juu ya usemezano katika *Qurani*. Muktdha wa maneno yao ulikuwa kuangazia jinsi kazi za Kiislamu zinavyomulika siasa kwa waislamu. Wanasema ya kuwa ukwasi wa usemezano huu unadhihirishwa kwa mifano ya usambamba, urejelezi, marudiorudio na mabadiliko ambayo yametapakaa katika *Qurani* nzima (uk 133). Hata ingawa Fischer na Abedi hawakujishughulisha na ushairi wa Kiswahili, ufafanuzi wao kuhusu mifano ya usemezano katika Qurani umetufaidi katika utafiti huu kwa kuelewa usemezano zaidi. Huku kurudiarudia kwa njia ya usambamba na urejelezi kunapatikana pia katika diwani hii. Mifano ni kwenye mashairi kama vile, “Sikate Tamaa” (uk. 1), “Wananambia Mchafu” (uk. 7) na “Sema.” (uk. 14). Tofauti ni kuwa, utafiti huu umefanywa kwenye Qurani huku utafiti wetu umelenga diwani ya *Sikate Tamaa*.

Bennett (1990) alipokuwa anafafanua juu ya sajili, hakusahau kumtaja mtunzi Bakhtin na kuelezea mawazo yake kuhusu ushairi. Kwake Bakhtin, tanzu bora zaidi ni riwaya. Hata hivyo Bennett anatilia shaka suala la kwamba utanzu huu wa riwaya ukishatangaa na kuanza kuathiri kazi zingine katika matumizi yao ya lugha, je haitakuwa kwamba kazi zingine zitabadilika na wala sio vile vile kubakia vile vile kama alivyodai Bakhtin? Anashikilia kuwa ikiwa riwaya ina sifa za kutokuwa na tamati na ni wazi katika kupokea mabadiliko, basi na kazi zingine pia zitafuata mkondo huu huu wa mabadiliko na vivyo ushairi. Kauli hii ya Bennett inaupa utafiti huu nguvu kwa kuyakinisha kuwa tungo za ushairi zinaendelea vile vile kubadilika kama ilivyo riwaya. Mawazo haya yanaonekana pia katika diwani tunayoichambua ambapo mtunzi ameonyesha kuwepo kwa

mabadiliko kwenye ushairi kwa kuvyaza mbinu mbalimbali ili kufanya ushairi uvutie zaidi. Mashairi mengi kwenye diwani yake yanadhihirisha ubunifu mwingi wa kisanaa kama vile “Mbele ya Safari” (uk. 10) shairi ambalo kibwagizo kimefupishwa.

Grogan (1989) alipokuwa anatafiti ushairi wa W.S Graham, alitumia vigezo na maelezo yale yale ya Bakhtin kuthibitisha kuwa ushairi pia umo katika usemezano. Anasema kwamba binadamu hakuwako kabla ya kuwako binadamu mwingine hivyo basi lugha haikuwako kabla ya mazungumzo kuwako. Lugha inaweza kuwa uzungumzi wa mtu mmoja pindi mazungumzo yanapokatika au yanapovunjika. Kutokana na ufafanuzi huu ni dhahiri kuwa mwanadamu alianza kujihisi kama mwanadamu wakati alipokuwa na mwenzake na vivyo hivyo lugha ipo katika usemezano kwa kuwako maongezi. Basi ikiwa lugha ni usemezano na ushairi ni vivyo hivyo. Yaani shairi ni usemi na “yeye”, popote atakapokuwako mshirika huyu. Haya yanaonekana kwenye diwani ya Said Ahmed katika shairi “Mwanakupata” (uk. 36) ambapo kuna mshirika msemewa ambaye ni Mwanakupata, msemaji anayetoa usemi ambaye ni Mwhija na vile vile kuna msomaji ambaye anasemewa anaposoma shairi hili. Grogan (1989) anafikia tamati kwa kusema kuwa ushairi wote sio kitu cha kutia katika fikira pekee bali ni mwito baina ya mnenaji na mnenewa. Haya yanaonekana kwenye shairi “Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo” (uk. 20) ambapo Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo wanasemwana kuhusu utawala. Maelezo haya ya Grogan yanatufaa kwa kuwa kupitia kwa utafiti wake tumefahamu kwamba ushairi upo katika usemezano. Uchunguzi huu ni tofauti na wetu kwa kuwa Grogan alijishughulisha na ushairi wa W.S. Graham nasi tunajikita katika *Sikate Tamaa*.

Mukarovsky (1977) alitanguliza kwa kutoa tofauti iliyopo baina ya usemezano na uzungumzi wa mtu mmoja. Katika sehemu ya uzungumzi wa mtu mmoja, anasema kwamba kiisimu humaanisha yale maneno ya mtu mmoja tu bila kutilia maanani kuwako kwa mazungumzo hayo. Yeye anatoa sifa tatu za usemezano teule; sifa hizi zinatokana na mahusiano yaliyo baina ya wahusika wawili. Wahusika hawa hutambuana kama “mimi” na “wewe” na wakati wa maongezi yao majukumu ya mnenaji na mnenewa hubadilishana mara kwa mara. Isitoshe kuna mahusiano ya washiriki wa mazungumzo na mazingira waliyomo. Mazingira haya yanaathiri moja kwa moja mwelekeo wa maongezi au huyaathiri kwa mbali wakati mazingira yanapokuwa maudhui ya mazungumzo. Uhusiano wa tatu ni ule wa muktadha wa usemezano. Muktadha hueleza taratibu za maana ambazo huonyeshwa kwa urejelezi tofauti katika maongezi. Kama vile kwenye “Imani ya Mwana” (uk.30),

panaonekana kuwa mazingira ni maudhui ya mazungumzo. Mwana anapozungumzia madhila ya babake nyumbani na mateso ya mama.

Njogu (1993) anapinga, kwa ithibati, nadharia ya Bakhtin ambayo imesisitiza kuwa riwaya ndiyo tanzu bora na kuutweza ushairi kwa kudai kuwa ni uzungumzi wa mtu mmoja. Yeye anaonyesha kuwa usemezano unaweza kuwepo katika ushairi wa fasihi simulizi. Anafaulu kuonyesha kuwa ushairi ni wa kisemezano. Uthibitisho wake umetokana na ushairi wa Afrika Mashariki, ushairi ambao ulihusisha ushairi wa gungu, gicaandi na kimondo. Kwa kutumia ushahidi, Njogu aliweza kuonyesha jinsi tungo hizi zidhihirishavyo vipengele vya usemezano. Hivyo basi kulingana na Njogu, sifa zote zinazopewa riwaya, zinapatikana katika ushairi pia. Licha ya kuwa Njogu alijishughulisha sana na ushairi simulizi, yeye ameangazia ushairi andishi pia ijapokuwa kwa uchache, haswa ushairi wa Kiswahili, wa Kikikuyu, mashairi ya Hassan Bin Ismail na Abdilatif Abdalla. Aidha Njogu alionyesha japo kwa ufupi sana usemezano katika *Al-Inkishafi* (Njogu 1993:92). Uchunguzi huu umetufaa katika kuelewa kwa kushirikisha wahusika katika kuuliza maswali, kujibu, na kuyatenda mambo jinsi usemezano unavyohitaji. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa kuwa Njogu ametafiti kuhusu ushairi simulizi wa gicaandi na kimondo ilhali uchunguzi wetu umelenga usemezano katika diwani ya *Sikate Tamaa*.

Karama (1996) katika tasnifu yake, '*Ushahidi wa usemezo katika Al-Inkishafi*', ameonyesha kipengele kimojawapo cha nadharia ya Usemezano, nacho ni kuwepo kwa kuathiriana na maandishi mengine. Karama alidhihirisha haya kwa kuonyesha kuwa kuna mwangwi wa *Al-Inkishafi* katika *Tabaraka Dhul Ulaa* iliotungwa na Hujjatul Din Muhammad bin AbdulAziz Al-Waraq. *Al-Inkishafi* ilioandikwa na Sayyid Abdalla na *Tabaraka Dhul Ulaa* zimeathiriana. Kazi hizi mbili zimeingiliana na kutegemeana.

Kwa mujibu wa Karama tendi hizi mbili zaonekana kufanana kwa kuwa mianzo yao haikosi kulitaja jina la Mwenyezi Mungu. Katika ubeti wa kwanza wa *Tabaraka*, mwandishi Al-Waraq hakuanza na utajo wa neno bismilahi kama vile alivyofanya Sayyid Abdalla bali alianza kwa kumsifu Mwenyezi Mungu, ambayo pia ni tafsiri nyingine ya "himdi", ambayo kwa maelezo ya maneno marefu tafsiri yake ni "kila jinsi ya sifa njema zamstahiki Mwenyezi Mungu" na baada ya kutoa shukrani zake, yeye anaanza tena kutaja utukufu wa Mwenyezi Mungu.

Katika dibaji ya utendi wa *Inkishafi*, Sayyid Abdalla anasema;

7. Makusudi yangu ya kudhamiri
Nda kutunga koja kilidawiri

8. Na ina nikite *Inkishafi*
Kiza cha dhunubu kiniukiye

Katika *Tabaraka*, mwandishi ana maelezo kama haya. Anasema;

66. Nimetoa kwako naswada nayo ndiyo kusudio langu
Shikamana katika mambo na yale ambayo yanapelekea

Kwenye njia za salama na kuokoka.

Katika beti hizi mbili ambazo zimedondolewa, wazo linalojitokeza ni kuwa kila mwandishi alitaka kusema kwa kauli yake dhamiri ya kuandika utendi wake. Inadhihirika kwamba dhamira kuu ya kuandika tendi hizi mbili ni nasaha ya kutaka umma uokoke, yaani umma usalimike na mateso ya humu duniani na kesho akhera. Hivyo basi tendi hizi mbili zaonekana kufanana kwani *Al-Inkishafi* na *Tabaraka Dhul Ulaa* zimeathiriana.

Karama vile vile ameangazia majibu ya usemezano; akilenga *Al-Inkishafi* anasema kwamba katika usemezano majibu haswa ambayo mtu anapata ni ule msisimko wakati tamko fulani linapotamkwa. Msisimko huu mara nyingi unaweza kuwa wa kupinga au kutolea rai, au hata kuzidisha nguvu. Mtu asipojibu kwa kutamka, ukimya ule wa msemzwa vile vile hutafsiriwa na msemzwa kuwa ni jibu. Hii ni kwa kuwa jibu si sharti litolewe papo kwa hapo walakini hata kama jibu hilo likiachwa mpaka baadaye, huo mshawasha alioupata msemzwa bado utachukuliwa kuwa ni jibu. Ni kutokana na majibu basi ndio dhana ya usemezano inajidhihirisha au kujitokeza. Haya yanaonyesha kuwa matamshi yote yako katika usemezano. Hata kama mhusika ndiyo tu anaanza kutamka, matamshi yake hayatokani na ombwe tupu ila kuna aliyemtangulia katika kusema, ikiwa sio leo na si juzi, ni siku nyingine yoyote. Hakuna binadamu yeyote ambaye anaweza kudai kuwa anaweza kusema kwamba tamko fulani yeye ndiye wa kwanza kulisema, chambilecho Bakhtin (1981:279).

Yeye anadai kwamba, *Inkishafi* ni jibu la Sayyid Abdalla kwa umma ambao ulikuwapo wakati huo na wa siku ambazo zitakuja. Ni mshawasha kwa kuwa kabla yake, kulitanguliwa na tendi nyingine ambazo zilikuwa maarufu kama jinsi ulivyo utendi wa *Al-Inkishafi* hivi leo. Mifano ni *Swifa ya Mwana Munga* (1517) na *Hamziyya* (1652). Utafiti huu ni muhimu katika uchunguzi wetu kwa kuwa umetuwezesha kufahamu kauli za Bakhtin vyema kama vile kuathiriana kwa matini. Hata hivyo uchunguzi huu ni tofauti na utafiti wetu kwa sababu umeangazia usemezano katika *Al-Inkishafi* huku wetu ni usemezano katika diwani ya *Sikate Tamaa*.

Bakari (2008) ameangazia uwili wa usemi na jinsi unavyotatua matatizo ya uelewaji na usadikifu wa hadithi au kazi za kiuhalisiajabu. Ameangazia sauti ya Proteus na K. Anasema kwamba K alipofufuka upya aligeuza sauti ya Proteus kiasi kwamba wote wakawa wanazungumza. K naye alipochaguliwa kuwa kiongozi, naye aligeuza tabia zake na kuwa zimwi. Vilevile Bakari ameangazia mwingiliano wa matini. Ametaja kisasili cha Proteus na kuonyesha kwamba kuna mwangwi wa *Babu Alipofufuka* (2001) katika *Bina-Adamu* (2002) kwa kuwa waliochaguliwa kama viongozi katika riwaya ya *Bina-Adamu* wanakuja kuwa mazimwi wa leo wanaokuja kuwajeruhi waliowachagua. Haya yanaonekana pia katika *Babu Alipofufuka* wakati ambapo mhusika K alipochaguliwa kuwa kiongozi naye pia akaja kuwa zimwi kwa kuwatesa wanajamii. Mawazo haya ya Bakari yanatusaidia kuelewa zaidi kuhusu vipengele vya usemezano kwa mfano tumeweza kuelewa namna ambavyo uwili lugha unavyojitokeza katika kazi ya fasihi na mwingiliano matini. Utafiti wake ni tofauti na wetu kwa kuwa umeshughulikia riwaya za Kiswahili huku utafiti wetu unaangazia ushairi wa Kiswahili.

Murithi (2002) alifanya utafiti kuonyesha namna usemezano unavyojitokeza katika tamthilia kadhaa na kuangazia namna mihimili ya nadharia ya usemezano ilivyojitokeza. Katika uchunguzi wake alionyesha kuwa usemezano upo katika tamthilia za Kiswahili. Yeye aliangazia lugha ya wahusika pale ambapo amesema kwamba, wahusika wanapewa lugha wanayotumia kwa kutegemea majukumu yao. Kulingana na Bakhtin (1981) lugha ambayo wahusika hupewa huwa mara nyingi inaonyesha matumaini na imani ya mwandishi kwa kuwa lugha yao huwa ya “wengine”. Mwandishi hawezi kupanua mawazo na fikra zake kupitia kwa lugha anayowapa wahusika wake peke yake, hivyo basi lugha ya wahusika pamoja na lugha ya “wengine” hutumiwa ili kuleta uwingi wa ndimi.

Murithi akimrejelea Pearce (1994) akifafanua usemezano, ametoa jazanda ya simu pale ambapo kuna wahusika angaa wawili, anayesema na anayesemewa. Yeye anasema kuwa msemzwa wa mazungumzo ya rununu hana budi kuonyesha kuwepo kwa yule anayepokea simu; msikilizaji wake. Mahitaji ya mawasiliano humlazimisha kutoa sauti. Kwa hivyo inakuwa ni kama kwamba mzungumzaji na mzungumziwa huweza kuzungumza ambapo sauti ya mmoja wao huwa ni ya mzungumzaji na kwa upande mwingine kuna sauti ya msikilizaji. Kama vile simu, neno ni nafsi iliyoko na iliyomilikiwa na msemaji na msemewa kwa pamoja kwani hii ni sifa iliyoko kati ya hadhira na mbunaji.

Utafiti huu umetufaa sana kwa kutupa mwanga kuhusu namna ambavyo nadharia hii ya usemezano inavyotumiwa kuhakiki kazi za fasihi hususan tamthilia na hata ushairi. Hata hivyo uchunguzi huu umetofautiana na utafiti wetu kwa sababu huu ulijikita katika tamthilia za Kiswahili ilhali wetu unatafiti usemezano katika ushairi wa Kiswahili.

Kea (2006) ameangazia athari za muktadha na mazingira katika matini. Amesema kuwa kuna uhusiano kati ya muktadha na usemezano. Muktadha unaelezea taratibu na maana ambayo hubainishwa kwa kutumia urejelezi tofauti katika mazungumzo au maongezi au mazungumzo. Ni kutokana na mtazamo huu ndipo alichunguza muktadha na mazingira ya utungaji na uimbaji wa nyimbo za taarab ambazo zilitungwa na Juma Bhalo na Maulidi Juma Iha. Mazingira ambayo yanakuza muktadha wa utunzi wa watribu hawa Juma Bhalo, Maulidi Juma Iha na Zuhura Swaleh ni ya mji wa Mombasa. Mji huu kihistoria ulichaguliwa kwa minajili ya makaazi na wageni waliouita Mombasa, jina ambalo lilitokana na jina la mji uliokuweco Omani ya leo. Hii ilikuwa ni kwa minajili ya nafasi ya kijiografia iliyokuwa imechukua mji wa Mombasa; ulioweza kuunganisha vyema bara Hindi na Afrika. Mji wa Mombasa ulikuwa umekumbwa na vita (Mvita –mji wa vita).

Anasema katika desturi za waswahili, majukumu ya mwanamke ni kumtunza mume wake na wana wake na shughuli au kazi zao zote hulenga suala hilo. Alieleza kwamba watoto walio kati ya miaka mitatu na sita walikuwa wanapelekwa kwenda kufunzwa duksi (kusoma ili kuelewa na kuikariri Korani tukufu). Wanawake wana wajibu wa kuwafundisha mabinti au watoto wao wa kike maadili mema. Watoto wa kike wa waswahili hushauriwa wawe wenye tabia njema kabisa. Hii ni kwa kuwa uswahilini mwanamke sio tu mtu mrembo, bali pia mrembo wa tabia.

Bhalo aliamua kufumba maana kwa kutumia dhana ya gunia na namna au njia ambazo zinatumiwa katika uchukuzi katika shughuli na mazingira ya bandarini. Amesema kwamba gunia lake ni zito sana katika ubeti wa kwanza. Inabainika kuwa yeye ameathiriwa na mazingira yake, hivi kwamba ametumia gunia kuelezea maudhui ya malezi, yaani msichana aliyeshinda wazazi wake kwa tabia yake oza tena mbovu. Bhalo akamfananisha na gunia ambalo halibebeki. Anasema binti kama huyo aliyejaa kiburi na madharau ni mzito kama gunia lililojaa mizigo na hivyo kuwa jambo gumu kulibeba. Wanaume pia wenye nguvu hawawezi kuliinua gunia kama hilo. Hili linaonyesha kuwa binti kama huyo huleta matatizo tele hivyo hata akiolewa na mwanamume yeyote ni nadra sana kuishi naye.

Uchunguzi huu umetufaidi katika utafiti wetu kwa kuwa kupitia utafiti huu, tumeweza kufahamu kwamba muktadha una athari katika kazi ya fasihi. Hii ni kwa sababu mtunzi hutunga kuhusu mambo yanayomzunguka katika mazingira yake anamokulia. Utafiti huu umetofautiana na wetu kwa kuwa huu utafiti wa Kea umejikita katika usemezano katika taarab huku wetu unaangazia usemezano katika diwani ya *Sikate Tamaa*.

Nyandoro (2014) ameangazia usemezano katika riwaya za Said A. Mohammed alipokuwa akichunguza matumizi ya barua katika riwaya hizo. Riwaya alizozichunguza ni pamoja na *Utengano* (1980), *Kiza katika Nuru* (1988) na *Nyuso za Mwanamke* (2010). Ameangazia jinsi muktadha umeathiri kabisa barua ambazo ziliandikwa katika riwaya hizo tatu. Nyandoro ametaja kuwa nyaraka hizo katika kazi hizi tatu zinaonekana kuwa zinafafana. Waraka ni mwitikio au jawabu la andiko. Barua hizi zimezungukia mambo ya kifamilia, ambapo mhusika mmoja anamwandikia mhusika mwingine waraka kwa kutoa ushauri au kuomba msamaha au wa kutoa ushauri. Mfano ni mzazi kwa mwanawe na kutoa ujumbe mahususi kwa mtu fulani. Mfano ni barua katika *Utengano* (uk.106) Bwana Maksuudi aliandika barua kwa kuomba msamaha mke wake aliyemtaliki kwa maovu aliyomfanyia na kumsihi arejee nyumbani ili waweze kuishi pamoja yaani kama mume na mke.

Amefafanua vile vile kuwa katika *Kiza Katika Nuru* (uk. 258), kuna barua ambayo iliyoandikwa na afisa mkuu wa magereza ili kumfikia hakimumu wa mahakama walikokuwa wameshtakiwa, Bi Kudura na mwana wake Mbishi kwa sababu ya mauaji ya Bw. Juba. Katika *Nyuso za Mwanamke*, Bi Mkubwa alimwandikia waraka Nana bintiye. Barua ambazo aliziandika Bi Mkubwa aliziandika

mapema kabla ya kifo chake na bintiye anakuja kuzipata wakati alipokuwa umri wa utu uzima. Barua hii (uk. 25) ilikuwa ni wasia aliomba bintiye Nana ili kuwezesha kumwandaa na kumsaidia kabisa atakapofika umri wa utu uzima. Kutokana na utafiti huu, ilibainika kwamba kazi za fasihi huingiliana na kuwa zinahusiana. Isitoshe imeonyesha kuwa wazo ni jibu kwa wazo lingine. Maelezo haya ya Nyandoro yametuongoza katika utafiti wetu kwa kuwa umetuonyesha kuwa maandishi katika waraka ni jibu la andiko kama ilivyo usemi jibu la usemi mwingine. Licha ya hayo utafiti huu ni tofauti na wetu kwa kuwa umechunguza matumizi ya barua katika riwaya za Said A. Mohamed na utafiti huu umelenga usemezano katika mashairi ya *Sikate Tamaa*.

Tarde (1989) akitoa hoja kuhusu usemezano anadai kuwa watu mara nyingi wanazungumza juu ya wahubiri wao, waandishi wao, wazazi wao na walimu wao. Kwake yeye uzungumzi wa mtu mmoja aliye na mamlaka ya juu huleta usemezano kati ya walio sawa. Hii ni kwa kuwa wajibu wa wenye mamlaka na ambao hawana huwa tofauti. Hivyo basi kwa maoni yake uzungumzi wa mtu mmoja una hadhi ya juu.

1.6.2 Yaliyoandikwa kuhusiana na Mashairi katika Sikate Tamaa

Katika sehemu hii, tumeshughulikia yaliyoandikwa kuhusu mashairi katika diwani hii. Hii inajumlisha tafiti za mwanzo zilizofanywa kuhusu mashairi yaliyo kwenye diwani hii, matokeo ya uchunguzi, namna ambavyo utafiti ulitufaidi na jinsi ambavyo utafiti unatofautiana na huu uchunguzi wetu.

Abdalla aliyemwandikia S.A. Mohamed utangulizi, amesema kwamba mwandishi huyu amejasiri. Amedokeza kuwa kuna mambo mawili ambayo yamo katika tungo hizi. Mambo haya ndiyo yaliyompa nguvu sana ya kuitikia na kukubali kuziandikia utangulizi wakati S.A. Mohamed alipomsihi. Amesema kwamba mambo haya mawili yametokana na ukakamavu wake na hivyo alimpa pongezi za dhati ya moyo wake na angetaka watunzi wengine wafuate mkondo huo. Amesema kuhusu tungo hizi pia kwamba mtunzi amekomaa kwa sababu alisemea jamii pana na wala sio jamii finyu.

Abdalla anamsifu Said A. Mohamed kwa kuwa yeye hakuishia katika kuyafahamu yale ambayo yako mbele ya pazia tu bali alifungua pazia hilo na kufunulia jamii yale yaliyofanyika ndani ya pazia hilo na kuyaulizia maswali. Mfano ni katika tungo hizi: “Siku Njema” (uk. 5), “Naandika”

(uk. 17), “Nimeamka” (uk. 4), “Nimeona” (uk.8), “Wananambia Mchafu” (uk. 7) na “Ajabu” (uk. 9).

Ukakamavu wake wa pili kulingana na A. Abdalla ni katika miundo ya mashairi aliyoitumia kwenye baadhi kubwa ya tungo alizoandika katika diwani hii. Muundo uliozoewa wa arudhi au ya kwamba mashairi ya Kiswahili hufuata vina, mizani na mishororo, yaani muundo wa shairi la tarbia, halikuzingatiwa zaidi na mtunzi huyu kwani alivyaza mbinu mbalimbali. Hii ni ishara mojawapo ya umahiri wake. Isitoshe ni jambo dhahiri kwamba katika jumla ya mashairi arubaini na nne yaliyo katika diwani hii, ni mashairi sita tu ndiyo yenye muundo huo. Mifano, “Neno Limekuwa Kitu” (uk. 41), “Watoto wa Afrika” (uk. 2), “Kifo Kitamu” (uk. 42), “Sema” (uk. 14) “Chui wa Kufuga” (uk. 29) na “Kama Asali Yaua” (uk. 44).

Abdalla alisema kuwa mashairi yaliyomo kwenye kitabu hiki, yamegawika katika vikundi viwili vikuu. Kundi la kwanza limekusanya mashairi yanayohusu siasa moja kwa moja huku kundi la pili, maudhui yanahusu wasifu, nasaha, mapenzi, maisha kwa ujumla, kejeli, vijembe, huzuni na furaha. Mawazo ya Abdalla katika mashairi haya yametufaidi sana kwa kuwa yametusaidia kufahamu zaidi kuhusu tungo zilizo kwenye diwani hii na hivyo kurahisisha uelewa katika utafiti wetu. Mchango wa Abdalla unatofautiana na wetu kwa kuwa yeye aliangazia mashairi yote katika diwani kwa sababu alikuwa anahariri huku utafiti wetu umelenga usemezano katika mashairi haya.

Mwingine ambaye amezungumzia kuhusu *Sikate Tamaa* ni Indede (2011) alipokuwa akitoa maoni yake kuwa “Mwanamke angali tata katika ushairi wa kisasa.” Alisema kuwa mtunzi Said A. Mohamed anamwona mwanamke kama ua katika diwani ya *Sikate Tamaa*. Alisema hivyo akirejelea shairi “Ua” (uk. 34) ubeti wa saba na nane.

Katika ubeti wa saba unaeleza kwamba ua ni mama mzazi ambaye ana uwezo wa kuongeza idadi ya watu duniani. Kwake mama ni mwandani, mtimiza haja yake na mtosheleshaji. Anampenda mama kwa namna afanyapo kazi na sio tu namna anavyopendeza. Anasema mama hana uzembe na hivyo ndivyo anavyolitazama ua.

Katika ubeti wa nane anasema kuwa ua ni mamake mpenzi kati ya vitu vyote vilivyo na uhai. Anamthamini na kuonea fahari heshima na maneno yake ya himizo. Pia anawaenzi rafiki zake na

yeyote anayejishirikisha naye. Mama anapodhulumiwa yeye anahuzunika sana kwa kuwa anamthamini na kumpenda.

Mwandishi anafafanua mitazamo mbalimbali ya walimwengu kuhusiana na namna wanavyolifasiri na kulitazama ua. Anatoa ufafanuzi wa namna anavyomtazama mama mzazi kuwa huyu ni mtu ambaye ana thamani hasa kutokana na maumbile. Ndipo (ub. 7 & ub. 8) anaelezea ufasiri wake wa dhana hii nyeti ya ua, kwa kuipa fasiri mbili, ya kwamba ua ni mama mzazi na pili kuwa ua ni mmea.

Vile vile Indede (2008) ameanika kuhusu diwani hii alipokuwa akichambua mada ya “Mabadiliko katika umbo la ushairi na athari zake”. Yeye anasema kuhusu namna ambavyo msanii huyu mwenyewe alivyojihisi kuwa amebadilika kifani kutokana na kupevuka kwa hisia za mitindo na miundo mbalimbali. Amevyaza mbinu mbalimbali katika ushairi wake. Kwake ushairi sio tu jambo la vina na mizani pekee na wala sio uhuru tu bali ni uhuru wa busara ambao unashikamana na hisia na zaidi ya hayo ni ufundi wa utunzi. Kwa uthabiti na ujasiri, mtunzi huyu anahusika kwenye mgogoro wa mabadiliko ya ushairi kwa kutilia mkazo kwa kusema kwenye shairi lake “Nawaita Washairi” (uk. 3) kwamba watu waandike mashairi kwa ari kuu.

Anasema katika ubeti wa kwanza na wa pili kwamba anawaita watunzi wawe na umoja katika na safari ya utungaji wa mashairi iliyojaa mapambano. Anawarai wasanii wenzake kuwa waache mashindano kabisa na watunge mashairi kwa hima. Anaendelea kuwachochea wawe na mitindo mbalimbali inayoingiliana waondoe utata na kuonyesha mwingiliano. Wawe na upendo mwingi kama watu walio kwenye msongamano na waandike mashairi kwa msukumo mkubwa kabisa.

Mawazo haya ya Indede yametufaidi sana kwa kuwa yametuwezesha kuyaelewa zaidi mashairi yaliyo kwenye diwani hii na hivyo kurahisisha uchunguzi wetu. Kauli hii imetofautiana na utafiti wetu kwa kuwa mawazo haya yameshughulikia namna ambavyo mwanamke angali tata katika ushairi wa kisasa ilhali uchunguzi wetu umeegemea suala la usemezano katika diwani hii.

Wamitila (2002) amechambua dhamira na maudhui pamoja na suala la lugha katika *Sikate Tamaa* akilenga shairi la “Kifo Kitamu” (uk. 42). Yeye amesema dhamira katika shairi hili ni ‘umuhimu wa kutetea haki yako kwa kila hali.’ Ujumbe huu ndio umekaririwa na kipokeo au mkarara wa shairi hili.

“Kama kuishi kuchungu, kifo huwa ni kitamu”.

Katika shairi hili tunaambiwa ya kwamba ni heri mtu afe akipigania haki yake kuliko aishi maisha mema huku akinyonywa na kuteswa. Maelezo haya yaliyo katika ubeti unaofuata yanadhihirisha dhamira hii.

Iwapo dhila nidhamu, bora ivunjwe kwa dhati
Kinyume chake wazimu, kufuata usaliti
Mwenye akili timamu, hajiweki katikati
Kama kuishi kuchungu, kifo huwa ni kitamu. (uk. 42)

Akiangazia lugha, Wamitila ameonyesha tamathali za usemi katika shairi hili. Ametaja “kwelikinzani” kwa kulenga maneno haya: “kifo kitamu” tukijua bila shaka kifo hakiwezi kuwa kitamu bali ni jambo la kuhuzunisha mno lakini mtunzi ametumia maneno haya ya kwelikinzani ili kusababisha dhamira yake ieleweke zaidi.

Kauli hii ya Wamitila imetusaidia kwa kutuwezesha kufahamu maudhui yanayojitokeza katika mashairi yaliyo kwenye diwani hii na vile vile matumizi ya lugha. Hili limetupa mwangaza kuhusu mashairi tunayoyashughulikia. Hata hivyo mawazo haya yanatofautiana na yetu kwa sababu tumeangazia usemezano kwenye kazi hii.

Ngolo (2011) katika kushughulikia mabadiliko ya kimtindo katika mashairi ya Said A Mohamed, ameangazia mashairi ya tathlitha. Ametaja kwamba mashairi ya tathlitha katika diwani tatu za Said A Mohamed, yana miundo minne kulingana na miundo ya vina, mizani, vipande na vituo. Tungo za tathlitha huwa zimeundwa kwa vipande viwili viwili vyenye mtiririko wa vina na uwiano wa mizani. Hata hivyo, kama alivyosema Abedi, (1954:29) idadi ya vipande na mizani inaweza ikawa tofauti lakini ni lazima iwe sawa na isiende kinyume na desturi yake. Hivyo, miundo yake tofauti inaendana na sheria hii. Ngolo anasema kuwa aina ya kwanza ya tathlitha ni muundo ambao una sehemu mbili na mishororo mitatu. Mfano wa shairi lenye muundo huu ni “Maisha Mapya” (S.A.M. 1980:25.) Ni shairi la bahari ya ukara kwa kuwa vina vyake vya nje vinalingana katika shairi zima au lote. Amesema aina ya pili ina vipande viwili lakini kuna tofauti katika kina cha mwisho cha kiitikio. Mfano wa muundo kama huu unapatikana katika Jicho Geni (S.A.M. 2002:45). Aina ya tatu ni muundo wenye sehemu tatu. Mfano unaonekana katika shairi “Ndoto” (S.A.M. 1980:26) na

kwamba aina ya nne ni muundo wa sehemu nne na wenye ubeti mmoja pekee kama ilivyo katika shairi la uteto (S.A.M. 2002:16).

Ngolo vile vile anadai kwamba kuna mabadiliko kwenye maudhui. Tungo za tathlitha kwa kawaida zilizungumzia ujumbe sahili haswa kwa lengo la kutumbuiza. Tungo za tathlitha za Said A. Mohamed zinashabihiana na zile za kijadi ijapokuwa zingine zinatofautiana. Mfano mwafaka ni shairi la “Ndoto” (1980:26) ambalo lina jumbe nzito. Tofauti hizi za kimaudhui hutokea kwa sababu mshairi huyu kama walivyo washairi wengine wa leo wanajitokeza kutunga mashairi kwa kutumia mtindo wa kuvutia wakati wa kuandika.

Utafiti huu wa Ngolo umetufaa pakubwa kwa kuwa kupitia uchunguzi huu, tumeweza kupata mwangaza kuhusu mashairi yaliyoandikwa katika diwani hii na hivyo kutuelekeza katika uchambuzi wetu. Licha ya haya utafiti huu ni tofauti na wetu kwa kuwa tumetafiti juu ya usemezano katika diwani ya *Sikate Tamaa* na uchunguzi wake Ngolo umejiegemeza katika mabadiliko ya kimtindo katika ushairi wa Mohamed.

Munyao (2016) ameangazia uhuru wa kishairi katika *Sikate Tamaa* alipokuwa akichanganua uhuru wa kishairi katika *Miale ya uzalendo* na *Sikate Tamaa*. Anasema kwamba uhuru wa kishairi umejitokeza kwa kiasi kikubwa sana katika diwani ya *Sikate Tamaa*. Alishughulikia inkisari, tabdila na mazida. Mfano ni kama vile inkisari inavyojitokeza katika diwani hii. Katika shairi la kwanza “Sikate Tamaa” (uk. 1) ametoa mifano ifuatayo. Sikate badala ya usikate katika kibwagizo cha shairi katika shairi lote. Shairi la “Ajabu” (uk. 9) na asonayo (ub.1) badala ya asiye nayo, shairi la “Mbele ya Safari” (uk. 10) twataka badala ya tunataka (ub. 5) na ‘mekuwa badala ya imekuwa. Kupitia kwa uchunguzi huu ilibainika kwamba mtunzi ametumia uhuru wa mshairi ili kutimiza mahitaji ya muundo wa shairi kama vile urari wa vina na mizani.

Utafiti huu wa Munyao umetusaidia katika uchunguzi wetu kwa kuwa umetuwezesha kufahamu zaidi mashairi yaliyomo katika diwani hii. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu umejikita katika kuchanganua uhuru wa kishairi huku wetu umelenga katika kutafiti usemezano katika diwani ya *Sikate Tamaa*.

1.7 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu unaongozwa na Nadharia ya Usemezano. Kulingana na Mbatiah (2001), nadharia ni mfumo wa kimawazo wenye kanuni mahususi. Nadharia inatoa mwelekeo wa jinsi ya kushughulikia na kuhakiki fasihi. Nadharia hii ndiyo kigezo cha kupimia ujumbe au maana inavyojitokeza katika diwani ya *Sikate Tamaa*.

Wamitila (2002) anasema kwamba nadharia ya usemezano iliasisiwa na mhakiki wa kirusi aliyeitwa Mikhail Mikhailovich Bakhtin aliyeishi kati ya 1895-1975. Anasema kwamba mhakiki huyu alipata kuandika kazi zake katika miaka ya mapinduzi ya urusi ya 1917. Mazingira ambamo aliandikia yalikuwa magumu sana. Hii ni kwa kuwa alikumbwa na matatizo kama vile: kushindwa vitani, baa la njaa, uvunjifu na usumbufu, lakini hali hii haikuweza kuathiri kazi zake. Mawazo yake Bakhtin yaliishia kuenea katikati ya mwishoni mwa karne ya ishirini ikisambazwa na mhakiki Julia Kristeva.

Nadharia hii ilijitokeza baada ya kipindi cha wanaumuundo. Nadharia hii ilijitokeza na majibu ambayo nadharia ya umuundo ilishindwa kuyajibu. Suala mojawapo ni kama vile ufungamano wa ishara au alama na hali halisi ya kauli nzima.

Kwa mujibu wa Bakhtin alama “iliyotimilika” huashiria maana kamilifu na ina sifa za urasmi. Sifa za urasmi (kama wakati, hali, jinsi na idadi) huwakilisha ishara ambazo kila mnenaji anazijua na hazitangamani na maoni ya mtu binafsi, hubakia vile zilivyo wakati wote. Sifa za umaana hujibidiisha katika kuondoa hisi zozote za mnenaji ili ziwe kama sifa za urasmi japo haziwezi. Hii ni kwa sababu maneno yenye sifa za umaana hutegemea mfumo maalum wa urejelezi wenye muktadha maalumu ndiyo maana halisi hupatikana (Holquist 1990:16). Katika muktadha huu huu wa neno kuwa na sifa mbili ndipo Bakhtin anapodokeza kwamba kauli (sentensi) sio kipashio cha juu zaidi katika lugha. Kwa Bakhtin sentensi vile ilivyo kamwe haileti maana bila ya kuwekwa katika jumua nzima ya mawasiliano. Jumua nzima ya mawasiliano yanayoelekeza tamko ina sifa tatu. Kwanza, mahala pamoja walipo washiriki au wazungumzaji, pili ni ujuzi na uelewaji wa pamoja wa hali waliomo washiriki na tatu ni ule utathmini wao wa pamoja wa hali hiyo.

Sifa hizi tatu ndizo ambazo husaidia wasomaji na wasikilizaji kuelewana katika kila tamko linalotamkwa; kuwako mahali pamoja, kuielewa hali ilivyo na kuitathmini hali hiyo wakiwa pamoja kutasaidia kuielewa maana ya tamko lolote lile hata liwe la namna gani. Mifano ni kama maneno ya viingizi kama “ah!” na “ala!” au maneno ya amri kama “amkeni!”, “ondoka!” ni maneno madogo na wakati yanapotamkwa hutolewa kwa upesi sana, lakini yana sifa ya ukamilifu na ambayo kwamba hutarajiwa mnenewa ajibu matamshi haya kwa kusema au kwa vitendo. Haya yote yatatukia ikiwa tamko litachukuliwa kuwa ni mshikamano katika jumua nzima ya mawasiliano (Bakhtin 1986). Kipengele hiki cha tamko kinatiwa nguvu na suala la matamshi kuingizwa na viimbo. Viimbo ni sauti zinazoandamana na tamko lolote na hudhihirika katika masikizi. Ni kutokana na viimbo hivi ndivyo huashiria kama tamko hilo ni swali, kauli, rai, mshangao au amri. Viimbo ndivyo vyenye kuleta athari zinazokusudiwa katika usemezano kwa sababu maana inapatikana iwapo msemewa ameelewa aliloambiwa ikiwa ni kuulizwa au kuamrisha. Ndiyo maana Bakhtin akasema kwamba sentensi ni kipashio cha lugha chenye kutofautiana na tamko ambalo ni kipashio cha mawasiliano katika uzungumzaji. Maelezo haya ya matamshi na viimbo yamesaidia uchunguzi huu katika kuelewa maana halisi aliyodhamiria mtunzi wa *Sikate Tamaa*. Katika suala la matamshi kuwa na mshikamano, utafiti huu umenufaika kwa kuelewa muwala uliopo katika mashairi haya kwa jumla.

Amali anazozifanya binadamu huathiri pakubwa hata matamshi yake; nayo huonekana katika lugha anayoitumia. Matamshi haya hayaonyeshi malengo yake kutokana na maudhui au mitindo ya kiisimu (kama utumizi wa msamiati) tu bali pia katika mtindo wa kuyatumia matamshi hayo. Ni kweli kuwa kila tamko liko pekee, lakini kila lugha huzoeleka kutumiwa katika nyanja fulani hadi matamshi haya yakajimakinisha katika nyanja mahususi. Kulingana na Bakhtin (1986:60) lugha hizi zinaweza kuitwa sajili. Jambo au suala hili la sajili laonekana kuwa matamshi yana mipango au chembe ya ratiba (mpango) lakini Bakhtin hataji mipango hii kutokana na nadharia yake kwa kuwa maana imefungika katika muktadha na muktadha haukufungika. Hali hii ya kutofungika kwa matamshi inatokana na madai ya usemezano kwamba katika wakati fulani, pahali fulani, kuna nguvu fulani zisizothabiti ambazo zitalipa neno lilitamkwa hapo hapo maana ambayo wakati mwingine na pahali pengine litakuwa na maana iliyo tofauti kabisa.

Kwa mfano katika *Sikate Tamaa*, Said A. Mohamed ametumia neno “dunia” kwa maana tofauti katika mahala kuwili tofauti katika shairi la “Sikate Tamaa” (uk. 1).

(Ub. 2, Mshororo 3)

“Dunia” baa, nyanyuka, anza tena kujipinda.

(Ub. 3, Mshororo 1)

Sivunjwe moyo, “dunia”, hivyo itakunyanyasa.

Katika ubeti wa 2 mshororo wa 3, “dunia” ina maana “ulimwengu” lakini katika ubeti wa 3 mshororo wa kwanza “dunia” imetumiwa kwa maana ya “maisha” yaani maisha hunyanyasa.

Bakhtin (1981:267) anaonelea kuwa riwaya peke yake ndiyo sajili bora kwa sababu lugha yake nzima imo katika usemezano. Yeye anasema kuwa lugha ya ushairi kuanzia mwanzo hadi mwisho wake ni kama mtu mmoja tu anayezungumza wala hakuna ushirika wowote. Katika lugha ya ushairi ni mshairi tu ndiye asemaye wala hakuna mtu yeyote mwenye kumjibu mshairi kwa sababu lugha ya ushairi haikubali mwingilio wowote wa wasemazwa: Katika upande wa lugha ya riwaya, Bakhtin anasema kuwa ndiyo pekee inayochanganya sajili zote kwa pamoja na pia ndiyo pekee yenye kukubali maingiliano na hadhira yake. Pia ndiyo yenye kujuza kwamba kuna wahusika wawili wanaoshirikiana katika kusemezana na basi ndipo riwaya inaendelea. Maelezo haya yamechangia katika kufanikisha utafiti huu kwa kuchochea uchunguzi zaidi na kuthibitisha kwamba ushairi kama ilivyo riwaya uko katika usemezano. Hii ni kwa kuwa katika shairi la ngonjera, kuna wahusika wanaosawiriwa kuwa katika hali ya majibizano au hali ya mjadala. Mfano ni kama vile shairi la “Mwanakupata” (uk. 36) ambapo Mwanakupata na Mwiha ni washiriki katika shairi hili wanaojibizana. Lugha ya usemezano pia inakutanisha maoni ya washiriki wanaojibizana.

Mbali na msememeza (ambayo ndiyo nafsi ya mtunzi) kuna nafsi nyingine, “yeye” ambayo husemezana na msememeza. Kwa hivyo, kila mnenaji anavyoendelea kunena, huwa tayari anachukua jukumu kubwa la kumjibu mnenewa. Majibu haya si sharti yasikike lakini katika kuisimka kwa mnenewa kunamjuvya mnenaji achukue njia gani na aendele vipi katika usemezano wake. Hivyo basi, lugha ya usemezano ni yenye kuingiliana na isiyokuwa na mwelekeo mmoja bali mielekeo miwili. Mfano ni kwenye shairi la “Kifo Kitamu” (uk. 42) ambapo msememeza ambaye ni mwandishi anasemazana na msememewa ambaye ni msomaji kuhusu kupigania haki, yeye anasema heri mtu afe akipigania haki kuliko kuishi huku akidhulumiwa. “Kupambana ndio sifa, na kuishi siko radhi” (ub. 5 mshororo wa 3). Mwandishi anasema kama kuishi kunakuwa kuchungu basi kifo kinaweza kuwa

ni kitamu. Katika maneno haya msemazwa (msomaji) ambaye ni nafsi ‘yeye’ atasisimka licha ya kuwa hajampata msemaza moja kwa moja.

Katika hali hii ya kuona kuwa lugha ni usemezano, basi ile nadharia ya mawasiliano kwamba kuna msemaji na upande wa pili kuna msikilizaji ambaye hafanyi kitu kingine ila kusikiliza tu inakataliwa na nadharia ya usemezano, (Morson (1986:3). Nafsi ya “mimi” haiwezi ikaweza kujitambua, hadi itambue kwamba kuna nafsi ya “yeye”. Yaani nafsi moja haiwezi kujijua hadi pale ambapo itapata nafsi nyingine. Kwa hivyo “mimi” itajitambua kwa “yeye”. Maana ya suala lolote haijulikani hadi ipate jibu kutoka kwa suala lingine. Kwa mfano maana ya “mwanga” haijulikani hadi litokee “giza”, kwa hivyo jibu la mwanga ni giza. Katika kujibu ndiyo maana ya kitu inajulikana. Kuwako kwa kitu kutategemea kama kitu hicho kina maana (Holquist 1990:49). Walakini, “mimi” nitamtambua “yeye” kwa “yeye” kunijibu “mimi” na hapo ndipo kuwako kutaleta maana inayokusudiwa.

Uzungumzi nafsi ni usemezano vile vile. Katika muktadha huu wa kujibizana kati ya “mimi” na “yeye” na utambuzi wa kuwa kuna nafsi zinazoshirikiana katika usemezano huu ndiyo, Mukarovsky (1977:96) anasema ya kwamba katika uzungumzi nafsia, nafsi moja hujisemea yenyewe ikawa ni kwa mawazo tu au inajiambia kwa sauti mpaka watu wanasikia. Katika uzungumzi nafsia, nafsi moja inachukua nafasi ya nafsi mbili ili kutosheleza usemezano.

Bakhtin anasema kwamba majibizano baina ya mzungumzaji na mzungumziwa yanatokana na kule kuathiriana kwao (Morson 1986:92). Hakuna mtu yeyote anayetoa tamko halafu akajigamba nalo kwamba yeye ndiye wa kwanza kulisema isipokuwa Adam peke yake ndiye aliyekuja na kuanza kutumia maneno, kwani yeye ndiye wa kwanza kufundishwa maneno. (Bakhtin 1981:279). Kulingana na ufafanuzi huu basi, ni dhahiri kwamba hakuna atamkaye neno au usemi ila ameathiriwa kwa njia ama namna moja au nyingine. Ama atalipinga, atalitolea rai, ataliongeza au atalipunguza.

Kulingana na Bakhtin (Holquist 1990:88) riwaya peke yake ndiyo sajili inayotegemea sana uathiriano wa matini nyingine. Ijapokuwa matini nyingine huathiriwa na nyingine lakini si kama kwa kiwango cha riwaya. Riwaya hudondoa sana kazi nyingine kwa njia moja au nyingine. Na

athari moja ni kuwa riwaya huathiri kazi nyingine ambazo hujisifu kwa kuwa safi na pweke na hazina chembe ya athari.

Matini nyingi huathiriana na kutokana na kuwa nafsi mbili zikishajitambulisha kwamba zinapatikana, basi nafsi moja haitoanza kutamka hadi ijue nyingine inasema nini. Kwa hivyo, “mimi” tayari ashawaza jibu la “yeye” kabla ya “yeye” kulitamka. Na “mimi” naye hatamki ila amemsikia “yeye” akisema. Kulingana na maelezo haya, uathiriano ni kwenda nyuma (kumsikia mtu akisema) na kwenda mbele (kuathiri majibu ya atakaye kuja hatimaye). Na kutokana na maelezo haya, nadharia hii ya usemezano inatumiwa kama kipimo cha kuhakiki mashairi katika diwani ya *Sikate Tamaa*.

1.7.1 Mihimili ya Nadharia ya Usemezano

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), majibizano ndiyo ambayo yanahuisha usemezano baina ya wahusika. Katika kutumia kigezo hiki, mashairi ya Said A. Mohamed yamechunguzwa namna yalivyoendelezwa kutokana na majibizano baina ya wahusika kama vile katika shairi la “Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo” (uk. 20) kuna wahusika wawili wanaojibizana. Katika hali hii ya kujibizana ni dhahiri kwamba kuna ushikamano wa tamko moja na lingine. Pia majibizano haya yameshikana ili yapitishwe vyema kwa hadhira.

Kuna maongezi, mfano mazungumzo ya kawaida au ya kila siku. Hii ni dhana ambayo inarejelea mazungumzo kati ya wanadamu. Hili hutokea pale ambapo mtunzi amewasawiri wahusika wakiwa katika hali ya mazungumzo.

Kuna athari ambazo zinapatikana kutokana na matamshi ya mzungumzaji na mzungumziwa, kwani nafsi hizi mbili huathiriana. Holquist (1990:88) anasema, nafsi moja haitoanza kusema mpaka ijue nyingine inaweza kusema nini. Kwa hivyo, nafsi “mimi” tayari ashafikiria jibu la nafsi “yeye” kabla “yeye” kulitamka. “Mimi” naye hatamki ila amemsikia “yeye” akisema. Kulingana na maelezo haya hali ya kuathiriana ni kule kwenda nyuma (kumsikia mtu akisema) na kwenda mbele (kuathiri majibu ya atakaye kuja baadaye).

Kuna dhana ya diskosi au usemi, ambapo kuna usimulizi wa kisanaa wa moja kwa moja ambao unafanywa na mtunzi. Hii imechukua nafasi kubwa na yenye umuhimu mkubwa katika uhakiki wa

ki-Bakhtin kwa kuwa inaaminika kuwa mtunzi anaposema kimaandishi, anaamini kuwa yule anayesimuliwa (msomaji) atapata ujumbe ijapokuwa hamwoni msimulizi kwa hali ya moja kwa moja. Msemezwa anaposisimka baada kuyasoma yaliyoandikwa itakuwa ni dhahirisho kuwa amepokea ujumbe.

Usemezano huiangalia lugha kama njia ya mawasiliano na vile vile huiona lugha kama chombo. Bakhtin aliiangalia fasihi kama utendaji au utekelezaji wa lugha kwenye hali halisi (Wamitia 2002). Tangu kuumbwa kwa binadamu, lugha ndiyo kipawa anachokitumia ili kuelezea hisia zake, tajriba zake maishani na mawazo aliyonayo bongoni mwake. (Bakhtin 1986:67). Kwa ubunifu na usanifu mkubwa alionao, mwanadamu ameweza kuitumia lugha kueleza matukio muhimu katika maisha yake kimtungo. Mfano ni S.A Mohamed alivyotumia lugha katika shairi lake la “*Sikate Tamaa*” (uk.1).

Yeye ametumia lugha “shaurifu”, “arifu” na “zindushi.”

Ub. 4 Una nguvu, simama, wewe upambane nao,
 Una werevu, simama, uzepuke njama zao,

 Usiche kovu, simama, ujifunze vumilio,
 Sikate tamaa.

Nadharia hii ya Usemezano imeteuliwa kutokana na kwamba sifa zake zaonekana katika diwani hii. Nadharia hii pia inaafiki katika utafiti huu kwa vile vigezo vyake ni mufti kupimia ushairi hususan *Sikate Tamaa*.

1.8 Mbinu za Utafiti

Katika sehemu hii tumeonyesha jinsi tulivyoteua data yetu, namna tulivyochanganua data na jinsi tulivyowasilisha data. Kwanza, tumesoma kazi za ushairi zilizoandikwa na Said Ahmed Mohamed zikiwemo *Sikate Tamaa* (1980), *Kina cha Maisha* (1984) na *Jicho la Ndani* (2002). Baada ya kusoma kazi hizi tumeteua diwani ya *Sikate Tamaa* kama diwani lengwa katika utafiti wetu. Hii ni kwa kuwa mashairi katika diwani hii yametupa data tunayohitaji.

Pili, tulisoma mashairi yaliyo katika diwani ya *Sikate Tamaa* kwa sababu diwani hii ni chanzo cha utafiti wetu. Tuliteua mashairi kumi na manane kati ya mashairi arubaini na manne yaliyoandikwa

kwenye diwani hii. Hii ni kwa sababu haya ndiyo yanayotupa data tunayohitaji katika uchunguzi wetu. Uteuzi wetu wa mashairi haya ni wa sampuli ya kimakusudi.

Tatu, tulisoma mashairi haya ili kutambulisha vipengele vya usemezano vya kimsingi katika utafiti wetu. Pia tumesoma yaliyoandikwa kuhusiana na mwelekeo huu wa uhakiki wa usemezano katika vitabu, majarida na makala mbalimbali pamoja na mtandao. Maelezo haya yalituhami na yalituwezesha kuelewa nadharia hii kwa kuzingatia jinsi misingi ya madai yake inavyotumika katika uhakiki wa ushairi na kwa njia hiyo kufanikisha ufahamu wetu na utafiti wetu.

Nne, tumechanganua data yetu na kuiwasilisha kwa kutumia ufafanuzi, kueleza, kujadili na kutathmini. Tano, tulitafuta ushauri kutoka kwa wasimamizi wetu, wahakiki wa fasihi hususan ushairi, wahadhiri mbalimbali wakiwemo wanafasihi, wanaisimu na pia wasomi wa isimu.

1.9 Hitimisho

Katika sura hii tumeeleza kwa ufupi dhana ya usemezano. Kisha tumeshughulikia tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti na maswali ya utafiti ambayo ni matatu. Pia tumeeleza sababu za kuchagua mada ambayo ni kuonyesha kuwa usemezano upo katika ushairi wa Kiswahili kinyume na madai ya mwasisi wa nadharia ya usemezano na kwamba vipengele vya usemezano vinachangia kujenga dhamira na maudhui katika diwani ya *Sikate Tamaa*. Tumetaja upeo na mipaka ambayo ni usemezano katika diwani ya *Sikate Tamaa*, tukilenga mashairi kumi na manane huku tukilenga vipengele saba vya usemezano. Vipengele hivi ni: majibizano kati ya wahusika, lugha ya wahusika, uhusiano na matini zingine, usimulizi wa kisanaa, usemi kuwa jibu la usemi, dhana ya shani kwa mujibu wa Bakhtin na kumiliki sajili nyingi za lugha.

Jambo lingine tulilolishughulikia ni yaliyoandikwa kuhusu mada ambapo tumeona yaliyoandikwa kuhusiana na nadharia na yale yaliyoandikwa kuhusiana na diwani ya *Sikate Tamaa*. Aidha tumeshughulikia msingi wa nadharia ya uhakiki ya usemezano ambayo tumeeleza mihimili yake. Hatimaye tumeeleza njia zetu za utafiti. Sura inayofuata imeshughulikia vipengele vya usemezano katika ushairi wa Kiswahili.

SURA YA PILI

VIPENGELE VYA USEMEZANO KATIKA USHAIRI WA KISWAHILI

2.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeeleza vipengele vya usemezano kwa ujumla na kufafanua namna vipengele hivi vinavyofanikisha ukuzaji wa maudhui yaliyokusudiwa na mwandishi. Tumefanya haya kwa kutoa mifano kutoka kwa mashairi mbalimbali ya Kiswahili. Tumelenga vipengele vifuatavyo: Uzungumzi nafsia, kuonyesha kuwa tamko ni jibu kwa tamko lingine, utendaji, majibizano au mjadala, usimulizi wa kisanaa, uwingi sauti, kuwepo kwa sajili mbalimbali, kani pewa na kani kitovu pamoja na kanivali.

2.1 Uzungumzi Nafsia

Mukarovsky (1977) anasema uzungumzi nafsia ni namna moja ya usemezano. Hii ni kwa sababu mtu anasema na nafsi yake. Biersteker (1996) amejadili namna ambavyo watunzi wa karne ya ishirini wameathiriwa na Muyaka. Katika shairi ‘Moyo’, msemaji ni moyo wake na msemewa ni nafsi yake. Moyo unamwambia msemewa (nafsi) kwanza afanye jambo lakini asifanye ishara. Shairi hili linachora tofauti kati ya kile moyo unasema na kile nafsi inatamani. (Abdulaziz 1979:72)

Katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* (1973) mshairi pia anadhihirisha uzungumzi nafsia, pale ambapo kuna usemezano baina ya moyo na nafsi yake. Mtunzi Abdalla katika shairi “Moyo iwa na Subira” (uk. 48) alikuwa ametiwa gerezani baada ya kuchochea watu dhidi ya uongozi wa wakati huo nchini Kenya. Yeye alikuwa amekereka sana na kuhisi uchungu kwa sababu wakati wake wa kutoka gerezani ulikuwa umetimia lakini akaongezewa siku zingine za kuzidi kubakia pale ndani. Hili lilisababisha mtunzi huyu kutunga shairi hili ili kuutia moyo wake nguvu na uvumilivu ili asubiri hadi tarehe 20 Oktoba, 1971.

Katika ubeti wa kwanza, mshairi ambaye ni mzungumzaji anazungumza na moyo wake “usilie”. Anauambia moyo kuwa unyamaze kwani ulimwengu huwa hivyo (moyo), itabidi kuwa tu na subira. Anautia moyo wake tumaini. Anauambia kuwa usilie wala kusikitika bali utulie

tu kwa kuwa ukisikitika kwamba moyo wake utajiumiza bure. Ulimwengu kwa kawaida huwa na mambo yanayokera hivyo anauambia moyo wake utulie na kuzidi kusubiri. Kutokana na maelezo haya, tunaona maudhui ya unyanyasaji kwani ulimwengu hutendea watu uhuni na dhuluma kama vile Abdalla alivyotendewa.

Katika ubeti wa tano mshairi (mzungumzaji) anauliza moyo wake maswali ya balagha. Angetaka kujua sababu ya moyo wake kulia na kuomboleza, angetaka kuyafahamu kulia huko kwote ni kwa nia gani, anauambia moyo wake unyamaze kwani anauonea moyo wake huruma kwa kuwa unapolia, tendo hilo linamfanya pia yeye kulia hivyo basi kwa kuisitiza unamhimiza moyo kuvumilia na kujaa subira.

Katika ubeti huu tunadhihirishiwa kwamba nafsi ya mshairi inawakilishwa na 'ni' ambacho ni kiambishi cha nafsi (waniliza) 'na' (nakuoneya). Nafsi inasihi moyo uwache kulia bali utulie tu.

Katika ubeti wa kumi na moja nafsi inamwambia moyo wake kuwa ni zamu ya kujaribiwa kwamba moyo wake yuko kama mwanafunzi anayefanya mtihani kwa sababu umepewa mtihani na itabidi ujikakamue; inamweleza kuwa itabidi moyo uwe mwangalifu sana ili upite mtihani huo. Inamwahidi tuzo iwapo utafaulu kwa hilo jaribio, kwa kuwa inampenda bila shaka. Nafsi inamrai moyo uzidi kuvumilia.

Usemizano mwingine wa nafsi na moyo unadhihirika katika *Al-inkishafi* iliyoandikwa na Sayyid Abdallah bin Ali bin Nassir katika miaka ya 1810-1820. Akizungumzia kuanguka kwa Pate, Sayyid Abdalla ameangazia nafsi inayosemezana na moyo kuhusu hali ya madanganyo ya dunia. Nafsi inamwambia moyo wake kuwa maisha yametawaliwa na mabadiliko, akiwaza kuhusu uzuri na umaarufu wa Pate na jinsi ilivyo sasa ilivyoteketea; nafsi inamweleza moyo kuwa iache tamaa na masuala mengine ya raha za maisha. Nafsi inamwambia moyo kuwa watu wangapi waliokuwa mabwanyenye waliomiliki mali nyingi sana. Watu waliokuwa wana mazuri, waliomiliki vitu vya haja, vya bei ya juu sana, waliokuwa na dhahabu pamoja na fedha. Nafsi inamshauri moyo kwamba uache tamaa na mambo mengi ya raha na anasa maishani

Ewe moyo nenda sijida yake
Hela tafadhali unabihike
Shetani rajimi asikuteke
Kesho kakuona kuwa kamaye

Maana ya tamko hili ‘ewe’ ni moyo wa msikilizaji yeyote.

Haya pia ni mazungumzo ya nafsi na moyo, kwa sababu nafsi inamshauri moyo utekeleze faradhi ya sala. “Sijida” ni neno linalotumika katika sala ya Kiislamu pale ambapo mtu anapoweka kipaji chake chini pamoja na ncha ya pua yake. Matamshi haya baina ya nafsi na moyo hukuza maudhui ya dini, kwa mfano kuwa na unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu. Kipengele hiki cha uzungumzi nafsia hakijajitokeza katika diwani tunayoichambua.

2.2 Tamko ni Jibu la Tamko Lngine

Usemezano hudhihirika pale ambapo washairi au watunzi wa mashairi wanaposemezana kwa kupitia tungo zao. Yaani utungo kuwa jibu kwa utungo mwingine. Katika shairi la Abdalla (1973) ‘Usiniuwe’ (uk. 20) mtunzi anaeleza mawazo yake kuhusu uavyaji wa mimba. Mawazo haya yanaonekana yameathiriwa na imani ya dini ya Kiislamu. Abdalla alitekeleza haya kwa kumpa sauti kijusi ambaye amenyimwa nafasi ya kuishi na mamake ambaye anataka kuavya mimba na kisha kukiua kijusi hiki. Katika shairi hili mtunzi anachora picha halisi ya uhusiano uliopo katika jamii. Katika jamii kuna uhusiano wa kitabaka yaani uhusiano kati ya wenye nguvu na wale dhaifu, hapa ikiwakilishwa na mwenye nguvu ambaye ni mama na yule dhaifu (asiye na nguvu) yaani kijusi. Kijusi hiki kinamsihi mamake kimpesha nafasi ya kuishi hata kama dunia ina majanga kwani kina imani kuwa hakitakosa wa kukitwaa na kukilea. Yeye anasema uhai ni haki yake. Msemaji ni kijusi ilhali msemewa ni mama mjamzito ambaye karibu atajifungua lakini anawaza kuiharibu mimba yake. Kwa sababu ya swala hili ibuka kusheheni Afrika Mashariki, mashairi yametungwa kuhusu swali hili la uavyaji mimba.

Kulingana na Bakhtin tamko ni jibu kwa tamko lingine. Ni kutokana na maoni haya ndipo Ahmad Khamis Ahmad (1978) alitunga shairi lake ‘Hutaniuwa’, naye Habib A. Salim (1977) akatunga shairi lake ‘Nitakuuwa’ yote yakiwa yanajibu shairi la ‘Usiniuwe’. Katika mashairi yote shina la kitenzi ni ‘ua’ yaani tendo la kutoa uhai.

Katika ‘Usiniuwe’ msemaji anayeomba kupewa uhai ni kijusi azungumzaye na kumsihi mamaye. Katika ‘Nitakuuwa’ sauti neni anayesisitiza kwamba atatekeleza tendo la kuua bila kusita ni mama (msemaji) akikiambia kijusi kilicho tumboni (msemewa). Mama aliye mjamzito anasema anahofia mateso ambayo mwanawe atakumbana nayo punde tu atakapozaliwa kwa kuwa hakuwa amepanga

kupata mtoto; kwake mimba yake ilikuwa ajali. Kijusi katika ‘*Hutaniuwa*’ kinajibu sauti ya mamake kwa kumweleza kuwa kina haki ya kuishi na kumlaumu mamake kwa kuwa kiruka njia. Haya mashairi yanadhihirisha usemezano kati ya washairi na kwamba shairi ni jibu la shairi lingine.

Katika ubeti wa ishirini na saba na ishirini na tisa, kijusi kinasema kuwa kimejaribu kulilia haki, uhai na mauti kwa minajili ya kuwarai wamsikilize mamake ili wambakishe angaa aweze kuitazama dunia. Anasema kwa kusikitika sana kuwa kimevumilia na hivyo angetaka wamwombee mama radhi ili asimue. Aidha kijusi hiki kinasema na mauti. Kinamweleza mauti kuwa yasimsichukue kwa kuwa hana vita na mauti kwani hakukosea mauti. Kinamsikitikia hata kinayapigia magoti ili kumshawishi kwamba yasimsikilize mamake.

Katika *Sauti ya Dhiki*, kijusi kinamlaumu mamaye kwa ujauzito ambao naye sasa anataka kuuavya au kuuharibu. Kijusi hiki kinaona afadhali kiitwe mwana haramu kuliko kung’olewa tumboni kife. Kwake yeye anaona afadhali mama afe ili yeye aishi (kijusi).

Lakini katika ‘*Nitakuuwa*’ sauti neni ya mama mjamzito inarejea. Anathibitisha kwamba yu tayari kumuua kijusi kwani tayari anaashiria ameshameza vidonge vya kuharibu mimba. Mama anasisitiza kuwa ni sababu ya mapenzi kwa mwanaye ndiposa ameona ni vyema aavye mimba yake ili asije akateseka wakati atakapozaliwa.

Anasema katika ubeti wa saba na nane kuwa hiyo ndiyo sababu ya yeye kufanya upesi kumweleza hisia zake. Anadai kwamba alipanga kumuua ili mateso ya dunia yakimpata asilaumiwe bali ibakie tu katika roho yake. Mama anasisitiza kuwa mwanaye ayafahamu vyema yale maneno anayomwambia na kutilia maanani. Anasema kwamba anampenda sana mwanaye na angetaka mwanaye ayapime kwenye ratili kisha aelewe kuwa si mapenzi ya mdomo tu wala ya kubuni akilini bali ya kweli.

Mama mjamzito katika kukijibu kijusi kinachoomba kupewa nafasi ya kuishi anasema kuwa yeye hatarajii lawama siku ya hukumu kwa sababu anaamini kuwa kuavya mimba sio kuua ni kama tu kulivunja yai kabla kuku kulitamia. Anasema mtu anawezaje kulaumiwa eti ameua kitu ambacho hata hakikuwa na uhai?.

Tumeona ya kwamba mashairi haya yana maudhui yanayofanana kabisa ya kuavya mimba au kuua yaani tendo la mtu kutoa uhai. Shina la kitenzi katika mashairi yote matatu ni **-ua** (usiniue, nitakuua na hutaniuwa).

‘Nitakuuwa’ pamoja na ‘Hutaniuwa’ ni jibu la ‘Usiniuwe’.

Abdalla (1973) katika shairi lake ‘Tuza moyo’ (uk. 6) shairi ambalo lina beti moja pekee anadhihirisha kuwa usemi ni jibu kwa usemi uliotangulia. Abdalla anadai kwamba alipokuwa kifungoni alitumiwa ujumbe wa kumtuliza. Ujumbe huo ulikuwa umeandikwa kishairi (Abdalla 1973: xiii) na mtu mmoja kati ya wale waliomwonea Abdalla uchungu. Shairi hili lilimtuliza kwa kuwa lilibeba ujumbe wa kushauri. Mtunzi huyu alimpa mawaidha Abdalla kwamba ategemea Maulana kwa kuwa kamwe Rabuka hakosi jibu kwa watu wake na kuwa ni mtetezi kamili.

Abdalla aliandika shairi “Tuza moyo” (uk. 6) ili kulijibu shairi aliloandikiwa na mwenzake (1973: xiii) akimweleza kwamba naye atulize moyo wake wala asifadhaike kwa sababu hakuna lisilokuwa na mwisho kwani siku ya kutolewa gerezani kukiwadia naye hatakuwa na budi kuondoka. Alimwahidi kwamba angesubiri muda utimu na kumuomba Mwenyezi Mungu kwani ameshapata na kuyashika mashauri yake.

Anamwambia atulize moyo wake kwa sababu kilicho na mwanzo lazima kiwe na mwisho wake pia. Siku itakapofika yeye ana imani kuwa ataondoka kifungoni na kuepuka minyororo ya jela. Yeye atazidi tu kutulia na kumuomba Mola wake. Abdilatif alifurahia wasia wake na aliufuata. Dhana hii ya tamko kuwa ni jibu kwa tamko lililotangulia linadhihirika katika diwani ya *Sikate Tamaa*. Hii inajitokeza katika shairi la “Nawaita Washairi” (uk. 3) ambapo mtunzi Said A. Mohamed alitunga utungo huu kama jibu lake kwa washairi wenzake katika mwaka wa sabini pale ambapo kulikuwa na mgogoro mkubwa kati ya wanamapokeo na wanamapinduzi.

2.3 Utendaji

Utendaji ni namna au jinsi ya kufanya jambo. Hiki ni kipengele cha usemezano ambacho kinaruhusu utagusano wa kisemezano katika utendaji ulio katika mjadala, lazima mshairi ajitambulisha kwa hadhira yake.

Kwa mujibu wa Bakhtin (1986) utendaji ni mbinu mojawapo ya lugha; ni namna ya kuzungumza. Mtendaji au mshairi anastahili kuvutia hadhira yake kwa kunasa fikra zao kabisa. Anastahili kutumia ishara na kiimbo yaani kupandisha sauti na kushusha chini sauti. Mtendaji wa shairi anawasilisha ujumbe wake kwa hadhira kwa kupitia toni ya shairi lake. Toni inaweza kuwa kejeli, chuki, huzuni na kushawishi.

Kulingana na Njogu (2004) mshairi anabadilisha kiimbo, mahadhi na sura yake. Hadhira lazima iwe makini ili ipate kusikia na kutekeleza jukumu lake katika utendaji la kuitikia ili kusaidia wahusika kukumbuka kile ambacho kimesemwa. Ubeti mmoja na mwingine huunganishwa kwa kutumia urudiaji au uradidi kwa mfano kurudia kina cha mwisho. Utendaji katika shairi mfano wa gungu, huandamwa na viziada lugha kama vile ishara na vitendo. Msemaji anafahamu kwa kurejelea tajriba zake za pale awali.

Abdulaziz (1979) kuhusu shairi la gungu anasema kuwa, gungu ulikuwa ushairi wa kucheza kule Mombasa. Ulikuwa unachezwa Mombasa hasa katika harusi ama sherehe na mikutano ya siasa. Watunzi wa mashairi wangekutana ili kutiana motisha katika utunzi wa mashairi. Takriban mji mzima ungehudhuria hafla hiyo. Ulikuwa wakati ambao watunzi wangekutana sio tu katika kutumbuiza bali pia kunoana na kubadilishana kauli.

Mfano wa gungu uliotendwa Pate (Njogu 2004:109)

Bwanrehema

Shaha usishike uongo
Sisi hatukulala lango
Henda tukicheza kwa shingo
Inuka twende gunguni.

Shaha

Eeh! Chaa
Eeh mumenililia mabwana
Mwanichuchuliza zijana

Sauti: Ana nini huyu? (kicheko)

Kulingana na Njogu (2004) mmoja wa hadhira anasema ‘Ana nini huyu?’ Swali hili linaelekezwa kwake Shaha alipodai kuwa watendaji wengine wameleta wanawake wadogo ili wamsihi acheze. Basi hivyo ndivyo mmoja wa waliohudhuria alishangaa ni nini Shaha anamaanisha kwa kutaja

wanawake wadogo katika hadhira. Anamaanisha kwamba Shaha anawachokoza na ndipo kicheko kinafuata. Shaha alifanya mzaha ili kupata kuchekesha wasikilizaji; hili lilimchochea kusema kuwa mzaha huo usitiwe gunguni. Hili linadhihirisha kuwa katika utendaji, mzaha unaweza kugeuzwa ili kuchekesha hadhira na kufanya watu kuwa wachangamfu kama ilivyo kwenye gungu. Huu utendaji huwa na viongezi kama vile vitendo na ishara. Hivi viongezi ambavyo havipo katika ushairi huongezwa na watafsiri au watendi wa shairi ili kusababisha utendaji ufikie kile kiwango cha juu cha umilisi. Hili huchangia sana mawasiliano kati ya watendaji na hadhira na zaidi kupitisha maudhui ya kufundisha na kuburudisha.

Usemezano katika ushairi hufikiwa kwa namna mshairi anavyoingiza mitindo tofauti na sauti za kupendeza katika muundo wake. Hili hufanywa kwa kurudiarudia maneno ili kupata mahadhi ama ridhimu inayohitajika. Mfano:

Shaha:

Silaha iko nyumbani, sende wala sende walikuapo kondo
Silaha iko nyumbani, sende walikuapo kondo.

Hadhira:

Sende walikuapo kondo, sende walikuapo kondo
Silaha iko nyumbani, sende walikuapo kondo. (Njogu 2004:125)

Mshairi anatumia istiaru ‘silaha’ kutoa onyo kwa hadhira yake kuwa wasiende vitani kama silaha zao zimo nyumbani. Hii ni kwa sababu kule vitani kuna maadui na basi wanaweza kukumbana naye na kumpa fedheha ama hata huenda akatazamana na mauti. Shairi hutumia istiaru ya vita kwa sababu huchora picha ya ushindi, utukufu na heshima.

Kipengele hiki cha utendaji kimechangia katika kujenga dhamira na maudhui katika shairi hili la gungu. Maudhui yanayojitokeza ni mapambano kwa sababu mshairi ameangazia vita na kwamba ameonya kuwa mtu asiende vitani kama amewacha silaha nyumbani kwani anaweza kufumaniwa. Kipengele hiki hakijadhihirika katika diwani ya *Sikate Tamaa*.

2.4 Majibizano

Majibizano ni hali ambayo mtu au kundi la watu wanatupiana maswali na majibu. Usemezano hujitokeza katika majibizano kwa kupitia wasemaji wawili au vikundi viwili vinavyobadilishana

usemi. Msemaji A anaweza akamuuliza swali msemaji B au msemaji B kutoa kauli kwa msemaji A. Majibizano hutokea mara nyingi katika aina za mashairi ya ngonjera ama malumbano. Majibizano haya yanaweza yakawa katika shairi moja au katika mashairi tofauti.

Haya yanaonekana katika diwani ya Abdalla (1973:17) katika shairi ‘Mnazi: Vuta N’kuvute’. Katika shairi hili mnazi ni mti ambao hutoa matunda (nazi), hivyo basi ili kuchuma nazi mtu yeyote hana budi kukwea mnazi ili ajipatie nazi kutumia. Shairi hili linahusu ndugu wawili Alii na Badi ambao wanamiliki mnazi kama urithi wao. Inaonekana ya kwamba mmoja wao ananufaika kutokana na mti huo wa mnazi. Badi alikuwa katika mnazi akiendelea kuangua kwani hataki kushuka chini, lakini Alii angependa naye apande kwenye mnazi pia naye apate nafasi ya kuchuma nazi ili apate kuipa familia yake. Alii anapomsihi Badi ashuke alikataa. Inaonekana wote wawili walifanya hima katika kupigania uhuru nchini. Hata kama walikuwa na haki sawa, Badi alimpa Alii kitita kidogo sana na yeye kujibakishia buyu zima la asali. Katika hali hii huo ushirikiano ukavunjika na Alii akapewa nafasi ya chini kabisa. Naye akaambiwa iwapo anataka kupanda mnazi tena ni lazima akubaliane na lile agano la awali kuwa mtenda haki. Alii alihisi kwamba zamu yake na familia yake imefika ya kuchuma nazi ambayo ilikuwa urithi kutoka kwa wazazi.

Usemizano kati ya Alii na Badi ni taswira ya kihistoria ambapo wafuasi wa upinzani baada ya uhuru nchini Kenya walikuwa wamefanya kazi pamoja na wanachama wa chama kilichokuwa kikitawala. Walishirikiana wote hadi pale ambapo chama hicho kilichokuwa uongozini kilipoanza kuwabagua wale wa upinzani na hapo ndipo wao walianza kujitenga. Katika ubeti wa ishirini Alii anamweleza Badi kwamba alikubali kushirikiana naye bali yeye alianza kuenda kinyume na kutengana na Alii, hivyo basi Alii aliona ilikuwa vyema kujiondoa kwa kuwa Badi alimnyanyasa.

Hapa tunawaona Alii na Badi wakiwakilisha mawazo ya wanachama wa vyama hivi viwili vya kisiasa, vinavyosimamia matabaka mawili yanayokinzana. Beti hizi zinadhihirisha majibizano haya. Katika ubeti wa kwanza na tatu Alii anamweleza Badi ashuke ili naye apande lakini Badi alikataa katakata na kumjibu Alii kwamba hawezi kamwe kushuka na kwamba yale anayoambiwa ni upuuzi. Alii aliendelea kumrai Badi ashuke chini ili yeye apate kukwea ndipo aweze kuangua nazi ili naye apate kula.

Mshairi katika shairi hili anatuchorea suala la ubinafsi na siasa. Haya yanaonekana pale ambapo mwanasiasa mmoja (Badi) akipata nafasi ya kuongoza anajinufaisha mwenyewe. Anamsahau mwenzake (Alii). Hivyo basi inadhihirika kuwa siasa ni njia ya kumdhulumu mwingine. Majibizano yanajitokeza katika diwani ya *Sikate Tamaa*. Hujidhihirisha katika shairi “Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo” (uk. 20) na malumbano kwenye shairi la “Imani ya Mwana” (uk. 30).

2.5 Usimulizi wa Kisanaa

Usimulizi kwa mujibu wa Wamitila (2002) ni utambaji au maelezo ya jambo fulani. Usimulizi unatazamwa sambamba na kipengele cha wakati. Katika usimulizi sauti neni ni muhimu sana kwa sababu huonyesha ya kwamba, hadithi imesimuliwa kwa nafsi ya kwanza, pili au tatu. Vilevile katika usimulizi, msimulizi na msimuliwa huwekwa makini. Mfano ni *Swifa ya Nguvumali* (1968). Huu ni utenzi simulizi unaosimulia kuhusu kutoweka na kifo cha mwanamke kwa jina Salima na kumtafuta mhalifu katika kijiji cha Mteniapa nchini Tanzania, kule ambako Hassan Bin Ismail aliishi.

Mshairi anaanza kwa kujinyenyekeza mbele ya Muumba kwa kuanza utenzi wake kwa jina la Mola mwenye nguvu na mtume Muhammad. Anaomba Mungu ampe utulivu wakati anatumka shairi ili asiwe na tatizo. Anaomba Maulana ampe ufahamu na kupata elimu na kutia shairini.

(Ub. 2) Nakuomba ya Rabbana
 Unijalie kijana
 Nitungapo shairina
 Pasiwe tena udhia (uk. 1)

Katika utenzi huu, ubeti wa kwanza, pili na tatu, msemewa ni Mungu ambaye ana nguvu za kuumba. Ni Mungu ndiye alimpa mshairi uwezo wa kuutumka utenzi bila shida yoyote. Kwa sababu shairi hutendwa kwenye mikutano ya hadhara, hadhira inayosikiliza pia ni simuliwa.

Tunaona ya kwamba nafsi neni ni ‘ni’ (**nijalie**, **nitungapo** na **nipe**). Inayowakilisha nafsi ya kwanza umoja; nafsi hii ni ya msimulizi. Hii humaanisha ya kuwa mtunzi ndiye anayesimulia shairi lenyewe. Msimuliwa au msemewa ni Mungu, ambaye amewakilishwa na kiwakilishi ‘ku’ (**nakuomba**).

Katika ubeti wa tisa (9) msimuliwa au mzungumziwa amebadilika kutoka Mungu ‘ku’ hadi mwalimu ‘u’ (**unisamehe**). Utenzi huu umedhihirisha kipengele cha usimulizi wa kisanaa kwa sababu unasimulia kisa ambacho ni cha kustaajabisha katika maeneo ya Kilwa kuhusu namna mauaji ya mwanamke mmoja aliyetitwa Salima Hanifu yalivyotekezwa na wachawi.

Mtunzi anadhihirisha usimulizi kwa kupitia msamiati ama maneno teule katika utenzi wake. Katika ubeti wa sita mshairi anasema ‘kukhadithi’ kuonyesha kuwa anaeleza kuhusu jambo. Anasema kuwa anaanza kuhadithia hadithi yao kwamba dunia imebakia tu thuluthi moja kwa sababu imani za watu zimedidimia. Anasema:

6. Nitaanza kukhadithi
Nawaitu khadithi
Dunia baki thuluthi
Imani zimepungua (uk. 1)

Katika utenzi huu usimulizi wa kisanaa umetupa mwangaza kufahamu maudhui ya mtunzi. Maudhui yanayojitokeza katika utenzi huu ni ya uchawi au ushirikina. Hii ni kwa sababu katika utenzi huu, kuna wachawi wanne. Binti Jizi aliyekuwa kiongozi wa wachawi, Bwana Shambi Bin Dima aliyekuwa kinara wa wachawi, Binti Ramadhani na Binti Hanifu aliyeagizwa na wachawi wenzake kuwa atoe ndugu yake mhanga kwa wachawi wenzake (uk. 40). Wachawi hawa waliamini kuwa dawa ambazo wanatumia zinaweza kumwita mtu kutoka pahali alipo na kuenda mpaka penye wachawi hao wapo ili wamfanyie chochote ambacho wangetaka.

Katika ubeti (75-76) inadhihirika kuwa dawa za waganga zilimpeleka Salima Binti Hanifu mpaka akapotea kabisa na wala hakuonekana baada ya wachawi kumchukua. Hakuna ambaye angeweza kulifumbua fumbo hili na hapo ndipo mganga Nguvumali alipendekezwa. Nguvumali akatambua waliotenda kitendo hicho kwa kuwanyesha washukiwa dawa.

Usimulizi wa kisanaa umejitokeza katika diwani ya *Sikate Tamaa*. Mtunzi ametumia methali kusimulia yanayotendeka katika jamii. Haya yameonyeshwa katika mashairi haya: “Uungwana” (uk. 45) ambapo methali hizi zimetumika, kwanza **uungwana sambe, ni jadi kubeli na si kupanda ngazi, usijali kushuka**. “Huba kwa Wazee Wangu” (uk. 47) **damu haiwi maji** na katika shairi la “Muhali” (uk. 48) **hujipalia makaa na ni firauni wa kweli, utayaona mageni**. Aidha miundo ya methali hizi imegeuzwa katika mashairi haya sio kama namna ambavyo zimeandikwa kwa kawaida.

2.6 Uwingi Sauti

Kazi za ushairi huonyesha sauti nyingi tofauti ambazo ziko huru. Wahusika kwa mara nyingi huwa na sauti zilizo na mamlaka sawa na sauti ile ya msimulizi ambayo inahusika katika usemezano na sauti za wahusika wengine. Sauti haiwezi kurejelea msemaji peke yake bali pia hurejelea yale mahusiano yale ya nguvu yanayoathiri na kumweka msomaji katika hali fulani. Kipengee hiki hakijadhihirika katika diwani ya *Sikate Tamaa*.

2.7 Sajili Mbalimbali

Kazi za fasihi huwa zimetumia sajili mbalimbali ili kurahisisha uwasilishaji wa ujumbe. Baadhi ya sajili hizi ni: sajili ya magazeti, sajili ya sheria, sajili ya mazungumzo na sajili ya biashara kama ilivyo katika shairi “Nilipokwenda Dukani”(uk. 24) katika diwani ya *Sikate Tamaa* ambalo hueleza kuhusu matukio pale dukani Baniani alipokuwa anauza bidhaa. Mnunuzi ambaye ni msimulizi katika shairi hili anachora jinsi mambo yalivyokuwa pale dukani ambapo Baniani (mwenye duka) anawahudumia Mzungu (mteja) na mteja wake mwingine (msimulizi). Katika shairi la “Ukoloni na Ukoloni Mamboleo” (uk. 20) sajili ya siasa inadhihirika pale ambapo Ukoloni anatoa hatamu ya uongozi kwa Ukoloni Mambo-Leo kwa kuwa zamu yake ya kuongoza imefika mwisho.

2.8 Kronotopu

Kulingana na Wamitila (2002), kronotopu ni matukio yanayotimbwa haswa katika mpito wa wakati na mahali fulani. Kronotopu kimsingi hurejelea hali ya kazi za kifasihi zinazoweza kukiuka mipaka ya mahali na wakati, kiasi cha kutoweza kuonekana kwamba kazi fulani ya ushairi ni ya kipindi gani au mahali gani. Mfano ni kazi kama *Bina-Adamu* ambayo inaakisi wakati wa kidhahania, usioelekea kuwa na athari za kisaikolojia. Wamitila (2002) anadai kuwa Bakhtin anaamini ya kuwa kuna uhusiano mkubwa sana wa uingilianaji na wa kiutegemeaji kati ya mwanda na wakati. Kazi za kifasihi zinasawiri na kuakisi uhalisi na picha za ulimwengu kwa kutegemea mianda-wakati iliyotofautiana. Kazi hizi zinaweza kuwa na mianda-wakati changamano. Haya hayajajitokeza katika *Sikate Tamaa*.

2.9 Kuwa Na Kani Pewa Na Kani Kitovu

Wamitila (2002) akimrejelea Bakhtin (1981) kani pewa ni sifa ya utanzu fulani au mtindo ambao unaweza kubadilika katika mpito wa wakati huku kani kitovu ni sifa ya utanzu ambayo haibadiliki. Kuna utofauti baina ya kani pewa na kani kitovu. Utofauti huu unaleta upinzani. Upinzani huu unatenganishwa na kani kitovu iletayo mshikamano katika masimulizi au maandishi. Dhana hii ya usemezano haidhihiriki katika *Sikate Tamaa*.

2.10 Kanivali

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) anasema kuwa kipengele kingine kilicho muhimu katika uhakiki wa ki-Bakhtin ni “kanivali” na “ukanivali”. Mhakiki Bakhtin alitumia istilahi “kanivali” kurejelea sherehe ya kitamaduni iliyofanyika kule Ulaya pale ambapo watu walikuwa wanajivisha maguo na mafigu yaliyoficha sura zao. Halafu watu hao wakiwa kwenye hali hiyo walifanya sarakasi na matendo yaliyokuwa yanakwenda kinyume na mambo yanayokubaliwa. Mikhail Bakhtin (1981) alisema vitendo vya kanivali ni vya kiucheshi na havikuwa vinategemea mighani bali vilitegemea uzoefu na uvumbuzi huru. Hutumia wakati ambao tunao ili kuelewa, kusawiri na kutathmini uhalisi wa mambo na kwamba huchanganya mitindo na sauti mbalimbali. Kipengele hiki hakikujitokeza katika diwani ya *Sikate Tamaa*.

Njogu (2004) anasema kwamba kwake Bakhtin, kanivali humaanisha namna ya kuonyesha kuwepo kwa mhusika mwingine. Akimrejelea Bakhtin (1984) aliona hali ya kuwa na mhusika mwingine ”yeye” hutambua kuwa neno la mhusika “mimi” kwa “yeye” huingiliana na hutegemeana mno. Hii ni kwa kuwa, katika muktadha wa usemezano mtu hawezi kujielewa bila kujiunganisha na mhusika mwingine.

2.11 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia vipengele vya usemezano vinavyoonekana katika ushairi wa Kiswahili. Tumevitaja vipengee hivi na kuonyesha jinsi vinavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili. Tumefanya hivyo kwa kutoa mifano kutoka mashairi mbalimbali ya Kiswahili. Tumegundua kwamba vipengele hivi vinachangia katika kujenga dhamira na maudhui ya mwandishi, kwa mfano katika shairi la “Usiniue” (uk. 20) katika *Sauti ya Dhiki* (1973). Tumeweza

kuonyesha kuwa tamko linaweza kuwa jibu kwa tamko lingine. Shairi hili limeangazia maudhui ya uavyaji mimba miongoni mwa wanajamii. Shairi la Habib A. Salim (1977), “Nitakuuwa” ni jibu kwa shairi hili. Abdalla ametumia kijusi kinachomrai mamake asikiue. Katika uchunguzi wetu tumethibitisha kuwa usemezano upo katika ushairi wa Kiswahili kinyume na madai ya Bakhtin (1981) mwasisi wa nadharia ya usemezano.

Sura inayofuata inachambua namna vipengele vya usemezano vinajitokeza katika diwani ya *Sikate Tamaa* na jinsi vinavyoendeleza dhamira na maudhui ya mwandishi.

SURA YA TATU

USEMEZANO KATIKA DIWANI YA SIKATE TAMAA

3.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeangazia vipengele vya usemezano katika diwani ya *Sikate Tamaa*. Tumetoa mifano kwa kulenga mashairi yaliyomo humu kitabuni. Vipengele vifuatavyo ndivyo vitakavyolengwa katika sura hii: majibizano, dhana ya shani kwa msingi wa Bakhtin, sajili mbalimbali, lugha ya wahusika, usemi kuwa ni jibu la usemi, masimulizi ya moja kwa moja ya kifasihi na uhusiano na matini zingine.

3.1 Majibizano

Majibizano ni hali ambayo watu wawili au vikundi viwili vinabadilishana usemi katika hali ya kubishana halafu mwishowe wanakuwa na makubaliano.

Bakhtin (1981,1984) ameishughulikia dhana ya majibizano kama inavyojitokeza katika utanzu wa riwaya kama ilivyotumiwa na mwasisi huyu. Dhana ya majibizano ni nyeti na mara nyingi huishia kuwakanganya watumiaji wake. Unyeti huu unatokana na dhana za majadiliano yenye uhusiano. Kwanza, kuna majibizano kati ya wahusika wawili au zaidi au majadiliano yenye wahusika wawili au zaidi wanaozungumza kama ilivyo katika maongezi ya kawaida. Pili usemi mmoja hufumbata sauti za watu wawili tofauti. Hivi ni kusema kwamba, usemi huo unaweza ukawa jawabu kwa semi zilizotangulia na zitakazofuata. Pamoja na kuwepo kwa uchangamano huu, aina hizi za majadiliano yanayozungumziwa na Bakhtin yanaweza kueleweka kwa kuzingatia diwani ya *Sikate Tamaa*.

Kitengo hiki kinakusudia kufafanua kwa undani jinsi ushairi unavyosemezana na semi ambazo zimechipuka kutoka kwenye ngonjera kwa madhumuni ya kupanua mawasiliano; semi zinazotokana na ngonjera huingizwa kwenye ushairi na washairi kama sitiari katika kuendeleza masemazano. Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1999) ngonjera ni mazungumzo ya kishairi yanayojibizana kuhusu mada fulani mahususi. Mhusika mmoja kawaida huwa anajua mambo zaidi kuliko mhusika au wahusika wengine. Suluhisho hupatikana kufikia hatima ya shairi.

Katika diwani hii kuna mashairi matatu yanayoonyesha majibizano. Hayo ni “Mwanakupata” (uk. 36) “Ukoloni na Mambo-Leo” (uk. 20) na “Imani ya Mwana” (uk. 30).

3.1.1 Mwanakupata

Malumbano yaliyomo ndani ya shairi “Mwanakupata” ni baina ya Mwihaja na Mwanakupata. Majina yao ni ya kimajazi kwani Mwihaja ana haja ya kupata msaada kutoka kwa Mwanakupata ambaye alikwishapata nyadhifa za uongozi.

Maudhui yanayokuzwa katika shairi hili ni masuala ya matabaka katika jamii. Mwanakupata ni mtu katika tabaka la juu na huku Mwihaja ni wa tabaka la chini. Tunamwona Mwihaja akienda kwa nduguye wa zamani Mwanakupata kuomba msaada lakini anafurushwa. Mwihaja katika ubeti wa pili (uk. 36) anaonyesha shabaha ya kuenda kwake Mwanakupata; Mwihaja ni maskini aliye na shida na hivyo angehitaji msaada, kutoka kwa Mwanakupata. Anasema “Niafu haraka, niwe sitarani” ubeti wa kwanza mshororo wa tatu.

Mwanakupata naye katika ubeti wa pili anamkana peupe. Anamwambia kuwa hata hamfahamu, hata atokako na kile kimemleta hakijui. Anamweleza Mwihaja kwamba watu hawaishi kumwomba yeye kila mara na papo hapo anamfukuza nje, bila huruma. Katika ubeti huu mwandishi amekusudia kuonyesha matajiri wanavyowadharau maskini katika jamii. Maudhui yanayoendelezwa ni athari ya matabaka katika jamii.

Mwihaja anazidi kumrai kwa kumkumbusha kwamba walikuwa rafiki walipokuwa wadogo, naye maisha yakamweka jinsi alivyo na akawa fukara na hakuwa na budi kujikaza kisabuni kujipa shughuli na kukabiliana na maisha namna yalivyompata. Haya ni kwa mujibu wa ubeti wa tatu. Ubeti huu unaendeleza maudhui ya uchochole kwani Mwihaja hana mahitaji yanayomtosheleza ndipo akaenda kuomba msaada kutoka kwa Mwanakupata. Anasema “niafu haraka, niwe sitarani” mshororo wa tatu (ub. 2).

Mwanakupata anamkabili Mwihaja na kauli kuwa yeye alipata kwa kuwa ametia jitihada, naye anapokuwa uongozini ni wakati wake wa kula mema na kustarehe, hivyo anamtoa Mwihaja nje. Mwandishi amemtumia mhusika Mwanakupata kukashifu vitendo vya viongozi kwamba wanapopata madaraka wao hujinufaisha na kuwadharau waliowachagua. Haya yameonyeshwa na

Mwanakupata kwa Mwihaja. Katika ubeti huu wa nne, maudhui yanayokuzwa ni ya kiburi. Yamekuzwa na Mwanakupata pale ambapo anajitapa anapokuwa enzini bila hata kumsikiliza Mwihaja.

Katika ubeti wa saba, Mwihaja alihisi kukereka sana kwa maneno ya Mwanakupata, hata akajuta kuenda kwake kwa kuwa alimdunisha sana kiasi kwamba alimwamrisha kutoka nje kimabavu. Mtunzi anachora tabia za viongozi wakiwa madarakani, namna wamejaa kiburi na kero kwani hawawezi kuwasikiza watawaliwa.

3.1.2 Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo

Katika shairi hili ngonjera iliyomo ni baina ya Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo. Mwandishi ametumia majibizano hayo kukuza maudhui ya Ukoloni Mambo-Leo, kuonyesha kwamba waafrika waliotawala baada mkoloni mkongwe walipiga msumari kwenye kidonda, kwani waliwadhulumu waafrika vibaya zaidi kuliko wakoloni wenyewe. Waafrika watawaliwa walibaki wakiwa na majeraha yasiyoisha.

Mkoloni katika ubeti wa kwanza (uk. 20), anasema yeye anaondoka na kumwachia mwafrika mamlaka kwa kuwa zamu yake ya kuongoza imefika ukingoni na hivyo hana budi kung'atuka.

Katika ubeti wa pili, Ukoloni Mambo-Leo unawakilisha viongozi ambao waliuchukua usukani baada ya mzungu kuondoka. Yeye anasema atawadhulumu waafrika sana hata kuliko vile mkoloni alivyowadhakilisha; anasema bila uoga kwamba yeye ni “nge” ambaye atawauma na kusababisha majanga mwilini mwao kwa kuwadhulumu sana. Anaomba apewe nafasi ili awanyanyase waafrika. Katika ubeti huu, Ukoloni Mambo-Leo unaendeleza maudhui ya ukoloni mamboleo. Hii ni kwa sababu unasema kuwa utakuwa mbaya kuliko mkoloni mzungu.

Katika ubeti wa tatu, ni zamu ya Ukoloni kuzungumza; naye anasema kwamba anaondoka kwani alikwisha kataliwa na basi hangetaka tena kupewa lawama. Unadokeza kwamba ulifanya mema katika zamu yake na kuwa hakuwa na budi kuondoka.

Ukoloni Mambo-Leo unasema tena katika ubeti wa nne ukimwambia Ukoloni, kwamba yeye aliamua kuwaruhusu eti wawe katika raha mustarehe basi itakuwa kinaya kwa sababu watakuwa

kwenye shida. Ukoloni Mambo-Leo unaonekana ni katili kabisa aumizaye bila kujali lolote. Mwandishi anaonyesha namna viongozi waafrika ni sumu kwa waafrika wenzao. Ubeti huu kupitia kwa Ukoloni Mambo-Leo unaendeleza maudhui ya ukatili pamoja na ukoloni mamboleo. Mshororo wa tatu katika ubeti wa nne unathibisha haya.

“Yangu nia, wote wawe mashakani”

Ukoloni katika ubeti wa tano (uk. 20) unadai kwamba unang’atuka kwa kuwa ulipokuwa ukiongoza uliambiwa unafanya mambo mabaya, ndipo waafrika walipokasirika na kupigania uhuru wao. Imempasa aondoke kwa kuwa hana nafasi tena. Ukoloni Mambo-Leo nao katika ubeti wa sita unafurahia ukisema basi yeye atakuwa mbaya zaidi kwani pwagu kweli hupata pwaguzi, Atazua vurugu, kuwatesa na kuwaacha vinywa wazi hadi watabadili nia. Maudhui yanayoendelezwa ni uongozi au utawala mbaya. Hii ni kwa kuwa Ukoloni Mambo-Leo unadhamiria punde tu utakapoongoza utanza kuwadhulumu wananchi.

Katika ubeti wa saba Ukoloni unadai kwamba heri waafrika walalamke eti hakuwahudumia kuliko uambiwe utawale tena mara nyingine. Aliona jambo hilo kuwa ni kinyume na ameona ni heri ajipe shughuli. Ukoloni Mambo-Leo unawaambia wanadamu kwamba huwa wao wanaleta dhiki, hivyo basi utawasaliti kabisa wakati utapata nafasi ya kuongoza. Maudhui ya usaliti yanajitokeza kwani Ukoloni unadai kwamba wananchi wanamwendea kinyume.

Mwishoni Ukoloni unaamua kujiondoa na kumpisha Ukoloni Mambo-Leo ushike hatamu kwa kuwa haukutaka ubinafsi, unasema unawaacha watawaliwa wajute. Katika ubeti huu maudhui ya majuto yanajitokeza kutokana na maneno ya Ukoloni “kwa bayana, mwishowe wacha wajute”. Inasawirika kwamba Ukoloni ulichukizwa na waafrika hivyo ungetaka pia wao wajutie kitendo chao cha kujitafutie uhuru na kuulaumu Ukoloni kwamba uliwatenda mabaya.

3.1.3 Imani ya Mwana

Katika shairi hili majibizano yanaendelezwa na wahusika wawili, mwana na mama. Mtunzi anawatumia wahusika hao kujenga maudhui ya ukombozi, athari za mila, desturi, utamaduni pamoja na taasubi ya kiume.

Katika ubeti wa kwanza (uk. 30), mwana anaonekana kumhurumia mamake kwa kuwa anafanya kazi ya sulubu pale nyumbani hadi anachoka sana ilhali hakuna anayemsaidia wala kumwonea huruma. Anamwuliza mamake sababu ya kufanya kazi kama punda bila kupumzika hata kidogo. Jambo hili linatumiza mwana moyoni na kumsababisha kulia kwa kumhurumia mamake. Anamuuliza kwa uchungu mamake kama kweli binadamu aliumbwa ili ateseke maishani.

Mama kwa kumjibu mwanaye katika ubeti wa pili, anamwambia anyamaze kwa kuwa babake ni mkali kupindukia kwamba akizidi kulalama baba anaweza kuwapiga na kuwafurusha waondoke na nyumba waione paa. Anamweleza kwamba kama hataki ugomvi maishani mwake awache kulalama. Mama anamtahadharisha mwanaye asiseme kwa sauti ili baba asisikie kwani akisikia atamletea mama balaa.

Kwenye ubeti wa nne na wa tano mtunzi amemtumia mwana kukuza maudhui ya ndoa na taasubi za kiume. Mwana anaisawiri ndoa ya mama na babake; anaonyesha kwamba imejaa mateso na kutoshirikiana. Baba hafanyi chochote ila yeye ni kula, kufanya kero na kutoa kero na kipigo panapotokea dosari. Mama ndiye anayefanya kazi kipunda; aende shambani, arudi apike chakula kisha baadaye nguo azioshe, chakula kikiisha aondoke akatafute. Baba hafanyi chochote; kazi yake ni kupiga gumzo kwenye mtaa, akirudi anazua zogo kwa mama. Mama ananyanyaswa na kuachiwa majukumu yote, ilhali Baba hamthamini mama hata kidogo.

Katika ubeti wa sita, mwana anaeleza kwamba mamake huenda kukata kuni kisha aufunge mzigo wenyewe ili aelekee nyumbani kwa minajili ya kuandaa chakula kwa kuwa akichelewa baba atamfumana. Ubeti huu unaendeleza maudhui ya nafasi ya mwanamke katika jamii kwamba mwanamke ni shupavu na mwenye bidii. Familia inamtegemea yeye kwa sababu ni nguzo katika nyumba yake.

Kwenye ubeti wa tisa, shairi hili linakuza maudhui ya taasubi ya kiume. Baba anakandwa na mama, anamsinga kwa madawa ilhali hawezi kufanya chochote nyumbani ili kuifaa familia yake. Mama amefanywa kuwa mtumwa; anafanya shughuli zote za nyumbani na huku baba hamthamini, ila imejaa ukali kupindukia. Mama yuko kazini daima yu utumwani. Licha ya kazi hizo zote mama anazozifanya, baba akifika chakula kikiwa hakipo tayari moto unawaka; kipigo huanza. Hata mwana anatamani sana amlinde mamaye.

Kupitia shairi hili la ngonjera, katika ubeti wa kumi na kumi na moja (uk. 32), maudhui ya ukombozi yamefafanuliwa na mshairi. Mwana anamzindua mama. Anamweleza kwamba wakati wa kujikomboa umeshafika, anastahili kujua kwamba haki zake na za baba yake ni sawa kwani wote ni wanadamu walioko kwenye ndoa. Anamzindua mama kwamba aamke ili ajipinde kwa sababu amejitokea nyuma huku akidhulumiwa. Anadai kuwa mama kwa muda mrefu amekuwa akinyanyaswa ndoani na babake.

Mama kwa kujibu usemi wa mwana, anakiri ya kwamba ni kweli amekuwa taabani miaka na mikaka na haikuwa mapenzi yake; hakupenda majanga yaliyompata. Mama anakiri kuwa aliudhika kwa ubaya wa moyo wa baba na pia ameshachoka na kuchushwa naye hivyo anataka kuanza kupigania uhuru na haki yake angaa ajing'oe kutokana na mateso yake. Haya yameonyeshwa katika ubeti huu.

Ub. 11 Mama:

Wanitonesha kidonda, cha miaka na miaka
Usidhani nayapenda, madhila pia mashaka
Nakerwa na yake inda, na sasa nimeshachoka
Naanza kujipinda, kwa mapambano hakika
Hilo nakwambia. (uk. 32).

3.2 Dhana ya Shani kwa Msingi wa Bakhtin

Shani ni kipengele cha usemezano kilichoasisiwa na Bakhtin. Ni jambo linaloshangaza na ambalo si kawaida yake kutokea, kwani linastajabisha. Ni vituko. Ni kushiriki katika mambo ambayo yanaonekana kukera au kuudhi kama vile viongozi kunyanyasa umma. Kipengele hiki kina misingi yake katika uchunguzi wa riwaya ya Mfaransa Francois Rabelais ambayo ilijaribu kuyasarifu maisha katika jamii ya kizungu ya karne ya kumi na sita. Mwamzandi (2002) akimrejelea Bakhtin, *Rabelais and His World* (1984), anaelezea kuwa mtaalamu huyu anaonyesha jinsi jamii za wakati huo zilivyohiari kuivunja kwa makusudi miiko iliyowekwa katika enzi hizo za karne ya kumi na sita. Serikali na makanisa ya wakati huo yangetenga siku maalum ambazo wananchi na viongozi pia wangeshiriki katika mambo yanayoonekana muhali kutendwa siku zingine za kawaida.

Ari kuu ya Said Ahmed katika ushairi wake wa *Sikate Tamaa*, ilikuwa kutumia shani kama kifaa kitumikishi cha kisanaa ambacho kinaonyesha ukinzani wa utesi dhidi ya utawala wa wakati huo. Anatumia shani kupinga matakwa ya viongozi wa kijamii. Msingi huu umetumika na Said Ahmed dhidi ya utawala wa Tanzania na nchi zingine katika bara la Afrika.

Shani imetumka kurejelea jumla ya mambo ambayo yanakiuka miiko na mbeko za wanajamii. Mambo haya kwa kweli ni ya kufedhehesha yanapopatikana katika miktadha ya jamii.

Kiruthu (2002) anasema kuwa Tanzania baada ya uhuru wa mwaka 1961, ilikabiliwa na changamoto kwenye maswala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Tanzania imeweza kukabiliana na changamoto katika uongozi. Kiruthu anaendelea kusema kuwa kulikuwa na mapinduzi mwaka wa 1964 kule Zanzibar. Hili linasemekana misingi yake ilikuwa katika hali mbaya za utendaji kazi, mishahara duni, ufisadi, matakwa mabaya ya kutenda kazi, mwingilio mkubwa wa Waarabu ambao walishikilia nyadhifa kubwa na kumkandamiza Mtanzania wa kawaida.

Haya yanachorwa katika mashairi haya; ‘Watu Hawajali’ (uk. 18), ‘Watoto wa Afrika’(uk. 2), ‘Si Dunia ya kulala’(uk. 3), ‘Wananambia Mchafu’ (uk. 7), ‘Ajabu’ (uk. 9), na “Chui wa kufuga’ (uk. 29).

3.2.1 Watu Hawajali

Katika shairi hili “Watu Hawajali” (uk. 18), mshairi anaonyesha namna ambavyo ukiukaji wa utu unavyodhihirika katika jamii. Maudhui ya ubinafsi na kutowajibika kwa viongozi huonekana kwa uwazi kabisa.

Katika ubeti wa kwanza na pili uzembe umesawiriwa, ambapo imeelezwa ya kwamba ukienda kwenye ofisi watu ambao wanafanya kazi humo hawajali watu wengine hususan mtu mwingine anayeingia ama yule ambaye anapanga kuingia ili apate huduma. Wale wahudumu wako tu mle ndani lakini hawafanyi kazi yao. Hawatekelezi wajibu wao, kwani hawawajibiki na sababu yenyewe haijulikani ni gani. Ukienda kwenye duka, wauza duka hawataki kujua wala hawawezi kuona hitaji la wateja wao. Wao bora wameketi kuwasubiri wateja lakini maslahi yao hawataki kuwatetea.

Kwenye ubeti wa tatu na wa nne, shuleni walimu hawataki kujua kuhusu wanafunzi wao. Watoto wamejaa utundu lakini hakuna anayewarekebisha au kuwaonya badala yake walimu ambao wangukuwa wazazi pale shuleni wao wamejaa chuki mioyoni mwao, na hawajali wanafunzi. Hii ni shani kwani ni kinyume na matarajio. Hospitalini vile vile madaktari hawaoni wagonjwa, hata wale wanaozidiwa hawatibiwi hata hawashughulikiwi hadi pale mwisho wagonjwa wanakata roho. Haieleweki mbona matabibu hawajali hadi wagonjwa wanakufa. Ni jambo la kuhuzunisha na kukera sana. Maudhui yanayokuzwa katika shairi hili ni ya kutowajibika na kutokuwa na utu.

Kwa mujibu wa ubeti wa tano, sita na saba katika viwanda watu wote wanaofanya kazi pale wanaudhi tu, hakuna anayejali maslahi ya mwingine. Vile vile katika upande wa magari watu wako mbioni katika pilkapilka zao za kila siku hakuna anayetaka kujali mwingine. Abiria wakilalama kwa uendeshaji mbaya wa magari wao wanapuuzwa, wanaona kwamba watu hao ni wenye akili timamu na hivyo wanastahili kuwajibikia maisha yao wenyewe. Haya bila shaka ni shani kwa sababu ukweli ni kwamba wanakiuka miiko na mbeko za kibinadamu, na kuishi kama wanyama wa mwituni wasiokuwa na hisia na utu. Ubeti wa saba, unaonyesha kuwa wanadamu hawajali wengine japo wana akili zao timamu kwani wanaishi kama watu walio na wenda wazimu. Beti hizi zinakuza maudhui ya mapuuzwa kwani watu wanaorejelewa kama wale wanaofanya kazi viwandani wanapuuzwa majukumu yao.

3.2.2 Watoto wa Afrika

Shairi hili linadhihirisha kipengele cha shani kwa kiasi kikubwa. Mwandishi ametumia sitiari ya mama na watoto wake. Kwa kawaida mama na watoto wake wanakuwa karibu sana na iwapo watakosana ni kwa muda mfupi tu kisha watasameheana na kuendelea vyema baadaye. Mambo ni tofauti katika shairi hili. Maudhui yanayojitokeza katika shairi hili ni chuki na kero. Pale ambapo mama anaambiwa asidanganyike eti watoto wa Afrika ni wake, bali ang'amue kwamba hawa watoto sio wake, kwani hata wengi wao wanamfitini mama, hivyo mama anaambiwa atoe tumaini lake kwao, kwani wachache sana ndio wanaweza kuwa wanampenda mama kwa dhati. Kulingana na shairi hili mama ni bara la Afrika. Shairi hili, linasawiri wananchi barani Afrika kwamba hawapendi Afrika kwa dhati bali wanaishi tu huku wamechukizwa na Afrika. Wengi wametumiwa kuliharibia Afrika jina, jambo ambalo linakera. Waafrika wenyewe wananyanyasa Afrika kwa

kunyonya uchumi na kuharibu malighafi ya Afrika. Maudhui yanayoendelezwa ni unyanyasaji na usaliti kwani waafrika wanasaliti Afrika.

Maudhui yanayokuzwa katika ubeti wa pili ni maudhui ya chuki na kero. Mama anaambiwa kwamba watoto wake wamenunuliwa ili kumharibia jina, pia kwamba wameibiwa ili kumnyonya damu mama, hivyo mama anatahadharishwa kuwa na makini asiwe na matumaini. Kwa kuwa watoto wake wanamtakia mabaya kiasi cha kudai maisha yake. Tukitazama kwa undani ni kwamba kweli haya hayawezi yakafanyika bali hii ilikuwa njia moja ya mwandishi Mohamed kuonyesha namna ambavyo uongozi wa Tanzania ulikuwa wakati huo. Watu wachache ndio waaminifu na wengi ni wasaliti.

3.2.3 Si Dunia ya Kulala

Katika shairi hili “Si Dunia ya kulala” (uk. 3) kipengele cha shani kinadhihirika. Hii ni kwa kuwa shairi linaonekana kusawiri maudhui ya kutowajibika. Maneno katika ubeti wa kwanza yanasawiri mtu ambaye amechelewa kuamka huku muda wa kuamka ulishafika na hata kupita. Said Ahmed ametumia shani ili kuwashtumu watu ambao wamezembea katika jamii. Anaelezea kwamba kuna wanajamii ambao hawafanyi bidii katika kazi zao za kila siku za kutafuta riziki. Wao wanalala kwa muda mrefu sana bila kujua mahali ambapo watapata mahitaji yao mahususi kama vyakula. Mwandishi anawasuta watu kama hao katika jamii kwa sababu badala ya kuelewa hali na kufanya kazi, wao wanabaki gizani hawafahamu, kitandani bado wanakoroma usingizini. Hili ni jambo linaloshangaza sana kwa kuwa uzembe hulemaza maendeleo katika jamii na kusababisha umaskini. Mtunzi ana dhamira ya kuwahamazisha watu wawe wanawajibika kwa kutekeleza wajibu wao. Maudhui ya umaskini yanaendelezwa kwa kuwa ufukara unadhihirika katika ubeti wa kwanza. Watu wanaorejelewa hawana chakula wala makao.

Katika ubeti wa pili msimuliwa anakumbushwa kwamba yeye ndiye anastahili kuwasaidia wengine na asipowasaidia kutakuwa na majanga, hivyo basi wanajamii wanafaa wawajibike ili kuendeleza maendeleo katika jamii na kufaidi familia zao. Katika kufanya hivyo itawalazimu watoke gizani, wazinduke ili kuamka na kufahamu na kutekeleza wajibu wao na waache usingizi wa pono kisha wafanye kazi kwa bidii. Ubeti huu wa pili unawahamasisha watu watekeleze wajibu wao kwa kuwa

watu ndio wanaofaa wakati wa dhiki. Hivyo itawalazimu wapambane kwa kuwa katika dunia lazima mtu ajizatiti.

3.2.4 Wananambia Mchafu

Nafsi neni katika shairi hili ni mwanamke ambaye anahisi amedharauliwa ‘wananisubu siujali uke wangu’. Shairi hili linaonyesha huzuni. Hii ni kwa kuwa mwanamke anasimulia yale machungu ambayo ametendewa na watu katika jamii “wananambia mchafu”.

Kipengee cha shani kinadhihirika katika shairi hili kwa kuwa mambo anayoambiwa mwanamke huyu ni ya kustaajibisha na yanavunja desturi za waafrika na za kibinadamu. Kwa mfano, kutaja siri zake hadharani. Maudhui ya dharau na ukosefu wa utu yanaonekana katika shairi hili zima kwa kuwa huyu mwanamke anaambiwa kwamba ameharibu utu wake na kuchafua jina lake; kisha zaidi ya haya wanamfunua watu waone na kujua siri zake bila ya kutambua kinachomtatiza yeye. Haya yanadhihirika katika ubeti wa kwanza (uk. 7).

Mwanamke huyu anasema kuwa ni jambo la kukera sana wanaposema kwamba matendo yake ni maovu, eti yeye anatoa nguo zake hadharani na kuwa hajali wala hafuniki uchi wake. Bila shaka mtu ambaye ana akili zake timamu hawezi akafanya mambo kama hayo, licha ya kuwa anaweza akakumbwa na shida nyingi. Maswala haya yamepita mipaka na ndivyo tunaeleza kuwa ni shani. Haya yanaonekana katika ubeti wa pili (uk. 7).

Katika ubeti wa tatu na wa nne, msimulizi anasema kuwa watu wanazungumza vibaya kuhusu asili yake, mavazi anayoyavaa na vilevile wanamharibia kazi zake na ilhali hawajui matatizo yake. Anaendelea kusema kwamba wazazi wake wanamlaani, kwa kumwambia kwamba yeye hata hamheshimu Jalali na fauka ya haya wanamtakia mabaya kiasi cha kwamba wanasema hawatahudhuria mazishi yake yaani wanamtakia mwana wao afe! Mambo haya kabisa ni shani ndiposa tunasema yanakiuka miiko ya jamii za Kiafrika. Wazazi hawawezi kunenea na kumtabiria mwana wao kifo na hawastahili kusema kuwa hawatahudhuria mazishi ya mtoto wao ilhali ni damu yao. Ni jambo ambalo dhahiri linastajibisha hata kama mwana wao alikuwa mtu mbaya sana. Wazazi wake wamevuka mipaka ya utu. Ubeti huu unaendeleza maudhui ya ukatili, nafasi ya

mwanamke katika jamii kuwa mwanamke ameonewa katika jamii hivi kwamba anadunishwa kama mtu asiyekamilika.

Msimulizi (mwanamke) anasema kuwa watu hawamtaki kwani hawataki kujua tatizo linalomkabili; hawataki kufahamu chanzo cha yeye kuwa mchafu. Hawataki kujua furaha na huzuni yake. Ubeti huu unaonyesha maudhui ya ubinafsi katika jamii, pale watu wanajijali wenyewe bila ya kuwajali wengine. Isitoshe maudhui ya ubaguzi wa wanawake yakuzwa katika shairi hili kwani mwanamke ametengwa kwa kuwa hakuna anayetaka kujua kuhusu hali yake. Mshororo huu katika ubeti wa tano unaangazia haya.

“Hawatafuti, wakajua shida zangu” (uk. 7).

3.2.5 Ajabu

Shairi hili “Ajabu” (uk. 9) linaendeleza maudhui ya ubaguzi. Yanayodhihirika katika shairi ni yale yanayokiuka desturi za ubinadamu yaani shani. Kwani mambo hutendeka nyuma mbele. Yule mtu anayestahili kupewa au kutimiziwa haki zake hawezi kupewa haki na yule akiukaye ndiye anapewa haki. Yule ambaye amelima shamba lake havuni mavuno bali ambaye hakuhusika hata kidogo ndiye anavuna. Mohamed ametumia kipengele hiki cha shani ili kufungua macho wanajamii na kukashifu uongozi mbaya katika jamii na nchi za kiafrika kwa jumla.

Mwenye hoja za kuwasilisha hapewi nafasi ya kuwasilisha hoja zake ni yule ambaye hana hoja ama jambo la kuwasilisha ndiye anatunukiwa. Kisha yule asiye na jambo muhimu la kusema wala hawezi kuona kilichokuwa kimetendeka hapo awali, anasema chochote kisichofaa huku akimkabili mbele mwenye kustahili haki mbele ili kumharibia ndoto zake. Hili ni jambo la kustaajibisha mno. Haya yanaonekana katika ubeti wa kwanza. Maudhui yanayokuzwa ni ya ubinafsi kwa kuwa watu walio na nafasi ya kupunja watu wanafanya hivyo ili wenyewe wajinufaishe.

Mshairi anaonyesha kuwa kuna unyonyaji katika jamii. Anaashiria haya katika ubeti wa pili pale anaposema kuwa watu wanaolima hawawezi kula lakini wale ambao hawalimi, yaani wale wasiojua maana ya uandalizi wa konde ndio wenye kula na kuvuna tena sana. Wanakula vitu visivyo vya halali kwa kuwa hawakuvitolea jasho. Pia katika ubeti wa tatu, mshairi anasema ya

kwamba wale wanaofanya kazi kwa bidii hadi wakachoka hawapati nafasi ya kupata angaa lepe la usingizi ilhali wale wasiojukumika na wasiojishughulisha wako vyema. Hii ni kwa sababu wamejistarehesha kwa kulala pahali pazuri mno hadi wanakoroma.

Mshairi anasema anashangaa kuona kuwa wale wanaotenda mema wanadharauliwa lakini wale wasiotenda wanamiminiwa sifa nyingi mno. Hilo ni kero au jambo la kuudhi yaaani shani. Tumeona shani kwa mujibu wa shairi hili inaendeleza maudhui ya matabaka. Hii ni kwa sababu katika ubeti wa nne watu ambao ni watumishi na watumikiwa yaani wachochole na mabwanyenye wameangaziwa. Watumishi hawaonekani muhimu ilhali wanaotumikiwa wanasifiwa sana.

3.2.6 Chui wa Kufuga

Shairi hili linadhihirisha kipengee cha shani kwa kuwa mshairi katika shairi hili amesawiri viongozi ambao walikabidhiwa nyadhifa za uongozi lakini mwishowe walienda kinyume na matakwa ya wanajamii. Viongozi hawa waligeuka na kuwa wakatili mno, waligeuka na kuwa kama chatu anayemeza au kama chui anayeuma.

Katika ubeti wa pili (uk. 29) msimulizi anasema kuwa alipokuwa makini na kutazama kwa jicho pevu akaona kuwa kuna tendo la ulafi ndani ya wale waliowachagua. Tendo hilo lilimfanya kuonelea viongozi hawa watupwe kabisa kwa kuwa wao ni watu wasiojali fauka ya haya wana mawazo mabaya. Wanatenda maovu yasiyopendeza na yanavyoudhi. Tabia zao hazipendezi katu.

Katika ubeti wa tatu mshairi ametumia sitiari ya chui kumaanisha viongozi katili. Anasema kuwa wale waliochaguliwa walikuwa wanakiuka hali ya ubinadamu kwani walikuwa wanyama yaani machui wala watu. Hawa ni viongozi wanaowahini wapiga kura. Hili linamsababisha msimulizi kushangaa na kufikiri kuwa hawa ni chui kwamba sio wanadamu. Mwandishi anasema ‘chui wa kufuga’ kwa sababu walipochaguliwa wakawa wanatumia vyeo vyao kujinufaisha au kujilisha namna ambavyo mifugo hulishwa na mfugaji. Maudhui yanayokuzwa ni ya ukatili kwa kuwa viongozi hao wanaunyanyasa umma.

Katika ubeti wa nne wanajamii wanasema walidhani walipata viongozi wanaowaza na kutekeleza mema, kumbe walikuwa watu hatari na hawangetunukiwa uwezo wa kuongoza maana waligeuka

chatu wanawameza watu na kuwajeruhi mno. Mambo haya yanakera sana. Maudhui yanayoendelezwa na ubeti huu ni ya ukatili kwa kuwa waliopewa uongozi wanawanyasya waliowachagua.

Kwenye ubeti wa tano, wanajamii badala ya kupata matokeo mazuri baada ya uchaguzi wanapokea vitendo vya unyama kutoka kwa viongozi. Hasara waliyoipokea ni kubwa sana kushinda faida, hivyo shani imejitokeza kupitia kwa viongozi wanapoenda kinyume na matakwa ya jamii. Hali hii imekuza maudhui ya ukatili kwa kuwa viongozi wameutendea umma mabaya, jambo ambalo limesababisha hasara katika jamii. Viongozi hawa wameelekea kuwa wanyama wakatili kwa wanajamii. Aidha hawajali maslahi ya umma bali wamekuwa wabinafsi.

3.3 Sajili Mbalimbali

Bakhtin (1981) anasema kwamba ni katika matumizi ya sajili tofauti ambapo usemezano huweza kupatikana katika matini. Katika diwani ya *Sikate Tamaa* kuna matumizi ya sajili. Sajili zinazoonekana katika kazi hii ni sajili ya biashara katika shairi “Nilipokwenda Dukani” (uk. 24), sajili ya matangazo ya redioni katika shairi la “Siku Njema”(uk. 5) na sajili ya siasa katika shairi la “Ukoloni na Mambo-Leo” (uk. 20).

3.3.1 Sajili ya Biashara (Dukani)

Katika sajili ya biashara, kuna watu wawili wanaobadilishana usemi, yule anayehitaji bidhaa na yule anayezitoa. Kuna mnunuzi na muuzaji. Baniani auzaye duka na mteja anunuaye. Haya yanaonekana katika shairi hili; mnunuzi ndiye ambaye ni msimulizi katika shairi hili. Msimulizi ameenda dukani kwa baniani kununua saruni. Baniani alimpuuza mteja huyu alipomwona mteja mzungu ambaye alionekana kuwa wa hali ya juu kuliko mteja anayesimulia. Mteja anayesimulia alidhamiria kupewa saruni huku yeye akipeana hela kama malipo ya saruni. Hii ni ishara ya sajili ya biashara kwa kuwa lazima kuwe na ubadilishanaji wa bidhaa na pesa vile vile.

Katika ubeti wa pili baniani anapata mteja wa pili ambaye ni mzungu. Baniani akamhudumia mteja mzungu. Hivyo tunaona sajili hii ya biashara ikiendelezwa na baniani, mteja msimulizi na mteja mzungu. Maudhui yanayokuzwa katika sajili hii ya biashara ni ubaguzi wa rangi. Hii ni kwa sababu baniani alipomwona mteja mzungu alimwacha au kumpuuza mteja wa kwanza aliyetaka kununua

saruni na kumhudumia mzungu kwa sababu ya rangi ya ngozi yake na hadhi yake. Maudhui mengine yanayojitokeza ni utabaka. Hii ni kwa kuwa baniani amembagua mteja wa kwanza na kumhudumia mteja mzungu kwa kuwa aliwazia kwamba ana uwezo wa kuwa na pesa zaidi ya mteja wa kwanza aliyeonekana mlalahoi. Alichukulia kuwa mzungu ana uwezo mkubwa wa kifedha; mlalahai.

3.3.2 Sajili ya Matangazo

Katika shairi la “Siku Njema” (uk. 6), sajili ya matangazo imejitokeza. Sajili hii hudhihirika pale ambapo kuna tangazo ambalo hutolewa au hupitishwa kwa kutumia redio, runinga na magazeti. Katika shairi hili redio ilitangaza habari kwamba siku ilikuwa njema, wanajamii wakaamini matangazo hayo na kuchangamkia, lakini ukweli ni kwamba kulikuwa kumejaa changamoto zilizosababisha siku kuwa mbaya.

Kupitia kwa matangazo hayo, tunapata maudhui ya ukatili na unafiki katika jamii. Shairi hili kwa mujibu wa anwani “Siku Njema” ni kinaya kwa kuwa ukweli ni kuwa sio siku njema bali mambo ni mabaya mno. Uhalisia wa mambo ni kinyume na matangazo redioni. Hili ni jambo la kukera sana. Kupitia kwa sajili hii maudhui ya unafiki yanakuzwa yaani ni hali ya kutokuwa mkweli kwa minajili ya kupata kitu fulani ama nafasi fulani.

3.3.3 Sajili ya Siasa

Katika shairi la “Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo” (uk. 20), sajili ya siasa imejitokeza. Sajili hii inadhihirika pale ambapo kuna mvutano wa kisiasa baina ya wahusika wawili katika shairi hili. Wahusika hawa ni Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo. Wao wanazungumza kuhusu uongozi. Ukoloni unasema ungetaka kuondoka kwa kuwa zamu yake ya kuongoza umefikia hatima. Ukoloni unasema ungetaka kumpisha Ukoloni Mambo-Leo uendeleze uongozi huu kwa kuwa ulidhamiria kuondoka kwani haukuwa na haja ya mgogoro.

Ukoloni Mambo-Leo unasema uko tayari kutawala, hivyo basi unaomba upewe nafasi. Inaonekana kwamba una nia ya kuwatesa watawaliwa punde tu ukipewa fursa. Unasema kuwa utawaumiza vibaya hadi walie na unadai ya kwamba utawauma watawaliwa kama nge aumavyo. Misamiati ya sajili hii ya siasa inaonekana kama vile; “nakuacha utawale”, “zamu zangu ni za kale” na “uhuru kung’ang’ania”. Kwa mujibu wa sajili hii ya siasa maudhui ya usaliti na ukoloni mamboleo

yamekuzwa pale ambapo Ukoloni: Mambo-Leo unasema utawatesa wananchi kabisa. Pia kuna maudhui ya siasa. Hii ni kwa kuwa Ukoloni Mambo-Leo unaomba Ukoloni umpe nafasi ya uongozi.

3.4 Lugha ya Wahusika

Wahusika hupewa lugha wanayotumia kutegemea na majukumu yao. Kulingana na Bakhtin (1981) lugha ambayo wahusika hupewa huonyesha matumaini ya mwandishi kwa sababu lugha yao huwa ya “wengine” Mtunzi ametumia lugha shaurifu. Mfano katika shairi lake la kwanza “Sikate Tamaa” (uk. 1).

3.4.1 Sikate Tamaa

Katika shairi hili, lugha yenye matumaini imetumika, lugha iliyo na mvuto. Mtunzi katika ubeti wa kwanza ametumia lugha shaurifu. Katika ubeti wa kwanza ametumia lugha inayotia moyo, yaani lugha yenye mwelekeo mzuri ili kuwapa matumaini wajikaze hata wakipata msukosuko wasije wakafa moyo.

Ub. 1 Umeanguka, inuka, simama kama mnazi
Umechunika, inuka, tia dawa kwa ujuzi
Sasa inuka, inuka kijana ianze kazi
Sikate tamaa

Katika ubeti wa pili vile vile mtunzi amewapa wahusika wake lugha shaurifu “usife moyo” “nyanyuka” “anza tena kujipinda”, msemewa anapewa ushauri ya kwamba ajikaze, kwa kuwa ulimwengu una majanga mengi sana na kwamba hana budi kujitahidi “dunia baa hivyo itabidi ajikakamue”.

Mtunzi kwenye ubeti wa nne pia ametumia lugha arifu na zindushi. Lugha inayomfumbua mtu macho. Kijana (msemewa) anaarifiwa kwamba yeye ana nguvu hivyo anastahili asimame kidete na apambane na adui zake; anazinduliwa kuwa ana akili hivyo aepuke mipango yao mibaya naye ajifunze daima kuwa na uvumilivu. Lugha ya wahusika imekuza maudhui ya ushauri, matumaini, mapambano pamoja na utetezi wa haki. Hii ni kwa sababu inachochea mtu kutetea na kupigania haki yake licha ya kuwa dunia ina matatizo tele.

3.4.2 Nawaita Washairi

Katika shairi hili nafsi neni ni mwandishi. Lugha aliyoitumia Said Ahmed katika shairi hili ni yenye matumaini. Hii inatueleza mwelekeo mwema wa mwandishi kuhusiana na utunzi. Katika ubeti wa kwanza ukurasa wa tatu ametumia lugha shaurifu, anawaambia watunzi wenza kwamba washikane yaani wawe na umoja katika shughuli za utungaji wa mashairi. Waache mabishano na watunge mashairi kwa moyo uliojasirika kwa kuwa mashindano hayatawafikisha pahali popote. Lugha hii shaurifu inakuza maudhui ya umoja na ushirikiano kwamba washairi wawe na umoja kwa kuwa wanategemeana na kuingiliana.

Mtunzi katika ubeti wa pili ametumia lugha shaurifu vile vile. Anasema “tuyafichue mavundo” “tukishikilia upendo” Anawashauri watunzi wenzake kwamba wawe wabunifu, huku wakitenda wema, waonyeshe umahiri mkubwa na wawe na upendo ili waendeleze utanzu huu wa ushairi waandike kwa hima, tena kwa ufundi mkubwa. Lugha hii inachangia maudhui ya amani na upendo. Hii ni kuwa watunzi wakipendana inachochea kuwavuta na kuwapalilia watunzi wengine wanya wachipuke.

3.5 Usemi Kuwa ni Jibu la Usemi

Kwa mujibu wa Bakhtin (1981:127) jibu katika usemezano ni ule msisimko anaoupata mtu wakati tamko fulani linapotamkwa. Msisimko huu unaweza kuwa wa kupinga tamko lile, kulitolea rai, kulizidisha nguvu ama kulipunguzia. Hata mtu asipolijibu kwa kutamka, ukimya wa msemzwa hutafsiriwa na msemza kuwa ni jibu. Jibu si lazima litoke papo kwa hapo, walakini hata jibu hili likiachwa hadi hapo baadaye bado pia huo ni msisimko aliuopata msemzwa. Ni kutokana na majibu ndio ile dhana ya usemezano inajitokeza. Matamshi yako katika usemezano. Hata kama mtu ndio yanza kusema ama kutamka, matamshi yake hayatokani na ombwe tupu bali kuna yule anayemtangulia katika kusema ikiwa sio leo, jana, juzi, au siku yoyote ile. Hakuna mwanadamu yeyote anayedai ya kwamba tamko fulani yeye ndiye alikuwa mtu wa kwanza kulitamka isipokuwa Adamu pekee.

Kama vile *Inkishafi* ni jibu la Sayyid Abdalla kwa umma uliokuweco wakati huo na wa siku zijazo (Karama 1996), katika *Sikate Tamaa* shairi la “Nawaita Washairi” ni jibu la S.A Mohamed kwa washairi wenzake mwaka wa sabini ambapo kuliweco na mgogoro mkubwa sana kati ya

wanamapokeo na wanamapinduzi kuhusu muundo wa shairi la Kiswahili kama unafaa kufuata muundo wa vina na mizani au la. Kulingana na wanamapokeo, kama vile Abedi (1954), shairi huwa na sifa kama vile ya vina na urari wa mizani, ufasaha wa maneno, maneno ya mkato, lugha nzito ya kuvutia, uvutaji wa moyo, maneno ya hekima, fikra za ndani na lazima liweze kuimbika. Nao wanausasa ambao ushairi wao uliitwa mapingiti kama vile Kazilahabi (1977) na Mazrui (1988) wanasema kuwa si lazima shairi liwe na sifa hizi zote, bali wanasisitiza sana sifa za lugha na maudhui. Ni katika muktadha huu ndipo S.A Mohamed aliandika shairi” Nawaita Washairi” (uk. 3).

Anasema katika ubeti wa kwanza kwamba anawaita washairi wawe na umoja, (“tukutanishe mikono”) katika mwito wa utungaji wa ushairi, waache mabishano na mashindano. Japo kuna changamoto, wanastahili waandike kwa hamu sana ili watu wengine washiriki uhondo .

Katika ubeti wa pili Mohamed anasema kwamba washairi wageuze mitindo katika hali nzuri bila ugomvi ili waondoe kilicho kibaya na waonyeshe mivutano ilipo. Anashauri kuwa wote wawe na upendo, wawe watulivu na wenye bidii ili waweze kutunga mashairi kwa msisimko mkubwa sana. Haya yanaendeleza maudhui ya umoja na ushirikiano ili utungaji wa mashairi ufane kabisa.

3.6 Masimulizi ya Moja kwa Moja ya Kifasihi

Bakhtin (1981) amesema kwamba mwandishi hutumia masimulizi ya kifasihi moja kwa moja katika uandishi wa kifasihi ndipo ikawa na usemezano. Madai yetu ni kwamba masimulizi ya moja kwa moja ya kifasihi huendeleza maudhui ya mtunzi. Katika kazi ya fasihi masimulizi haya ni hadithi, methali, nyimbo, mashairi, mafumbo na michezo ya kuigiza. Matumizi ya tanzu zozote za fasihi simulizi huthaminiwa na kuenziwa kama njia mwafaka ya wanajamii hao ya kuielewa dunia yao. Kwa utaratibu huu tunaweza kusema au tukadai kuwa fasihi simulizi imefumbata semi za watu wengi ambazo zinafanikisha kazi ya kifasihi. Fasihi simulizi inaweza dumu na inaweza kupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine bila kupoteza thamani yake kwa urahisi.

Sikate Tamaa kama sanaa ya ushairi haikuachwa nyuma katika jambo hili. Uchunguzi wetu umeonyesha kuwa ushairi wa S.A Mohamed umetumia chembechembe ya fasihi simulizi kama vile methali.

3.6.1 Methali

Methali ina sifa ya kufafanua semi mbalimbali za wanajamii. Ukweli ni kwamba utanzu huu wa fasihi simulizi, huelezea kwa kifupi busara za wanajamii ambao hutumia methali hizo. (Njogu na Chimera 1999). Methali zinapotumiwa hunuiwa kuwasilisha swala, hali na kisha kuliambatanisha na mafunzo au maadili fulani yanayopendekezwa na jamii husika.

Katika fasihi simulizi ya Kiswahili, utanzu wa methali una uwiano mkubwa kabisa na ushairi. Sababu mojawapo ya ukaribu huo ni ile sifa ya methali kutumia lugha kwa mukhtasari ambayo ni sifa jumuishi ya ushairi. Methali hufafanua jumla ya busara za wanajamii kwa kuelezea yanayoelezwa katika ushairi.

3.6.1.1 Uungwana Sambe ni Jadi Kubeli

Maana ya methali hii ni kwamba mtu kuwa muungwana si lazima awe anatoka katika ukoo wenye utukufu ama unaojulikana bali utu wa mtu hutokana na usafi wa moyo. Watu wajigambao kwa utukufu wa asili za familia zao hupigiwa methali hii.

Mtunzi katika shairi la “Uungwana” (uk. 45) ametumia methali hii kama kibwagizo katika shairi hili. Kibwagizo hiki kimejirudia kutoka ubeti wa kwanza hadi ule wa mwisho. Methali hii hubeba ujumbe wa shairi kuwa uungwana ni utu na usafi wa moyo bali si kumiliki mali au asili za ukoo wa watu. Mtunzi ametumia methali hii kuwapigia watu wajitapao katika jamii kwa sababu ya utukufu wa familia zao. Katika ubeti wa pili mshairi anaelezea uungwana hautokani na kujenga nyumba za kifahari kisha kuanza kujigamba kwa uzuri wake bali uungwana hutokana na utu wa mtu. Anaendelea kusema katika ubeti wa nne kuwa ngozi ya mwili ikiwa imerembeka na kupambika vizuri huku mtu hafanyi chochote duniani cha kupendeza, uungwana bado haujaafikiwa kwani uungwana ni utu.

Katika ubeti wa sita mshairi anasema mtu hastahili kujiremba na kujigamba kwa sababu ya ukoo wao au uhusiano wa ndugu zake kwani atajiumiza mwenyewe. Hastahili kabisa kwa kuwa atajipa taabu na kupata hasara. Uungwana si kutoka ukoo mtukufu bali kutokana na fikra na matendo yake mazuri.

Methali hii imetumiwa na mwandishi kwa minajili ya kuchangia maudhui ya utu. Hii ni sababu inaeleza kwamba uungwana hautokani na mali nyingi na nyumba za kifahari zinazopendeza na kutamanika bali uungwana hutokana na utu wa mtu. Hivyo hufundisha wanajamii kuwa na utu maishani.

3.6.1.2 Si Kupanda Ngazi, Usijali Kushuka Chini

Methali hii imetumika katika ubeti wa sita katika shairi “Uungwana” (uk. 45). Maana ya methali hii ni kwamba mtu anayefanikiwa anastahili kuwa makini kwa kuwa ni rahisi kuharibikiwa. Mwandishi ametumia methali hii kutoa tofauti iliyopo kati ya uungwana na uongozi. Amesema hivi ili kuwatahadharisha wanajamii wale wanaojitapa kwa mali au asili yao. Anawakumbusha uungwana sio kama ngozi kwenye mwili wa binadamu na wala sio kama uongozi ambapo wakati mwingine mtu hupewa hatamu au kushindwa kwenye uchaguzi. Wala uungwana sio jambo la kutumia kujigamba. Amekariri ujumbe wake wa kukashifu majivuno. Methali hii imekuza maudhui ya ubinadamu au utu kwa kuwa inawaonya watu walio kwenye madaraka wasiwadharau walio chini yao kwa kuwa jambo hilo sio uungwana hata kidogo.

3.6.1.3 Damu Haiwi Maji

Methali hii kulingana na Ndalu A. na King’ei K. (1989) humaanisha ya kwamba watu wenye ukoo wa damu husaidiana sana kuliko rafiki au jamaa wa mbali nao. Methali imetumiwa katika shairi “Huba kwa Wazee Wangu” (uk. 47), ubeti wa kumi na moja.

Katika shairi hili mwana atoa shukrani kwa wazazi wake waliomlea vyema alipokuwa katika umri wa utotoni. Katika ubeti wa kumi na moja mwana anasema asante kwa babake ambaye alipokuwa hai alimfaa sana. Anamshukuru akisema kuwa baba na mama yake walimpa msingi mwema maishani. Anasema kuwa imani yao ilikuwa ngao katika maisha yake. Hivyo anasema damu kweli hakuna wakati itakuwa maji. Watu wa karibu sana wa ukoo si sawa na marafiki walioko mbali ndipo anatambua usaidizi wa wazazi wake na kutoa shukrani. Methali hii inaendeleza maudhui ya malezi mema katika jamii na nafasi ya wazazi katika malezi ya watoto wao.

Mwana anatambua umuhimu wa wazazi hususan baba katika maisha yake ya utotoni. Anasema wazazi wake walimwekea msingi imara maishani. Mtunzi ametumia methali hii ili kuonyesha umuhimu wa jamaa au mtu yeyote wa ukoo kuliko rafiki wa mbali katika malezi ya watoto.

3.6.1.4 Hujipalia Makaa

Methali hii imetumika katika shairi la “Muhali” (uk. 48). Maana ya methali hii ni kujiletea balaa au shida. Muhali ni ugumu wa kukataa jambo fulani au wazo. Mtunzi anasema katika ubeti wa nne kuwa muhali ni tendo ambalo linakera sana lakini watu wengi hujipata wamejihusisha nalo, badala ya kujitenga nalo. Wanajipata tayari wamelitenda. Hii ndio sababu mtunzi ametumia methali kuelimisha wanajamii kuwa watakuwa wanajiharibia jina au hata kujiletea shida wanapojihusisha na muhali kwani watajipaka tope kama samaki pweza. Methali hii imechangia kuendeleza maudhui ya ushauri kwa kuwa inaelekeza au kutoa mwongozo kwa wanajamii wawe makini kwa matendo yao ili wasije wakajidharau baadaye.

3.6.1.4 Ni Firauni wa Kweli, Utayaona Mageni

Methali hii imetumika katika ubeti wa tisa katika shairi la “Muhali” (uk. 48). Maana yake ni kuwa mja hafai kushtuka kwa maswala madogo madogo haswa anapoyaona, kwa kuwa kuna mengi ya kushangaza na kustaajabisha zaidi. Mtunzi ametumia methali kuwaonya wanajamii dhidi ya muhali. Anasema mtu akifanya jambo gumu bila kujua matokeo yake ataumia sana maishani mwake, kwani huenda ang’olewe jino au apigwe kichapo cha mbwa. Hivyo mtunzi anatoa tahadhari. Methali hii inakuza maudhui ya mawaidha. Hii ni kwa sababu inashauri watu katika jamii ili wawe na ujasiri, wasishangazwe na mambo madogo kwa kuwa kuna magumu zaidi.

3.7 Uhusiano na Matini Zingine

Katika usemezano, matini mbalimbali huweza kuhusiana na kuathiriana (Bakhtin 1981). Matini huhusiana pengine kwa kutajwa au hutumiwa ili kufafanua zaidi matini nyingine. Hii ni kwa sababu katika kuelezea kuhusu dhana fulani, matini tofauti zinaweza zikatajwa au kuhusiana na dhana iliyotajwa. Matini huathiriana kutokana na kwamba nafsi mbili huweza kujitambulisha na jinsi ambavyo zimetumika. Nafsi moja haiwezi ikaanza kutumiwa hadi ijue nafsi nyingine inasema nini.

Ni katika muktadha huu wa kuathiriana ambapo tumejadili athari na uhusiano wa matini nyinginezo na mashairi ya Said. A. Mohamed, hususan “Ndoto” (uk. 26) na “Mtu Hachagui Kazi” (uk. 23).

3.7.1 Mtu Hachagui Kazi

Katika shairi hili “Mtu Hachagui Kazi” (uk. 23), mwandishi anafanunua umuhimu wa kufanya kazi katika jamii. Anaendelea kueleza haya maudhui ya kazi kwa kutaja kuwa “kazi ni kitu azizi” kuliko vitu vingine. Ni wajibu wa kila mwanajamii kufanya na kuipenda kazi kwa moyo wa dhati ili ayashinde majanga ya njaa na uvivu. Anawahimiza wanajamii wasiwe wepesi wa kuchagua kazi wala waibague kwa kuwa kila kazi ina umuhimu wake. Anaeleza kwamba kazi ni kazi mradi inamsaidia mtu kupata riziki. Mtunzi ametaja aina nyingi za kazi, kama vile upagazi, kushona, kulima, ukwezi na uvuvi.

Kwenye ubeti wa tatu, mtunzi anasema hakuna kazi ya kiwango cha chini hivyo basi mtu asiidharau. Anasema kuwa madharau ni ugonjwa mkubwa sana na hata ni unyama. Kazi zote zina umuhimu hivyo wanajamii wasibague hata kidogo bali wakubali na kufanya kwa upendo na dhati ya moyo.

Katika ubeti wa pili, mshairi anasema binadamu hastahili kuipuuza kazi ambayo anawaza kuwa ni cha kiwango cha chini. Anafaa avumilie akifanya kazi hizo kama vile zaraa, ukwenzi, na uvuvi baharini kwani kazi zenyewe ni bora na watu wafaa kufahamu hivyo wasizipuuze. Shairi hili limekuza maudhui ya umuhimu wa kufanya kazi kwa kuwa binadamu anapotenda kazi hujipatia riziki na ambayo itampa uwezo wa kujikimu.

Shairi hili linaonekana kuwa na mwingiliano na hadithi ya “Mke Wangu” (uk. 1-9) katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Hadithi hii ya “Mke Wangu” iliandikwa na Muhammad Said Abdalla ambaye ni mzaliwa kisiwani Zanzibar. Mtunzi huyu ameandika hadithi ya “Mke Wangu” ambayo kama S.A. Mohamed imeangazia maudhui ya kazi. Ametumia mhusika wake Aziza ambaye ni mke wa Msimulizi. Msimulizi alibahatika kupata kisomo na kwamba alikulia mjini huku Aziza hakupata kisomo chochote naye alikulia shamba. Msimulizi akawa anabagua kazi na kudharau kazi nyingi za pale nyumbani na kuthamini kazi za kiofisi.

Hili lilisababisha ugomvi katika familia yao. Msimulizi hakutaka kazi kama vile kuchoma na kuuza mihogo, kukwea minazi, kuangua na kuuza na kuchunga punda. Akiulizwa mbona hafanyi kazi, anasema yeye hajapata bado. Aziza alimweleza kwamba kazi ni njia mmojawapo wa kupata riziki. Msimulizi hakutaka kazi kama vile kukwea minazi na hivyo akamhadaa mkewe kwamba hakuwa amepata kazi japo amekuwa akijibidiisha kutafuta. Aziza mkewe akamwuuliza sababu ya kukosa kazi. Msimulizi alijibu kuwa yeye hakutaka kazi kama ya kuchoma mihogo ili auze kwani angeonekana mwehu kwa kufanya kazi hizo. Alisema kwamba kazi hizo sio za watu wa hadhi kama yake. Msimulizi anaonekana kabisa kubagua kazi na kuhisi kazi hizo ni za viwango vya chini.

Jambo hili la kubagua kazi lilifanya ndoa yao isambaratike kiasi kwamba Aziza aliomba apewe talaka. Aziza alimpenda muuza madafu kwa kuwa alikuwa akifanya kazi na kupata pesa zake mwenyewe sio kama msimulizi aliyekosa kufanya kazi na kubakia kuwaomba wazazi wake pesa ilhali ni mtu mzima ambaye ameo. Aziza anasema kuwa kazi ndiyo kitu ambacho mwanadamu ameumbiwa kufanya hapa duniani; ndiyo ibada ya binadamu. Aziza alimlinganisha mumewe; msimulizi na muuza madafu, akisema kwamba yeye ni binadamu kamili kwa sababu anapenda kufanya kazi ili kujipatia riziki. Alisema muuza madafu ni mkulima tena anafanya kazi, kwamba hela anazozipata ni za halali kwa sababu katolea jasho. Hafikirii kukaa bure na kutegemea pesa za wazazi wake kama alivyofanya msimulizi. Aziza anaelezea kuwa kazi ndiyo ubinadamu. Duniani kazi ni ibada ya binadamu. Aziza anasema alimpenda muuza madafu sana kiasi kwamba aliona kuwa atakuwa mume wake na hivyo tendo hili lilimfanya aombe msimulizi ampe talaka.

Shairi hili “Mtu Hachagui Kazi” (uk. 23) na hadithi ya “Mke Wangu” (uk. 1-9) inaendeleza maudhui ya kazi. Shairi hili na hadithi hii inaonyesha umuhimu wa kazi katika jamii. Imeeleza kuwa kazi ni ibada ya binadamu hujipatia riziki yao kila siku. Kupitia haya mwandishi ameonyesha madhara ya kutofanya kazi katika familia hususan mume au mmoja wa wanandoa. Jambo hili linaweza kusababisha ndoa isambaratike.

Shairi la “Mtu Hachagui Kazi” (uk. 23) katika diwani hii ya *Sikate Tamaa* na hadithi ya “Mke Wangu” (uk. 1-9) kwenye diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, zina uhusiano wa karibu sana. Waandishi wa kazi hizi wameangazia maudhui ya kazi huku wakilenga umuhimu wa kazi katika jamii. Wamesisitiza kuwa binadamu yeyote hafai kubagua kazi yoyote kwa kuwa kupitia

kufanya kazi mtu hupata riziki yake ya kila siku. Wanajamii wanastahili kupenda, kuzienzi kazi wanazojaliwa kupata kwa kufanya, kwa bidii na kwa moyo wa dhati.

Kazi hizi mbili zinaoana kwa kuwa zinahusiana sana. Hii ni kwa sababu waandishi wa kazi hizi walikulia sehemu mmoja. Kuna uwezekano mkubwa kwamba waliathiriwa na sehemu hiyo. Hii ni kwa sababu fasihi ni kioo cha jamii na kila mwandishi huandika kile kinachoonekana katika jamii yake. Mwandishi wa shairi la “Mtu Hachagui Kazi” S.A Mohamed na wa “Mke Wangu” Muhammed Said Abdulla wamezaliwa na kukulia visiwani Zanzibar, hivyo kazi zao zinaingiliana. Waandishi hawa wamenuia kusema kwamba kazi ni muhimu maishani. Wanawashauri wanajamii kufanya kazi bila ubaguzi na kwa bidii.

3.7.2 Ndoto

Shairi la “Ndoto” (uk. 26) lina mwingiliano na riwaya ya *Utengano* (1980:96) ambapo Maimuna aliota ndoto kuhusu mnyama mkubwa amezaye watu. Shairi “Ndoto” linaangazia ndoto ambayo mtu aliota huku akiona mahali ambapo palitawaliwa na vita vikali. Aliona mnyama mmoja ambaye alikuwa na pupa na huleta shida. Ubeti wa tatu unaeleza mnyama huyo humeza bila kubakisha, huumiza, humaliza kabisa hata hufisha. Shairi hili linakuza maudhui yay a ukatili. Hii ni kwa kuwa mnyama anayerejelewa humeza bila kubakisha na mwishowe husababisha kifo. Ndoto hii inastajabisha, inaonyesha hali ya tanzia iliyokuwa kule Tanzania wakati huo. Shairi hili limekuza maudhui ya ukatili pale ambapo mwandishi amesawiri mnyama katili awezaye kumeza bila kusaza. Hii inamaanisha kwamba mnyama huyu hudhulumu sana, kwani anawatesa watu kwa kumwaga damu.

Katika *Utengano* (1980:96) mnyama ambaye ametajwa ni mkubwa sana halafu pia humeza bila kusaza, alimmeza Maimuna. Mnyama huyo alionekana anafanana na nduma kuwili, halina miguu wala mikono mwishowe akaonekana ni mwanadamu. Mnyama alionekana ana sura ya binadamu ambaye hatimaye alionekana kuwa yule mnyama alikuwa babake Maimuna yaani mzee Makuudi. Makuudi alimtesa sana bintiye Maimuna kwa ile hali ya kumtawisha nyumbani bila kupata uhuru wowote. Hili lilisababisha Maimuna kupotoka kimaadili punde tu alipopata nafasi ya uhuru wa kutoka nyumbani.

Said A Mohamed aliangazia maudhui ya dhuluma na ukatili kwa kulenga mnyama huyu anayemeza. Yeye alionyesha kwamba katika jamii kuna watu wakatili kama ilivyo katika shairi la “Ndoto”. Maandishi haya katika *Utengano* yamechangia maudhui ya dhuluma na ukatili yaliyoendelezwa na Maksiudi babake Maimuna. Shairi la “Ndoto” lina uhusiano na maneno haya katika *Utengano* (uk. 96) yaliyoandikwa na S.A Mohamed. Kazi hizi mbili zinaingiliana na kuhusiana kwa sababu kazi zizi hizi mbili zilitungwa na mtunzi mmoja yaani S.A. Mohamed, hivyo basi kuna uwezakano kuwa mwandishi alikuwa anasisitiza na kukashifu vitendo vya watu walio na nguvu kwa kutumia nafasi zao vibaya kudhulumu wengine wasio na nguvu.

3.8 Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia usemezano katika mashairi teule ya diwani hii. Tumeshughulikia vipengele vifuatavyo: majibizano, ambapo tumeonyesha wahusika wawili wanaojibizana kwa mfano mwana na mama katika shairi la “Imani ya Mwana”. Tumeonyesha vile vile dhana ya shani kwa mujibu wa Bakhtin, sajili mbalimbali, usemi kuwa jibu kwa usemi na masimulizi ya moja kwa moja ya kifasihi, uhusiano na matini nyingine ambapo tumbainisha kwamba mashairi haya yameonyesha uhusiano na matini nyingine kama vile *Utengano* na *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Pia tumeonyesha kipengele cha lugha aliyoitumia mwandishi pale ambapo tumbainisha kwamba ametumia lugha yenye matumaini. Tumeonyesha namna ambavyo vipengele hivi vinakuza dhamira na maudhui ya mwandishi. Tumechunguza na kubainisha kuwa vipengele hivi vya usemezano vimerahisisha uelewa wa mashairi haya ya *Sikate Tamaa* kwa kuyaweka wazi maudhui ya mtunzi.

Katika sura inayofuata tutashughulikia namna ambavyo muktadha wa mazungumzo huathiri mawasiliano kati ya wahusika wanaozungumza katika mashairi ya *Sikate Tamaa*.

SURA YA NNE

ATHARI ZA MUKTADHA KATIKA MAZUNGUMZO

4.0 Utangulizi

Katika sura hii tunashughulikia namna ambavyo muktadha unavyoathiri mazungumzo baina ya wahusika wanaowasiliana katika mashairi ya diwani ya *Sikate Tamaa*. Muktadha kwa mujibu wa Mbatiah (2001) ni mazingira au hali ambamo tendo, tukio au jambo fulani hutendeka. Katika *Sikate Tamaa*, muktadha umeathiri namna ambavyo wahusika wanavyowasiliana kwa kiasi kikubwa. Kuna miktadha mbalimbali kama vile miktadha rasmi na isiyo rasmi. Katika muktadha rasmi, tumeonyesha muktadha wa kiuongozi na katika muktadha usio rasmi tumeshughulikia muktadha wa kijamii ambapo tumejikita katika muktadha wa kifamilia kitabaka, kimaskini pamoja na muktadha wa kutoleana wasia.

4.1 Muktadha wa Kijamii

Katika muktadha wa kijamii, hali au mazingira mbalimbali huathiri mazungumzo miongoni mwa wanajamii wanapotagusana au kubadilishana usemi. Hali au mazingira haya ni pamoja na zile za kifamilia, kitabaka, kimaskini na katika utoaji wa wasia.

4.1.1 Muktadha wa Kifamilia

Hii ni hali ambayo watu wanaathiriwa kwa sababu ya uhusiano kati yao na jamaa zao au watu walio katika ukoo mmoja. Kwa mfano uhusiano baina ya wazazi na watoto au mume na mke. Katika shairi la “Imani ya Mwana” (uk. 30-32), tumeangazia uhusiano wa baba na mama pamoja na uhusiano uliopo baina ya mama na mwanawe. Katika shairi hili maisha katika familia yameathiri namna ambavyo wahusika wanawasiliana. Wahusika hawa ni mwana na mama. Mwana analalamikia namna ambavyo baba anavyoishi, yaani hawajibikii familia yake. Katika ubeti wa kwanza mwana anamuuliza mama swali “kwani mamangu u ng’ombe, au u punda wa dobi?” Angetaka kujua sababu ya mama kufanya kazi za sulubu pekee yake bila babake ilhali wote ni wazazi. Kwake mwana, wazazi wote wanastahili kuwajibikia familia yao kwa kutekeleza majukumu yao kwa pamoja. Mazingira haya ya kifamilia yanaathiri mazungumzo kati ya mwana na mama. Mwana anauliza mbona mama anafanya kazi nyingi sana na kwamba anateswa na

kuonewa. Anahisi uchungu eti mamake anafanya kazi kipunda. Hili linamchochea kutaka kufahamu kama kweli binadamu ameumbwa kupigwa na kudhulumiwa maishani. Anasema analia sana ndani yake kwa kumwona mamake akiumia. Namna ambavyo mwana anaeleza mambo, ni ithibati tosha kuwa ameathirika na jinsi mambo yanavyoendelezwa katika familia yao na hata mama vile vile. Haya yanadhihirika katika ubeti wa kwanza. Shairi hili linatuonyesha maudhui ya taasubi za kiume na kutowajibika. Mwana anauliza kama fadhila au wema wa kufanya kazi hizi zote ni kuchapwa na kuteswa. Kwa kuchunguza zaidi inaonekana kuwa mwana haishiwi na maswali kuhusu familia yake ishara ya kwamba ameathiriwa na namna familia yao ilivyo.

Mama katika ubeti wa pili, anamjibu mwanawe kwa kumweleza kuwa azungumze kwa sauti ya chini kwa kuwa hangetaka baba asikie anachokisema. Hili litaleta migogoro ambayo huenda babake akazua. Anamweleza mwana wake kwamba hangetaka aje apigwe na hata kuuliwa kwa kuuliza maswali anayoyauliza. Hii ni kwa sababu baba ni mkali sana na pigo lake haliwezi likalinganishwa na chochote na kuwa hakutaka mgogoro maishani.

Katika ubeti wa nne (uk 30), mwana anamuuliza mama sababu ya kwenda shambani akiwa peke yake na sababu ya kulima shamba hadi machweo huku jembe likilia kwa kuangukia kwenye kwekwe. Angetaka kujua kwa nini katika shughuli hizo za uandalizi wa konde hamuoni babake. Analalamikia kutowajibika kwa babake katika familia yao huku akimwonea mamake huruma. Hili linamfanya kuuliza kama binadamu aliumbiwa mateso.

Katika ubeti wa tano (30) mwana anaonekana kujawa na huzuni anapoona mamake akishughulikia kila kitu pale nyumbani huku babake anapiga gumzo mitaani. Anakereka pia wakati anamwona mama akiteseka huku baba hamjali wala hata kumthamini. Ana imani na mamake na kumpenda ndiposa anamhurumia. Hili linamchochea mwana kuuliza mamake kama hatima ya mtu ni dhuluma na mateso. Shairi hili limekuza maudhui ya nafasi ya mwanamke katika jamii. Hii ni kwa kuwa mama ameonekana kujukumika katika jamii yake.

Katika ubeti wa sita na saba (uk. 31), mwana anataja kazi zote ambazo mamake hufanya. Mama anakata kuni mwituni kwa shoka, afunge mzigo huo ili abebe kuja nao nyumbani, kuandaa chakula kwa wakati unaofaa kwa kuwa kikichelewa baba anamchapa mama. Mahitaji yote ya pale nyumbani mama anafanya hima kuyapata peke yake bila msaada wa baba. Mama afanya usafi

nyumbani, nguo azisafishe na kuwalea watoto. Vyakula vyote vilivyomo nyumbani, mama ndiye amevitafuta akiwa peke yake bila kuungwa mkono na baba. Vyakula hivyo vikiisha mama ndiye anajukumika kutafuta vingine. Anatafuta hata kama ni kwa kuomba. Anaandaa chakula mekoni kwa minajili ya familia yake. Wakati ambapo chakula kitakosekana baba atazua zogo ilhali yeye hawajibikii familia yake. Mama vile vile ananadhifisha nyumba, kuwalea watoto na kuwaosha ili wawe safi. Anamwandalia baba chakula na kumtilia mezani kisha anamnawisha. Shairi hili katika kulenga beti hizi, maudhui yaliyokuzwa na kuendelezwa ni ya kutowajibika na mapuuza. Baba anaonekana kuendeleza maudhui haya kwa kuwa hajihusishi na masuala ya familia yake, kwani amepuuza majukumu yake ya kuwa baba na mume. Baba hachangii katika maendeleo ya familia kama vile kutoa chakula na malezi mema bali yeye huleta ugomvi kila mara na kumdhulumu mama.

Katika ubeti wa tisa Mama anatekeleza majukumu yake vyema kwake baba kwa sababu anampenda sana. Mwana anaeleza kwamba mama anamkanda baba maungo, anamsinga kwa madawa ili maungo yake sawa lakini baba bila kuona hayo anamdhulumu mama sana na kumwacha kuwa mtumwa. Hili linamchochea mwana kusema kwamba anatamani sana amlinde mama ili asipate taabu zaidi. Hii ni kwa kuwa mwana anamuenzi mamake hakika.

Kwenye ubeti wa kumi maudhui ya ukombozi yanaendelezwa. Mwana anamzindua mamake kujikomboa kutokana na mateso ya baba. Anamweleza kutambua kwamba haki zao wote ni sawa. Alimwambia hastahili kusumbuka siku zote katika ndoa kwa kuwa daima atabaki nyuma jambo ambalo linakera mno. Uhusiano uliopo katika ubeti huu ni wa mwana na mama ambapo mwana anamhurumia mamaye kwa sababu ya dhuluma za baba. Mukadha wa kifamilia umeathiri mazungumzo ya mwana kwa mamaye. Ubeti huu umeendeleza maudhui ya ukombozi.

Mama anamjibu mwanaye katika ubeti wa kumi na moja (uk. 32). Anamwambia kwamba ameumia miaka mingi lakini hakuyapenda maisha yale kwa kuwa yalikuwa ya shida. Alikuwa anakerwa na baba na tayari amefika kikomo hivyo anaanza kujikomboa kutokana na mateso yale. Katika ubeti huu maudhui ya ukombozi yamekuzwa na mama anapoamua kujitoa kutoka matesoni. Shairi hili limedokeza kuwa uhusiano baina ya mwana na mama umeathiriwa na mazingira waliyomo na kwamba haya yameonekana katika mazungumzo yao.

4.1.2 Muktradha wa Kitabaka

Utabaka ni hali ambayo watu huishi kulingana na hadhi yao maishani, hususan mwanya ulioko baina ya mabwanyenye na makabwela katika jamii. Matabaka yanajitokeza katika diwani hii. Tumeangazia matabaka katika mashairi mawili; “Mwanakupata” (uk. 36) na “Nilipokwenda dukani” (uk. 24).

4.1.2.1 Mwanakupata.

Katika shairi la “Mwanakupata” (uk. 36) muktadha ya kitabaka yanajitokeza. Mazingira haya yameathiri majadiliano baina ya hawa wahusika wanaobadilishana usemi yaani Mwanakupata na Mwihaja. Mwanakupata ni wa tabaka la juu kwa kuwa yuko enzini huku Mwihaja ni wa tabaka la chini. Hawa walikuwa rafiki hapo zamani walipokuwa wadogo. Hii ndiyo sababu ya hawa wahusika kukutana. Mwihaja alikuwa na shida hivyo akaenda kwa Mwanakupata ili aweze kumsaidia kwa kiasi fulani. Mwanakupata kwa sababu alikuwa amepanda cheo na tayari maisha yake yalikuwa yamekuwa bora na kuwa tajiri au bwanyenye alimpuuza rafikiye wa zamani Mwihaja. Mwanakupata kwa sababu yuko katika enzi anamfokea na kumwamuru Mwihaja atoke nje mara moja kwa kuwa alikuwa maskini. Mwanakupata anasema kwamba maskini hawaachi kuomba ndipo kwa haraka akamtema Mwihaja nje ya nyumba yake. Namna ambavyo Mwihaja anavyojieleza, anaonekana kuwa ameathirika na mazingira yake ya tabaka la chini. Mwanakupata anathibitisha kwamba tabaka lake la mabwayenye limeathiri mazungumzo yake kwa Mwihaja. Maudhui ya utabaka na ukosefu wa utu yanaonekana katika shairi hili kwa kuwa Mwanakupata ambaye ni tajiri hamsikilizi Mwihaja alipoomba msaada.

Katika ubeti wa kwanza (uk. 36), Mwihaja anaonekana yuko katika mazingira ya kutaka kusaidiwa kutoka katika shida. Anataka kusitiriwa na rafikiye wa zamani Mwanakupata kwa kumnyoshea mkono. Katika upande mwingine kwenye ubeti wa pili, tunaona mazingira ya utabaka kutokana na majibu ya Mwanakupata. Maneno yake yanaonesha ukuu na hadhi yake. Ameuliza Mwihaja yule aliyemleta na alikotoka. Vile vile amwambia kuwa maskini hawaachi kuomba. Alifanya hivi kwa kuwa ana uwezo mkubwa na kwamba yuko enzini. Mazingira ya kuamrisha yanaonekana anapoamua kuamrisha Mwihaja kuondoka ofisini mwake. Maneno yake Mwanakupata yameathiriwa na tabaka lake. Maudhui ya matabaka yamekuzwa katika ubeti huu ambapo tunaona Mwanakupata akiwa enzini na Mwihaja ambaye ni kabwela aliyeomba kusaidiwa.

Majina ya wahusika hawa, Mwanakupata na Mwihaja ni ya kimajazi kwa kuwa yanaona na hali zao za kimaisha. Mwanakupata ni mtu ambaye tayari amekwishapata kitu na kwa muktadha huu, amekwishapata mali hivyo yuko starehe sio kama pale zamani alipokuwa mdogo. Hili limebadili maisha yake na kumweka katika kiwango cha walio nacho. Mwihaja ni mtu ambaye ana haja sana ya kupata kitu na kwa muktadha huu ana shida na haja ya kupata msaada kutoka kwa Mwanakupata na ndiposa ameenda kumtembelea kwake. Umaskini umemwandama sana hivyo anaomba msaada.

Mwihaja anamkumbusha Mwanakupata kwamba wao walikuwa rafiki zamani walipokuwa bado katika umri mdogo. Hivyo basi hili limemchochea aende kwake ili amfae wakati wa dhiki. Anamweleza kwamba ufukara ndio umemleta kwani hakuwa na mbele wala nyuma.

Katika ubeti wa nne (uk. 36), Mwanakupata anamkana kwa kusema kwamba yeye alipata kile alichio nacho kwa kutoa jasho hivyo hataki asumbuliwe. Anasema kuwa ni wakati wake wa kujitapa akiwa enzini. Anamwamuru Mwihaja aondoke mbele yake.

Mwihaja alifedheheka na kurejea nyumbani akiwa amekereka kwa yale aliyofanyiwa na Mwanakupata. Alijuta sana mbona alielekea kwa tajiri huyo, 'nduguye' wa zamani ambaye kumbe hamthamini tena kwa sababu ya ufukara wake, hana utu na aliyemdharau hata kumtoa nje ya nyumba yake. Mwihaja alihisi kuvunjika moyo. Muktadha ya matabaka yanaonekana kwa kule Mwanakupata anajitapa na yuko katika enzi.

Shairi hili linachora maudhui ya utabaka na usaliti. Mwanakupata anamkana Mwihaja ambaye ni rafiki yake wa zamani na anakosa kumhurumia ila kumtimua nje. Haya yanapatikana katika ubeti wa nane (uk. 37).

4.1.2.2 Nilipokwenda Dukani

Katika shairi hili mazingira ya matabaka yanadhihirika. Katika ubeti wa kwanza na wa pili (uk. 24), maelezo ya msimulizi yanaonyesha kuwa kuna matabaka. Msimulizi alienda dukani kununua kitu kimoja ambacho ni saruni lakini muuza duka baniani alimpuuza. Alipoingia mteja wa pili aliyekuwa mzungu baniani alimhudumia kwa upesi huku akimwacha mteja wake wa kwanza aliyetaka saruni.

Baniani alimhudumia mteja mzungu kwa haraka kwa kuwa alikuwa ana uwezo mkubwa kihela na hata angeweza kununua vitu zaidi ya kimoja huku akimwacha mteja wa kwanza aliyetaka saruni pekee kwa kuwa yeye alikuwa maskini. Maudhui ya matabaka na ubaguzi wa rangi yanaendelezwa katika shairi hili. Hii ni kwa kuwa baniani alimwacha mteja wa kwanza kwa sababu yeye ni maskini hivyo ni wa tabaka la chini na kumtazama mzungu ambaye alionekana tajiri.

4.1.2.3 Chui wa Kufuga

Katika shairi hili matabaka yamedhihirika. Kuna watu waliopewa mamlaka na wakatumia mamlaka yale kujinufaisha wenyewe na kuwaaacha watawaliwa wakiangamia. Katika ubeti wa kwanza (uk. 29), msimulizi wa shairi hili amesema kuwa alipotazama nyuma, aliona maajabu kwamba watu waliokuwa wamesimama walikuwa kizani. Alishangaa kuona watu hao wakionekana kama chui ambao wana uwezo wa kuumiza, kuharibu na kujeruhi. Katika ubeti wa pili machui hao wamebainika kuwa ni viongozi walio na waliopewa uwezo wa kuongoza. Viongozi hao ni watu wa tabaka la juu yaani walala hai hivyo wana uwezo wa kuudhalilisha umma kwa kuwa wako enzini.

Watawaliwa ni wachochole kwa kuwa hawana uwezo sana wa kujimudu na kwamba matumaini yao kutoafikiwa na viongozi wao. Hii ni kwa sababu viongozi wamekuwa kama chatu anayemeza jambo ambalo limewafanya kukiri kuwa ni hatari kuwapa watu kama hao mamlaka. Matabaka haya yamekuza maudhui ya ukatili. Hii ni kwa kuwa walio na uwezo wanafanyia unyama umma usiyo na mamlaka.

4.1.3 Mukstadha ya Kimaskini

Mukstadha wa kimaskini ni hali ambayo watu au wanajamii wamo pale ambapo hususan mahitaji yao hayatoshelezi. Mukstadha huu umejidhihirisha katika mashairi haya; “Nilipokwenda Dukani” (uk. 24) na “Mwanakupata” (uk. 36).

4.1.3.1 Nilipokwenda Dukani

Katika shairi “Nilipokwenda Dukani” (uk. 24) mhusika msimulizi, ameathirika na mazingira yake. Anazungumza kama mtu aliyevunjwa moyo. Anasema katika ubeti wa kwanza (uk. 24) alipokwenda dukani alimkuta baniani ambaye ndiye muuza duka. Alipoagiza apewe saruni ambacho ndicho kitu kilichompeleka pale dukani, baniani alimpuuzwa kwa sababu yeye ni maskini. Alipoingia mteja mwingine ambaye ni mzungu, baniani alimhudumia kwa upesi na kumwacha

mteja wa kwanza msimulizi. Hii ni kwa sababu mzungu ana hela nyingi na anaweza kununua bidhaa nyingi kuliko msimulizi ambaye alipanga kununua kitu kimoja tu; saruni. Hili shairi linaonyesha maudhui ya ubaguzi wa rangi na utabaka kwa kuwa baniani anambagua msimulizi kwa sababu ya umaskini na kumuenzi mteja Mzungu kwa sababu ya hadhi.

Msimulizi katika ubeti wa pili, anasimulia kwamba alitaka kununua saruni na pesa alizokuwa nazo kulingana na uwezo aliokuwa nao. Wakati mteja mzungu alipoingia dukani na kuingiza mkono wake mfukoni, baniani akaruka, akamwacha mteja wa kwanza ambaye ndiye msimulizi na kumhudumia yule mteja mzungu kwa kuwa anaweza kununua vitu vingi kuliko msimulizi na kwa bei ya juu. Kwani msimulizi anasema alivumilia tu kwani hakuona uchungu. Namna ambavyo msimulizi anavyojieleza, inaonekana wazi kuwa ameathiriwa na hali yake ya kimaskini.

4.1.3.2 Mwanakupata.

Katika shairi la Mwanakupata muktadha wa kimaskini umeweza kuathiri mazungumzo baina ya wahusika wanaowasiliana. Mwishaja ambaye ni kabwela anahitaji msaada, hivyo anaenda kwa Mwanakupata ambaye ni mbwanyenye. Mazingira yake ya kimaskini yameathiri namna ambavyo anazungumza na kujieleza kwa Mwanakupata.

Mwishaja anamwambia Mwanakupata kwamba yuko mashakani kwani ameteseka. Anamwomba amwokoe upesi ili asiabike kutokana na hali yake ya ufukara. Anataka kufichwa dhidi ya aibu yake na hivyo anataka msaada kabisa.

Mwishaja anamwambia Mwanakupata katika ubeti wa tatu (uk. 36) kuwa akumbuke kwamba walikuwa rafiki zamani enzi za utotoni na kwamba walipokuwa wadogo waliishi pamoja vyema. Anamwambia kuwa amejinyima kabisa lakini amelazimishwa na umaskini jambo ambalo limemsukuma kumtembelea. Muktadha wa umaskini umeathiri mazungumzo yake.

4.1.4 Muktradha wa kutoleana wasia (Mawaidha)

Muktradha huu ni ule ambao mwandishi au mhusika katika kazi ya fasihi anatoa mashauri kwa mtu au kwa kikundi fulani cha watu katika jamii. Mawaidha hayo ni kwa minajili ya kuelekeza au kutoa mwongozo wa namna ya kutekeleza jambo fulani. Mashairi yanayodhihirisha muktradha huu ni; “Imani ya Mwana” (uk. 30-32), “Muhali” (uk. 48) na “Nawaita Washairi” (uk. 3)

4.1.4.1 Imani ya Mwana

Katika shairi hili la ‘Imani ya Mwana’, mwana anampenda sana mamake ndipo anamhurumia anapoteswa na baba. Hili linasababisha mwana kumpa mamake mawaidha. Sio jambo la kawaida mwana kumshauri mzazi lakini mwana katika shairi hili kwa sababu ya mapenzi yake kwa mama na huruma, anahisi kumtetea kutokana na maonevu ya baba na ndipo anamshauri. Mwana ameathiriwa na hali ya mama hivyo basi hili linaathiri mazungumzo yake ya kimawaidha kwa mamake mzazi. Mwana anamwona mama akifanya kazi zote za pale nyumbani kuanzia asubuhi hadi jioni huku baba akizurura kila mara mitaani kupiga gumzo huku akiwa na taasubi ya kiume. Baba ni mkali kupindukia. Anampiga mama na kila wakati ni kelele.

Mama anateseka kwa vile pia jamii haimsaidii kutoka katika madhila. Hili ni kwa sababu utamadani unamsaidia baba kumdhulumu mama kwa kuwa hata baba akikaa bila kufanya chochote hakuna atakayemwuliza chochote. Naye mama kitamaduni anastahili kufanya kazi zote za nyumbani na kuhakikisha kuwa familia yake iko sawa.

Mwana katika ubeti wa kumi (uk. 32) anajaribu kumzindua mama kuwa lazima aamke na kutetea haki zake kwa kuwa ameteseka kwa muda mrefu sana. Mwana anamshauri mama kuwa ni wakati wake mwafaka wa kujikomboa na kujing’oa kutoka utumwani. Shairi hili linatuonyesha maudhui ya ubabedume na mapuuza. Hali kadhalika kuna maudhui ya ukombozi na utu.

Mama kwa hakika baada ya kushauriwa na mwana aligundua kwamba yale aliyoambiwa yamekuwa ya kweli. Amekubali na kuamua kujikomboa kutokana na mateso ya baba ya miaka mingi katika ndoa yake na nguvu za utamaduni. Alikiri kuwa amekerwa na dhuluma za baba na kwamba ameamua yote yafike kikomo. Haya yameonekana katika ubeti wa kumi na moja wa shairi hili ambalo ni tamati la shairi hili. Maudhui yanayojitokeza katika shairi hili ni ukombozi pale ambapo mama amejitambua na kujitoa katika dhuluma za ndoa na minyororo ya utamaduni.

4.1.4.2 Muhali

Muhali ni hali ambayo huleta ugomvi baina ya watu. Ni jambo ambalo linaudhi au kukera. Shairi hili limetoa mashauri kwa wanajamii kwamba wanastahili waache mambo ambayo mara nyingi yanaleta mvutano baina yao na watu wengine kwa sababu mwishowe hutawaletea balaa. Pia haifai.

Katika ubeti wa kwanza na pili (uk. 48), shairi hili linadokeza kwamba mtu akiwa na tabia ya kukera watu, mambo mengi mara kwa mara yatamharibikia na kumsababishia aibu tele. Hii ni kwa kuwa kero hugonganisha watu kwa kuwa huchafua moyo kwa haraka sana. Mtu hawezi kufikiria vyema wakati ameudhika ndipo mshairi anashauri jamii kwamba waache muhali kabisa. Mtu yeyote anapoambiwa neno au jambo linalouudhi anaonekana mtu mzuri anatabasamu lakini uso wake unaonyesha aibu na chochote kibaya yeye anachukulia kuwa ni kweli hata likiwa ni kitu kibaya huliamini kwa wepesi. Maudhui yanayoonekana katika shairi hili ni madhara ya mambo yaletayo ugomvi katika jamii.

Maelezo yanayojitokeza katika ubeti wa saba na tisa ni kwamba hali ya kumchelea mtu husababisha mtu kupoteza mali yake na kujiingiza katika madeni. Anaweza kukosa hata kiwango kidogo cha mali yake ya kuweka kama akiba mfukoni. Mshairi anatoa mawaidha kwa jamii haswa kwa mtu yeyote yule asiukaribishe muhali kwa sababu anaweza kuona maajabu maishani.

4.1.2.3 Nawaita Washairi.

Katika shairi hili shairi “Nawaita Washairi” (uk. 3), mshairi anatoa wasia kwa wale wote walio na ujuzi wa kutunga shairi. Muktaadha aliomo ni ule wa kuelekeza. Maneno yake haswa ni ya kishauri. Katika ubeti wa kwanza, mshairi anawahimiza washairi wenzake wawe na umoja na ushirikiano katika uandishi wa ushairi. Anawashauri kuwa wasije wakawa wanabishana wenyewe kwa wenyewe bali wawe na ushirikiano mwema ili watunge mashairi kwa hamu. Maudhui yanayoendelezwa ni umoja na ushirikiano wazo ambalo litakuza utanzu wa shairi. Muktaadha huu wa kutoleana wasia umeathiri maneno ya msemaji hususan lugha ambayo ameitumia kwani ametumia lugha shaurifu na arifu.

Katika ubeti wa pili mshairi anashauri kwamba watunzi wawe wabunifu kwa kuvyaza mitindo tofauti tofauti ili kufanya ushairi uvutie zaidi. Wawe na upendo ili waweze kupaa katika utungaji na waandike kwa msisimko. Muktaadha huu umechenga na kuendeleza maudhui ya umoja na utangamano baina ya watunzi.

4.1.2.4 Mtu Hachagui Kazi

Katika shairi hili, mshairi anashauri kuwa, kazi zote ni muhimu mradi humfaidi yule ambaye anafanya. Hii ndiyo sababu ametoa wasia kwamba binadamu hastahili kubagua kazi bali anafaa afanye kazi yoyote ambayo amefanikiwa kupata bila kulalamika kwa kuwa kazi ni kama ibada kwa binadamu kwani wasipofanya kazi hawataweza kukiweka chakula mezani.

Ubeti wa kwanza (uk 23), mtunzi ameshauri kuwa kazi huwa ni kazi haijalishi namna ambavyo ilivyo mradi sio ulaghai. Amesema ushonaji pamoja na upagazi na kazi zingine nyingi mtu anastahili kufanya bila kubagua kwa kuwa ni jambo muhimu kuliko mambo mengine yote. Uteuzi wa maneno yake umeathiriwa na lengo lake la ushauri katika ubeti huu. Maudhui ambayo amesisitiza ni ya kufanya kazi. Ameonyesha haya katika mshororo wa nne ubeti wa kwanza.

“Kazi ni kitu azizi, wala vyenginevyo sivyo”

Katika ubeti wa pili, mshairi anadokeza kuwa binadamu yeyote hafai kudunisha kazi ambayo inaonekana kuwa ni ya kiwango cha chini bali mtu anafaa afanye kazi hiyo kwa uvumilivu na kujikaza. Mifano ni kama vile ukulima, uvuvi baharini. Anaelekeza kwamba kazi zote ni nzuri, hivyo watu wafanye kwa bidii bila ubaguzi. Mshororo wa nne ubeti wa pili unaonyesha haya.

“Hizi nazo njema kazi, yafaa uzibaini”

Ubeti huu unakuza maudhui ya umuhimu wa kufanya kazi bila kudunisha. Katika ubeti wa tatu na nne, shairi hili linaonyesha umuhimu wa kazi zote kwa kuwa kila kazi ina kiwango chake. Mshairi anashauri kuwa binadamu hafai kudharau kazi kwa kuwa hakuna kazi duni. Ni unyama kusema kazi yoyote ni duni kwani kazi zote zina viwango, hivyo binadamu anafaa afanye tena kwa umakini bila ubaguzi. Mshairi anasisitiza kuwa ni jukumu la binadamu kupenda kufanya kazi kwa moyo wake wote na kutenda kwa uadilifu, bidii na kwa umakini. Hii ni kwa sababu atafaulu kujitoka kwenye shida na kushinda uvivu maishani. Katika shairi hili tukilenga muktadha huu, mshairi ameendeleza maudhui ya umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii.

4.1.2.5 Sikate Tamaa

Katika shairi hili “Sikate Tamaa” (uk. 1), mshairi anatoa mawaidha kwa wanajamii kwamba wasiwe wepesi wa kukata tamaa kwa kuwa dunia inakajanga hivyo huhitaji uvumilivu. Katika ubeti wa kwanza mshairi anatoa mawaidha kwa kijana. Msemewa ni kijana. “sasa inuka, kijana

ianze kazi”. Anamshauri kwamba anastahili kujikakamua na kuamka kisha asimame kidete. Akichunika anafaa ainuke na kujikaza kwa kutibu pahala ambapo ameumia. Anamtia moyo kijana asimame na kuanza kufanya shughuli zake bila kufa moyo.

Muktadha huu umeathiri mazungumzo ya mshairi. Ameteua maneno yanayofungamana na muktadha huu. Mifano, “Inuka, simama kama mnazi” katika ubeti wa kwanza mshororo wa kwanza. Ubeti huu unaendeleza maudhui ya mapambano kuwa changamoto zipo lakini mtu anafaa apambane ili ashinde.

Katika ubeti wa pili na wa tatu, mshairi anatoa wasia zaidi. Anamweleza kijana kwamba asife moyo kwa kuwa ana uwezo wa kufanya mambo. Anamwambia kuwa watu wana hila na hivyo basi itampasa atie jitihada. Ulimwengu kuna matata lakini itambidi ajikaze asife moyo. Kijana anapewa tumaini kuna licha ya dunia kudhulumu akijikaza na kuwa na uvumilivu atashinda. Hali hii ya kutoa wasia imeathiri lugha ya mshairi. Ametumia lugha arifu, shaurifu na ya kimatumaini kutekeleza maudhui ya mapambano na utetezi wa haki. Anamzindua kijana ajikaze ili kutetea haki zake bila kupoteza tumaini. Ubeti wa tatu mshororo wa tatu huonyesha haya.

“Dunia baa, nyanyuka anza tena kujiunda”

4.2 Muktadha wa Kiuongozi

Mazingira ya kiuongozi yanaweza kuathiri mawasiliano. Hii ni kwa sababu viongozi wana mamlaka fulani kulingana na hadhi yao kazini. Viongozi wana uwezo kwa kuwa wako enzini. Mamlaka yale yanaathiri namna atavyozungumza na watu hususan wale walio chini ya uongozi wake. Muktadha huu hujumlisha uhusiano baina ya watawala na watawaliwa, muktadha wa kikoloni na kikoloni mamboleo. Watawala wanapozungumza na watawaliwa mazungumzo hubadilika sio kama watawala wanapowasiliana na watawala wenzao. Watawala mara nyingi wanatoa mwelekeo au mwongozo kwa watawaliwa au hutoa masharti hivyo kuna uhusiano wa mtawala na mtawaliwa.

4.2.1 Muktadha wa Kikoloni na Kikoloni Mamboleo

Ukoloni ni mfumo ambao nchi moja huweza kuitawala nchi nyingine. Kuna aina mbili za ukoloni; ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Ukoloni mkongwe ni mfumo wa utawala uliokuwa pale kitambo wa nchi moja kutawala nchi tofauti moja kwa moja. Ukoloni mamboleo ni mfumo au mtindo wa utawala wa nchi za kibepari kuwa na ushawishi sana wa kisiasa na kiuchumi katika nchi

zinazoendelea kwa manufaa au maslahi yao wao wenyewe. Wazungu waliwatawala waafrika kabla ya uhuru kwa kuwanyanyasa vibaya sana. Waafrika baada ya uhuru walijitawala wenyewe japo waliendeleza dhuluma za mkoloni mkongwe.

4.2.1.1 Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo

Katika shairi la “Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo” (uk. 20-21), muktadha huu wa ukoloni na ukoloni mamboleo upo. Muktadha huu unaonekana kuathiri mazungumzo baina ya wahusika hawa wawili; Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo. Ukoloni Mambo-Leo una hamu sana ya kuongoza hivyo unataka sana Ukoloni umpe nafasi ya kuongoza. Hali hii imeathiri mawasiliano kati yao. Ukoloni Mambo-Leo unatamani sana upewe uongozi ili uwatese watawaliwa. Unamwambia Ukoloni kwamba umpishe ili uweze kushika hatamu na kumwonyesha umahiri wake. Unadhamiria kuwaangamiza wananchi kwani unataka wote walie kwa sababu utawanyanyasa na kuwadhalilisha wakati akipewa mamlaka. Shairi hili linaonyesha maudhui ya ukoloni na ubinafsi kwani Ukoloni Mambo-Leo unajitakia makuu pekee bila kujali wananchi wanaoongozwa.

Ukoloni Mambo-Leo unamwelezea Ukoloni kwamba umetambua kuwa uliwafanya watawaliwa kuwa na furaha kwa kuondoka kwa wakoloni, lakini huo unakuja kwa nia moja ya kuwatesa na kuharibu furaha yao. Unasema kwamba utatumia mbinu ambazo watawala hawatatambua na tena watakuwa wamedanganyika wakidhani ukoloni umekwisha. Haya yanadhihirika katika ubeti wa nne na sita (uk.20).

Ukoloni basi unamjibu Ukoloni Mambo-Leo kuwa ikiwa wananchi watasema kwamba yeye Ukoloni aliwatendea mabaya basi hatakuwa na haja kwa kuwa watakuwa wakidaganya, hivyo hakuwa na budi kuwaaga, na kuondoka kwa kuwa wao ndio waliamua kupigania uhuru wao. Anapeana nafasi ya uongozi kwa mwenzake Ukoloni Mambo-Leo kwa sababu hataki kumnyima mamlaka yale. Lakini anajua wananchi watajuta baadaye kutawaliwa na mkoloni mamboleo ambaye atakuwa mbaya zaidi katika kuwahujumu. Hamu ya kutaka kuongoza imeathiri mazungumzo baina ya wahusika hawa. Ni ithibati tosha kwamba uongozi ni mtamu sana.

Muktadha huu wa kiuongozi umedhihirika kwa kuwa kuna misamiati ya sajili ya siasa kama vile ‘nakuacha utawale’ ubeti wa kwanza mshororo wa kwanza, ‘uhuru kung’ang’aniya’ ubeti wa tano

‘zimekwisha zamu zangu ni za kale’ mshororo wa kwanza. Muktadha huu umeendeleza maudhui ya kulipiza kisasi. Haya yanaendelezwa na Ukoloni kwa sababu ya malalamiko ya wananchi.

Wakoloni wametambua kuwa muda wao umekwisha na watawaliwa hawatawaruhusu tena wao kuwatawala. Ukoloni Mambo-Leo umetambua sasa kuwa wakoloni wameondoka hivyo unajitayarisha kuchukua nafasi yao ili kuendeleza ukoloni lakini kwa kutumia mbinu tofauti. Wakoloni wameona wazi kuwa hawahitajiki tena na wale waliowatawala na hawataki lawama zaidi. Kwa hivyo wanasalimu amri. Watawaliwa wamesema kwamba wakoloni walitenda maovu na kuwa wao wameyaona haya yote hivyo basi wameungana ili kutafuta ukombozi (uhuru wao). Ijapokuwa Ukoloni unaona kuwa kuna mazuri waliyoyatenda, watawaliwa wanayakumbuka yale mabaya kwa hivyo Ukoloni umeamua kuondoka na kutoa hatamu, kwa sababu hana haja ya kelele.

4.3 Hitimisho

Katika sura hii ya nne tumeangazia namna ambavyo muktadha unaweza kuathiri mazungumzo katika jamii. Tumefanikisha haya kwa kuchunguza muktadha rasmi na usio rasmi. Katika muktadha wa usio rasmi tumechunguza muktadha wa kijamii, kitabaka, kifamilia na muktadha wa kutoleana wasia. Katika muktadha rasmi tumetafiti muktadha wa kiuongozi ambapo tumechunguza tumelenga muktadha wa kikoloni na kikoloni mambo-leo. Tilitambua kwamba miktadha mbalimbali ya mazungumzo huathiri mawasiliano katika jamii. Sura ya tano inayofuata ni hatima ya utafiti wetu. Tumetoa hitimisho, matokeo ya uchunguzi, kutathmini madhumuni ya utafiti kama yameafikiwa na mapendekezo ya tafiti za baadaye.

SURA YA TANO

HITIMISHO, MATOKEO YA UTAFITI NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Katika sura hii ambayo pia ni hatima ya uchunguzi wetu, tumetoa muhtasari na matokeo kutokana na utafiti wetu. Tunadhamiria kubainisha iwapo madhumuni ya uchunguzi wetu yameafikiwa. Pia tumejibu maswali yetu ya utafiti na kutoa mapendekezo kwa tafiti za baadaye kuhusiana na mada hii ya utafiti.

5.1 Hitimisho

Katika tasnifu hii tumetafiti iwapo usemezano unapatikana katika ushairi wa Kiswahili. Tumetumia nadharia ya uhakiki wa usemezano ilioasisiwa na mhakiki wa Kirusi Mikhail Mikhailovich Bakhtin. Tumeangazia masuala ya kimsingi ambayo yanashughulikiwa katika kazi ya kifasihi inapotumia nadharia hii ya uhakiki. Tumeshughulikia yaliyoandikwa kuhusu nadharia hii na yaliyoandikwa kuhusu diwani ya *Sikate Tamaa*.

Katika sura ya pili tumeangazia vipengele vya usemezano katika ushairi wa Kiswahili kwa jumla. Tumeyaangazia hayo tukionyesha mifano mbalimbali kutoka mashairi kadha ya Kiswahili ili kuthibitisha kwamba usemezano upo katika ushairi wa Kiswahili, kinyume na madai ya Bakhtin (1981) kwamba usemezano upo katika riwaya pekee. Katika sura ya tatu tumechanganua mashairi katika diwani ya *Sikate Tamaa* kwa kuongozwa na vipengele vya usemezano. Tilitumia sampuli ya kusudi kuchagua mashairi kumi na manane. Tumefanya hivi kwa kulenga vipengele saba vya usemezano vinavyojidhihirisha katika diwani hii, na namna ambavyo vipengele hivi vinavyokuza dhamira na maudhui ya mwandishi. Kwenye sura yetu ya nne tumeshughulikia namna ambavyo muktadha wa mazungumzo unavyoathiri mawasiliano baina ya wahusika wanaowasiliana. Kutokana na uhakiki huu, mashairi ya Said A. Mohamed yamethibitisha utumizi wa vipengele kadha vya usemezano kama tulivyoona katika sura ya tatu.

5.2 Kuhusu Madhumuni Yetu

Utafiti huu ulilenga katika kuchunguza iwapo usemezano unabainika katika ushairi wa Kiswahili. Lengo lingine la utafiti huu limekuwa ni kutafiti namna usemezano huu umewasilishwa. Pia tulilenga kutathmini namna muktadha wa mazungumzo unavyoathiri mawasiliano baina ya wahusika wanaowasiliana katika mashairi ya *Sikate Tamaa*.

Ili kutekeleza malengo yetu tumetumia diwani ya *Sikate Tamaa* (1980) kuonyesha kuwa usemezano upo katika ushairi wa Kiswahili na umewasilishwa kwa namna gani. Kwa kutumia mashairi kumi na manane tasnifu yetu imefanikiwa kuonyesha kuwa usemezano kwa kweli unaweza kupatikana katika ushairi wa Kiswahili.

Imebainika kwamba katika ushairi wa Kiswahili kuna matumizi ya sajili mbalimbali. Mifano inaonekana katika shairi la “Nilipokwenda Dukani” (uk. 24), kuna sajili ya biashara au sajili ya madukani katika shairi la “Siku Njema” (uk. 5) kuna sajili ya matangazo ya redioni na sajili ya siasa katika shairi la “Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo” (uk. 20). Imedhihirika kuwa sajili hizi zinaingiliana na kutegemena katika kuendeleza maudhui katika mashairi haya.

Jambo lingine lidhihirikalo ni kuwa katika tungo tulizozichunguza kuna majibizano baina ya wahusika wawili. Haya yameonekana katika mashairi matatu “Ukoloni na Ukoloni Mambo-Leo” (uk. 20) “Imani ya Mwana” (uk. 30) na “Mwanakupata” (uk. 36).

Jambo lingine ambalo linaonekana katika utafiti huu ni kuwa mwandishi wa diwani hii ametumia masimulizi ya kifasihi ya moja kwa moja ili kuendeleza maudhui yake. Imedhihirika kwamba masimulizi ya kifasihi ambayo yametumiwa zaidi ni methali. Mtunzi ametumia methali uungwana sambe, ni jadi kubeli (uk. 45) katika shairi “Ungwana” (uk. 45), si kupanda ngazi, usijali kushuka (uk. 45), hujipalia makaa kwenye shairi la ‘Muhali’ (uk. 48), ni firauni wa kweli, utayaona mageni katika shairi lili hili ‘Muhali’ (uk. 48) na damu haiwi maji katika shairi ‘Huba kwa Wazee Wangu’ (uk. 47). Aidha miundo ya methali hizi ni tofauti na ilivyo katika hali ya kawaida.

Sifa nyingine ambayo imejitokeza katika uchunguzi huu ni kwamba katika mashairi ambayo tumechunguza wahusika wamepewa lugha teule. Wamepewa lugha ya matumaini katika shairi la “Sikate Tamaa” (uk. 4), mtunzi ametumia lugha shaurifu na zinduzi mfano “Umechanika, inuka,

tia dawa kwa ujuzi” katika kuzingatia mashairi tuliyoyateua, tumedhihirisha kuwa kinyume na madai ya Bakhtin (1981) kwamba hakuna usemezano katika ushairi, ni kweli kuwa usemezano upo katika ushairi.

Lingine lililobainika katika utafiti huu ni dhana ya shani kwa mujibu wa Bakhtin. Shani ni jambo linalostaajabisha katika jamii na kuwa si kawaida yake kutokea. Ni kushiriki katika mambo yanayonekana kukera au kuudhi kama vile viongozi kunyanyasa umma. Imebainika kwamba mtunzi wa diwani hii ametumia shani kama kifaa kitumikishi cha Sanaa ambacho kinaonyesha ukinzani wa utesi dhidi ya uongozi katika jamii. Mashairi yanayodhihirisha hali hiyo ya kero katika diwani ni kama vile; “Watu Hawajali” (uk. 18), “Watoto wa Afrika” (uk. 2), “Si Dunia ya Kulala” (uk. 3), “Wananambia Mchafu” (uk. 7), “Ajabu” (uk. 7) na “Chui wa Kufuga” (uk. 29) katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Hii ni kwa sababu shairi hili linakuza maudhui ya kazi na umuhimu wake. Isitoshe namna ambavyo shairi hili limeeleza dhana kazi inafanana na maelezo yaliyo katika “Mke Wangu”. Vile vile shairi la “Ndoto” (uk. 26) limehusiana na *Utengano* (1980:96).

Wazo lingine lililojitokeza katika utafiti kuwa, usemi ni jibu la usemi. Bakhtin (198:127) anasema hakuna mtu anayeweza kudai kuwa yeye ndiye wa kwanza kutoa tamko. Hii ni sababu matamshi hayatokani na ombwe tupu. Mtu anapotoa tamko mtu huwa analitolea rai, kujibu, kupinga au kufafanua. Ni kutokana na haya ndipo shairi hili “Nawaita Washairi” (uk. 3) ni jibu la S.Mohamed kwa washairi wenzake mwaka wa sabini ambapo kulikuwa na mgogoro mkubwa kati ya wanamapinduzi na wanamapokeo kuhusu muundo wa shairi.

Imebainika katika utafiti huu kwamba, tungo zilizomo katika diwani zina uhusiano na matini zingine. Shairi la “Mtu Hachagui Kazi” (uk. 23) inahusiana na hadithi ya “Mke Wangu” (uk.1-9)

Katika utafiti huu ilibanika kwamba muktadha wa mazungumzo unaathiri mawasiliano. Tumechunguza muktadha wa kitabaka, kutoleana wasia, kimaskini na muktadha kiuongozi.

5.3 Matokeo Kuhusu Maswali ya Utafiti

Usemezano unadhihirika katika mashairi ya *Sikate Tamaa* ili kufanikisha maudhui. Pili tumeweza kuyajibu maswali yetu ya utafiti kwa kutaja vipengele vya usemezano vinavyojitokeza katika

ushairi wa Kiswahili kama vile majibizano na masimulizi ya kifasihi tukilenga methali. Tatu tumeonyesha namna vipengele vya usemezano vinavyokuza dhamira ya mwandishi. Nne tumebainisha kuwa muktadha wa mazungumzo unaathiri mawasiliano.

Kimuhtasari ni kweli kwamba usemezano upo katika ushairi wa Kiswahili ili kufanikisha mawasiliano. Vipengele vya usemezano vinajitokeza katika diwani ya *Sikate Tamaa* kwa minajili ya kuendeleza dhamira na maudhui lengwa ya mwandishi. Muktadha wa mazungumzo umeathiri mawasiliano katika mashairi kwenye diwani hii.

5.4 Mapendekezo

Japo katika tasnifu hii tumethibitisha usemezano upo katika ushairi wa Kiswahili, ni mapendekezo yetu kuwa uchunguzi zaidi unahitajika katika kuendeleza na kufafanua nadharia ya usemezano. Kwanza ingawa Bakhtin (1981) anadai kwamba usemezano upo katika riwaya ya Kiswahili, hili ni jambo ambalo linastahili utafiti zaidi ili kuchunguza iwapo usemezano upo katika riwaya ya Kiswahili na umewasilishwa kwa njia gani.

Aidha ingawa Njogu (1993) na Karama (1996) na watafiti wengine wameonyesha kwamba usemezano upo katika mashairi, uchunguzi zaidi unahitajika kufanywa ili kuchunguza iwapo usemezano unaweza kupatikana katika mashairi huru na usemezano huo unajitokeza kwa jinsi gani.

Vile vile uchunguzi zaidi unahitajika kufanywa ili kuchunguza usemezano katika fasihi zilizohifadhiwa katika filamu. Pia usemezano unaweza kuchunguzwa katika tanzu za fasihi simulizi kama ngano, hadithi na vitendawili.

6.0 MAREJELEO

- Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*. Oxford University Press.
- Abdulaziz, M. (1979). *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Abedi, K. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amiri*. Dar es Salaam: E. A Publishing House.
- Ahmed, K. A. (1978). "Hutaniuwa." *katika Mulika No. 7*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili.
- Bakari, M. (2008). *Usemezano kama Mkakati wa Kufahamu Riwaya za Babu Alipofufuka, Bina- Adamu! na Mkusanyiko wa Hadithi Fupi Sadiki Ukipenda. Shahada ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.
- Bakhtin, M. M. (1981). *The Dialogic Imagination: Four Essays*. Austin: University of Texas Press.
- Bakhtin, M. M. (1984). *Rabelais and His World*. Bloomington: Indiana University Press.
- Bakhtin, M. M. (1986). *Speech Genres and other Late Essays*. Austin, Texas: University of Texas Press.
- Bennet, T. (1990). *Outside Literature*. London: Routledge.
- Biersterker, A. M. (1996). *Kujibizana. Poetic Dialogue as Political Action*. East Lansing: Michigan State University.
- Fischer, M. J. & Abedi, M. (1990). "Quranic Dialogics: Islamic Poetics and Politics for Muslims and for Us". Chicago: Chicago University Press.
- Graham, G. R. (1989). "A Dialogical Imagination" *In English Studies*. Canada: Vol XV.
- Grogan, R. (1989). " W. S Graham: A Dialogical Imagination " *In English Studies*. Canada VOL XV
- Holquist, M. (1990). *Dialogism: Bakhtin and his World*. London: Routledge.
- Indede, F. N. (2008). *Mabadiliko katika Umbo la Shairi na Athari zake*. Swahili Forum 15. (p. 80).

- Indede, F. N. (2011). *Mwanamke angali Tata katika Ushairi wa Kisasa*. Swahili Forum 18, (pp. 163-197).
- Karama, M. R. (1996). “*Al-Inkishafi: Ushahidi wa Usemezo katika Ushairi wa Kiswahili*”. *Shahada ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Kenyatta.: Haijachapishwa.
- Kea, P. (2006). *Usemezo katika Nyimbo za Taarab. Tasnifu ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Kenyatta: Haijachapishwa.
- Kiruthu. J. (2002). *The Evolving World, History and Government Course*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Marsh, Z. N. (1961). *An Introduction to the History of East Africa Third Edition*. . Cambridge University : Cambridge University Press.
- Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi. Standard Textbooks Graphics & Publishers.
- Mohamed, S. A. (1980). *Sikate Tamaa*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S.A. (1980). *Utengano*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S. A. (2002). *Jicho la Ndani*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Morson, G. S. (1986). *Bakhtin: Essays and Dialogues on his Work*. Chicago: University of Chicago press.
- Morson, G. S. (1989). *Boundaries of Genre*. Northwestern University Press.
- Mukarovsky, J. (1977). *The World and Verbal Art: Selected Essays*. . New Haven University Press.
- Munyao, K. (2016). *Uhuru wa Kishairi: Uchanganuzi wa Sikate Tamaa na Miale ya Uzalendo. Tasnifu ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.
- Murithi, J. (2002). *Usemezano katika Tamthilia ya Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Kenyatta: Haijachapishwa.
- Mwanzandi. I. (2002). *Usemezano katika Umalenga wa Kiswahili. Shahada ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Egerton: Haijachapishwa.
- Ndalu, A. & King'ei, K. (1989). *Kamusi ya Methali za Kiswahili*. Nairobi: East African Educational publishers.

- Ngolo, E. (2011). *Mabadiliko ya Kimtindo katika Ushairi wa Said. A. Mohamed. Shahada ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Kenyatta: Haijachapishwa.
- Njogu, K. (1993). *Dialogic Poetry: A contestation and social challenge in East Africa Poetic Genres. Ph.D Dissertation*. Yale University: Haijachapishwa.
- Njogu, K. (1997). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: Nairobi University Press.
- Njogu, K. (2004). *Reading Poetry as Dialogue*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njogu, K. & Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation
- Nyandoro, E. (2014). *Matumizi ya Barua katika Riwaya Teule za S.A.Mohamed. Tasnifu ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Kenyatta: Haijachapishwa.
- Pearce, L. (1994). *Reading Dialogics*. Routledge.
- Salim, H. A. (1977). "Nitakuuwa!" katika *Mulika No. 9*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Lugha ya Kiswahili.
- Tarde, G. (1989). *Communication and Social Influence: Selected Papers*. Chicago University Press.
- TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford Universty Press.
- Wafula, R. M. & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Walibora, K. & Mohamed, S. A. (2007). *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Nairobi. Moran Publishers.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.